ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Kuteuliwa
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa

11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Magogoni
13.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Donge.
14.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Kiembesamaki
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Gando
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la MaMakunduchi
18.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Jang'ombe
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Omar Othman Makungu	Mwanasheria Mkuu

22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
32.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake

38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
51.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
53.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
54.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani
55.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Jimbo la Mpendae
56. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Nafasi za Wanawake
57.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
58. Mhe. Mussa Khamis Silima	Jimbo la Uzini
59.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake

60.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
61.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
62.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
63.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Rashid Seif Suleiman	Jimbo la Ziwani
65.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
66.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
67.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
68.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
69.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
70.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
71.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
72.Mhe. Salum Amour Mtondoo	Jimbo la Bububu
73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
75. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Jimbo la Dole
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Ibrahim Mzee Ibrahim **Katibu wa Baraza la Wawalishi**

Kikao cha Ishirini na Mbili – Tarehe 19 Julai, 2011

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Naibu Waziri wa Habarí, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habarí, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa Mwaka 2011/2012. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari: Mhe. Spika, nichukue nafasi hii kukushukuru kwa dhati asubuhi hii ya leo na kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika hapa tukiwa na afya njema.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa Mwaka 2011/2012. Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 172

Ujenzi wa Barabara ya Mboriborini kwa Lami

Mhe. Jaku Hashim Ayoub (Kny. Mhe. Hamza Hassan Juma) – Aliuliza**:**

Katika Jimbo la Kwamtipura kuna barabara ya ndani inayotokea akro kwa Abass Hussein kupitia Mboriborini hadi njia ya Amani Darajabovu, kwenye Makao Makuu ya Wilaya ya CUF. Rais wa Awamu ya Sita Mhe. Dk. Amani Abeid Karume alitoa ahadi kwamba barabara hiyo itajengwa kwa lami wakati wa ufunguzi wa Skuli ya Chekechea ya Kwamtipura mwaka 2006. Vile vile wakati wa Kampeni ya Uchaguzi aliahidi kuitia lami barabara hiyo.

(a) Je, Mhe. Waziri unajua kuhusu ahadi za Marais hao kwa barabara hiyo.

(c) Je, unawaambia nini wananchi wa Jimbo la Kwamtipura kuhusu ujenzi wa barabara hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 172 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Wizara yangu inajua kuhusu ahadi ya Mhe. Rais Mstaafu wa Awamu ya Sita, Mhe. Dk. Amani Abeid Karume na ahadi ya Rais wa Awamu ya Saba, Mhe. Dk. Ali Mohammed Shein kuhusiana na kuijenga kwa lami barabara inayoanzia Saateni kwa Abass Hussein kupitia Mboriborini hadi njia ya Amani Daraja bovu kwenye Makao Makuu ya Wilaya ya *CUF* katika Jimbo la Kwamtipura.

(b) Nawaambia Wananchi wa Jimbo la Kwamtipura wazidi kuwa wastahamilivu kwani ahadi kama hizi za viongozi wetu wakuu ziko nyingi na hatuwezi kuzitekeleza zote kwa wakati mmoja. Wizara yangu inazijua ahadi zote hizo, inaziheshimu na kila tunapopata uwezo huwa tunazipunguza moja hadi nyengine. Nawaomba wasivunjike moyo na ahadi hiyo hadi muda wake utakapofika itatekelezwa.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, naomba tena kuungana na maelezo ya Mhe. Waziri aliyoyatoa wakati wa majumuisho ya bajeti yetu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, Mhe. Waziri ametwambia kuna ahadi nyingi, mimi naomba atutajie angalau ahadi nane tu walizokwisha kuzitekeleza.

Mhe. Spika: Hebu tunyooshe hili swali. Mhe. Jaku Hashim Ayoub ahadi nane hizi katika wizara hii.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ndio.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, Mhe. Rais ametoa ahadi nyingi, ahadi zake nane anazotaka kujibiwa Mhe. Mwakilishi naomba nimjibu ahadi hizo kwa upande wa barabara tu, tutaachana na ahadi nyengine alizozitoa Mhe. Rais zilizomo katika wizara yetu.

Mhe. Spika, Mhe. Rais ameahidi kujenga barabara ya lami kutoka Kitogani mpaka Ukongoroni. Mhe. Spika, Mhe. Rais ameahidi kujenga barabara ya lami kutoka Ukongoroni mpaka Bwejuu. Mhe. Spika, Mhe. Rais ameahidi kujenga barabara ya lami kutoka Cheju/Jendele/Unguja Ukuu. Mhe. Spika, Mhe. Rais

ameahidi kujenga barabara ya lami kutoka Kiboje mpaka Kizimbani. Hizo ni kwa upande wa Unguja. Mhe. Spika, kwa upande wa Pemba Mhe. Rais ameahidi kujenga barabara za lami nyingi.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri na kumbukumbu nzuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa barabara alizozitaja ni barabara ya Amani/Mtoni na ambayo kwa kweli hivi sasa iko chini ya ujenzi wa UUB kwa ufanisi mkubwa na barabara hii ni ya njia mbili kama ile ya Magomeni.

(a) Je, barabara hii ikimalizika itawekwa taa kama barabara za mjini ambazo zimo kwenye mpango wa serikali.

(b) Kwa kuwa njia aliyoitaja Mhe. Hamza Hassan Juma ni barabara ya ndani. Kwa kuwa teknolojia ya *Ro-mix* ilifeli. Je, Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kwamba kuna haja sasa Mfuko wa Barabara kujenga njia hii ili kumpa hadhi Mhe. Rais kutokana na ahadi yake.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, wajibu wa wizara yetu ni kujenga barabara na kumalizia mradi huu kwa ukamilifu. Suala linalohusiana na barabara nadhani wenyewe ni watu wa Manispaa. Suala la uwekaji wa mataa nadhani wizara yetu tulichukue kwa kushirikiana na mamlaka husika wakiwemo Manispaa katika uwekaji wa huduma hiyo muhimu katika uendelezaji wa mji na barabara zetu.

Mhe. Spika, swali (b) ni kwamba wenzetu wa Mfuko wa Barabara wana malengo hayo ya kutaka barabara zote kujengwa kwa kiwango cha lami. Kinachowakwaza ni kile kile kilio chetu cha serikali nzima, ni uwezo na upatikanaji wa fedha. Fedha zikiruhusu sidhani kama itakuwa kikwazo kwao kutekeleza huo ujenzi wa lami.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando): Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akijibu swali la msingi alisema kwamba ahadi za Mhe. Rais ziko nyingi kwenye masuala haya. Je, ni lini hasa barabara hii ya Kwamtipura itajengwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, katika jibu mama nilieleza kwamba pamoja na maelezo hayo niliyoyatoa naungana na maelezo aliyoyatoa Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano wakati wa majumuisho ya bajeti hii. Mhe. Spika, Mhe. Waziri katika majadiliano yale alisema tutaangalia hali ikiruhusu bajeti ijayo *inshaallah* tutaingiza mradi huu.

Nam. 183

Uhaba wa Walimu wa Masomo ya Sayansi

Mhe. Mjumbe aliyeuliza swali hili ameliondoa.

Nam. 38

Mchango wa SMZ Kituo cha Afya Kambi ya Vitongoji

Mhe. Saleh Nassor Juma – Aliuliza:

Kwa kuwa Kambi ya Jeshi la Wananchi iliyopo Vitongoji katika Jimbo la Wawi imeanzisha hospitali ya kisasa inayotoa huduma kwa askari pamoja na raia zaidi ya asilimia 80 kutoka katika vijiji vya jimbo hilo na majimbo jirani kama vile Ole na Chake Chake. Na kwa kuwa SMZ haitoi mgao wa madawa kwa hospitali hii.

Je, ni lini Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaunga mkono juhudi za kizalendo zinazofanywa na wapiganaji wetu kwa kuipatia hospitali hiyo mgao wa madawa.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu:

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 38 kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, kwanza napenda kulipongeza Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) kwa kuunga mkono juhudi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kutoa huduma za afya karibu na wananchi.

Mhe. Spika, napenda kumfahamisha Mhe. Mwakilishi kwamba katika kuunga mkono na kuthamini huduma zitolewazo na hospitali ya JWTZ Vitongoji, Serikali kupitia Wizara ya Afya imetoa wafanyakazi wa maabara na watoa huduma kwa akinamama wajawazito na watoto chini ya miaka mitano *(MCH).* Aidha, Wizara inasambaza chanjo kama kawaida, pia inawashirikisha wafanyakazi wakiwemo Maafisa wa Jeshi katika Warsha, Semina na Mikutano mbali mbali inayoandaliwa na Wizara.

Mhe. Spika, pamoja na hayo, Wizara yangu imekuwa na utaratibu wa kuwapatia dawa, alimuradi tu wanafuata utaratibu wa maombi ya dawa hizo sambamba na ule utaratibu unaotumiwa na vituo vyetu vya afya vya serikali.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa hospitali ya *Ali Khamis Camp* ni hospitali yenye vifaa vya kisasa na wanapima mpaka ukimwi. Kwa sababu yupo daktari mzuri ambaye ana kiwango cha *Assistant Medical Officer*, wanapima ukimwi lakini hawaruhusiwi kutoa dawa za *ARV*.

Je, ni lini wizara hii itawaruhusu hospitali ile kuweza kutoa dawa kwa wale waathirika wa ukimwi, huku ukitilia maanani kwamba hospitali nyengine hazina hata *Assistant Medical Officer* lakini wanatoa *ARV*.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, utoaji wa dawa za *ARV* unahitaji maandalizi, unahitaji timu ikamilike. Katika vituo ambapo *ARV* zinatolewa watu wale timu ile imekamilika na wameshapata mafunzo. Tunachokihitaji ile *ARV* isitolewe tu, tunahitaji daktari anayekuwepo kituoni saa zote. Huduma za *ARV* zinaambatana na maandalizi kwanza kunatakiwa kuwe kunatolewa ushauri nasaha tupate mtu huyo, tunatakiwa tupate mtu ambaye kwanza anahusika na wajawazito na watoto wachanga ili waweze kupimwa virusi vya ukimwi, baadae hatua ya tatu ndio tunatoa dawa kwa wale wanaohusika.

Hatua hizo pale kituoni zimo katika maandalizi na bado hazijakamilika. Tatizo kubwa lilioko pale huyo daktari anayemsema si mtu anayepatikana saa zote, ni mtu ambaye anakwenda akirudi ana shughuli nyengine nyingi ambacho hicho ni moja kati ya kikwazo tunachokipata kuweza kumuandaa yule daktari kutoa huduma za *ARV*.

Pale ambapo jeshi litapata mtu wa kukaa hospitali saa zote na kumuacha yule ambaye ana dhamana nyengine, hapo tunaweza tukakamilisha maandalizi ya taratibu na *ARV* zitatolewa. Huduma za *ARV* zitatolewa wakati maandalizi yatakapokuwa yamekamilika.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, ni kigezo gani kinachotumika katika wizara yako ili kuzipatia hospitali mgao wa dawa na ni hospitali zipi.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, dawa za Wizara ya Afya ziko katika makundi mawili. Kundi la kwanza ni zile zinazotolewa na serikali, kundi la pili ni zile zinazotolewa na *DANIDA*. Dawa zinazotolewa na *DANIDA* zinatolewa kwa vituo vya serikali tu hayo ndio makubaliano yetu. Dawa zinazotolewa na Wizara ya Afya ndizo zinazoweza zikagawanywa kwengineko kokote.

Kwa hiyo, mara nyingi *Ali Khamis Camp* huwa inapenda wapate mgao ule unaotolewa na *DANIDA*. Tumeshawaeleza kwamba kwa makubaliano ya wafadhili wetu hilo haliwezekani. Lakini dawa za serikali fuateni utaratibu, ni maombi tunachokihitaji zipo tunawapatia.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, ni wafanyakazi wangapi na lini wamepelekwa katika hii hospitali hii ya *Ali Khamis Camp.*

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, wafanyakazi waliopo pale kwetu ni wawili, kile ni kituo cha jeshi wao wanatakiwa kama kituo walikifungua wawe na wafanyakazi wao. Hospitali ya Bububu wana wafanyakazi wa kutosha, pale wanapopungua wakituomba tunawapa. Pemba tuna wafanyakazi wachache tulionao tumewapa, sisi wetu walioko pale ni wawili wengine wa jeshini mimi siwafahamu.

Nam. 185

Mradi wa Maji Mkoa wa Mjini/Magharibi

Mhe. Viwe Khamis Abdalla – Aliuliza**:**

Wakaazi wa Mjini Unguja na vitongoji vyake walipata matumaini ya kuepukana na tatizo la maji kutoka mpango mkuu wa mradi wa maji Mkoa wa Mjini Magharibi. Mradi huo umeshamalizika kwa awamu zipatazo mbili na mafundi wamesharudi makwao lakini tatizo la maji limebaki pale pale.

(a) Mhe. Waziri kwa nini tatizo la maji halijamalizika Mjini. Ni kiasi gani cha fedha za msaada na za SMZ zimetumika.

(b) Katika hali kama hiyo wahisani wetu Serikali ya Japan wanasemaje.

(c) Viongozi wa majimbo ya Mjini kwa umoja wanachimba visima vyao katika majimbo. Je, hali hii ya kueneza visima kila pembe sio hatari.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati – Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 185 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, naomba kukubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba matarajio ya wananchi wengi wa Mjini Unguja na vitongoji vyake ni kuwa kukamilika kwa mradi wa maji wa Mkoa wa Mjini/Magharibi ambao umefadhiliwa na Serikali ya Japan kupitia *(JICA)*

kungeliondosha kabisa tatizo la maji katika Mkoa huu. Lakini kutokana na uchakavu wa mtandao wa usambazaji maji katika mji wetu, ujenzi holela uliokithiri katika vianzio vya maji, pamoja na ujenzi holela wa mahodhi ya chini ya ardhi ambayo mengi yao hayakujengwa kitaalam na yanavujisha. Hivyo, husababisha upotevu mkubwa wa maji, husababisha kupungua kiwango kikubwa cha maji katika Mkoa wa Mjini Magharibi.

Aidha, mradi huu umegharimu Tshs. Milioni 960 ikiwa ni mchango wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Tshs. Bilioni 32 kama ni mchango wa wahisani.

(b) Mhe. Spika, wafadhili wetu Serikali ya Japan bado wana nia ya kuendeleza kuisaidia Zanzibar na tumeshasaini juu ya mradi wa kuijengea uwezo Mamlaka ya Maji na mazungumzo yanaendelea kuona namna ya kuangalia uwezekano wa kusaidia miundombinu.

© Mhe. Spika, Wizara yangu ina jukumu la utoaji wa huduma ya maji na usimamizi wa rasilimali maji. Katika kutekeleza kazi hizo kumekuwa na changamoto nyingi ikiwemo uchimbaji holela wa visima ambavyo huchimbwa bila ya mpangilio.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Je, Mhe. Waziri, Serikali kwa kupitia wizara yako imejipanga vipi katika kuondoa tatizo hili ili wananchi wajenge matumaini ya kuondokana na usumbufu huo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar lengo ni kuwasambazia wananchi wake maji safi na salama. Lakini gharama hizi za kuliondoa kabisa tatizo la maji Zanzibar ni kubwa mno kwa sababu ili liondoke tatizo hili basi inalazimika zipatikane dola za Kimarekani bilioni 120.

Kwa hiyo, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika kuliangalia hili itatenga kila baada ya mwaka mmoja bilioni 40 na baada ya kufikia miaka mitatu tunategemea tatizo hili la maji litaondoka katika visiwa vya Unguja na Pemba.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa tunajua kwamba kuna matatizo ya maji katika jiji hili la Unguja. Kwa kuwa wanaopata shida ni akinamama pamoja na wanafunzi.

(a) Je, Mhe. Waziri atakubaliana nami kwamba kuna haja ya kufanya utafiti wa hali ya juu ni sababu zipi ambazo zinawafanya wananchi wa Unguja Mjini wasipate maji.

(b) Kwa kuwa wenye fedha nyingi huwa wanachukua maji kwenye mabomba makubwa ili kuhakikisha kuwanyima wale ambao hawana uwezo. Je, Wizara yako suala hili inalijua.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kama nilivyoeleza kwamba kinachosababisha moja ni uchakavu wa *line* zetu pamoja na miundombinu hii ya maji. Isitoshe ujenzi holela wa mahodhi yanayojengwa bila ya wataalam hili ni moja ambalo linasababisha.

Mhe. Spika, jibu (b) Serikali kupitia Wizara yangu inalijua hilo na itajitahidi kulifanyia kazi ili tuhakikishe kwamba wananchi wanafaidika na huduma hiyo, pamoja na kuwafuatilia hawa watu wenye pesa wanaochimba visima kiholela na kuliondoa tatizo hili.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, nakushukuru kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kabla ya mradi huu mkubwa wa maji kutoka Japan kuja kufanya kazi hapa Zanzibar kulikuwa na maeneo walikuwa wanapata maji masaa 24 bila ya kukosekana. Lakini baada ya mradi huu kujengwa sasa maeneo yale yamekosa maji na hayapatikani kabisa.

(a) Je, Mhe. Waziri hili linasababishwa na nini yale maeneo yaliyokuwa yakipata maji na sasa hayapati.

(b) Je, Wizara yake imefanya utafiti ikajua ni maeneo gani yaliyokuwa yakipata maji na sasa hayapati.

(c) Je, kama inajua ni lini itayafanyia kazi kuwarudishia wananchi hao maji waliyokuwa wakiyapata hasa ukizingatia sasa hivi maji kama wanatakiwa wachangie.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kwanza nakubaliana nae kwamba ni kweli kuna maeneo maji yalikuwa yanapatikana kikamilifu lakini baada ya kuongezeka kwa wananchi au majengo au matumizi ya maji hayo basi yamepungua kupatikana kwake.

Mhe. Spika, pili ni kwamba serikali inalijua hilo kupitia wizara yangu na mpango ilionao kwa sasa hivi ni kuongeza miundombinu na uchimbaji wa visima ili tatizo hilo liondokane na wananchi.

TAARIFA

Mhe. Spika: Kabla hatujaendelea kuna taarifa moja ndogo. Waheshimiwa Wajumbe kati ya mafanikio yaliyoko chini ya wizara hii kuna wajasiriamali wengi ambao wanafanya shughuli mbali mbali na wapo baadhi ambao waliniomba waje waoneshe bidhaa zao hapa. Sasa hawapo hapa juu lakini wako pale nje wameniomba nisome taarifa yao ili muelewe walioko hapo nje ni nani.

Waheshimiwa Wajumbe miongoni mwa shughuli za Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika ni kusaidia wananchi katika shughuli za kiuchumi ambazo wanazifanya kwa ajili ya kuwasaidia kupunguza umaskini wa kipato. Miongoni mwa shughuli hizo ni ujasiriamali, shughuli hizo hufanywa na vikundi na watu binafsi mmoja mmoja.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika anafuraha kuwaarifu Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza pamoja na wote wanaoshuhudia kwamba hapo nje kuna vikundi mbali mbali vya wajasiriamali pamoja na watu binafsi wanaojishughulisha na kazi mbali mbali. Vikundi viliopo hapo nje ni *Mwanakwerekwe SACCOS Bank*, Chaza Mpya, *Masika Bites*, Nia Safi, *ZAPHA+*, Imani, Umoja ni Nguvu, Rabi Tuongoze, Ukweli Vitendo, Tamu Tamu, Neema Haichezewi, Mam Jopas, Mnazi ni Mkombozi, *Kijichi Spice*, Amani na Utulivu, *Kwaalinatu Tailoring Centre* na kikundi cha AMISUFI. Vile vile wako wajasiriamali binafsi ambao ni Bi Jina Faki Moh'd na Bi Salama Akida. Waheshimiwa Wajumbe, Mhe. Waziri anaomba kwa wakati wenu mpite kwenye vibanda hivyo ambavyo wajasiriamali hao kwa ajili ya kuona shughuli zao na kubadilishana nao mawazo ili kuwatia moyo. Kama mkitaka kununua mnaweza kununua pale pale kwa kuwasaidia ndugu zetu hao. Waheshimiwa Wajumbe, hiyo ndio taarifa niliyotumwa kwa kupitia kwa Mhe. Waziri, ili wenzetu hao tuwaunge mkono na kuwaendeleza katika shughuli zao.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wanachi Kiuchumi na Ushirika kwa mwaka wa fedha 2011/2012

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuweza kufika katika ukumbi huu tukiwa wazima. Pili nikushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii nikiwa mchangiaji wa mwanzo katika wizara hii kwa asubuhi ya leo.

Mhe. Spika, kwanza naomba nianze kwa kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mhe. Waziri kutokana na kuteuliwa kwake kusimamia wizara hii ambayo ni muhimu na wizara hii ni mpya na ina changamoto nyingi. Mhe. Rais kaliona hilo na akamteuwa Mhe. Haroun kwa kuamini kwamba Mhe. Haroun anaweza kuanzisha kitu, akakisimamia na kukiendeleza hadi kikawa.

Sisi wawakilishi ambao tumewahi kufanyakazi na Mhe. Haroun katika kipindi kilichopita, hatuna wasi wasi kwamba hili anaweza kulisimamia vizuri, akaianzisha wizara hii na ikafanya kama ambavyo tulitegemea. Pili nimpe pole kwa sababu hili jukumu ni zito, kukubali kwamba jukumu la uwezeshaji kila tulivyosikia kuwa kuna wizara mpya ya uwezeshaji, kwa kweli tulikuwa na fikra tofauti. Sisi tunafikra tofauti na wananchi wetu wanafikra tofauti. Inawezekana ikawa ni tofauti na vile ambavyo tunafikiria. Lakini yote hiyo inatokana na ukweli kwamba wananchi wanajenga matumaini makubwa katika wizara hii.

Mhe. Spika, baada ya pole hiyo kwa jukumu zito lililomuelekea Mhe. Waziri, nimpongeze sasa Mhe. Rais. Mhe. Rais katafsiri kwa vitendo utekelezaji wa ile dhana ya kuondosha na kupunguza umaskini. Kwa sababu tatizo kubwa linalokabili uchumi wetu hivi sasa ni tatizo la umaskini unaowakabili watu wetu. Tunaposema umaskini tunakusudia umaskini wa kipato. Kwa hivyo, baada ya kuona kuwa hii ni ajenda ya kitaifa na lazima ipate jawabu, ndio Mhe. Rais akaamua kuunda wizara hii ambayo ni Wizara ya Uwezeshaji. Kwa hivyo, mimi nampongeza Mhe. Rais na naamini kwamba ndani ya kipindi cha miaka mitano basi tutashuhudia mageuzi kwa vitendo katika utekelezaji wa dhana hii.

Mhe. Spika, kama nilivyosema kwamba tatizo letu linalowakabili watu wetu majimboni ni tatizo la umaskini tena umaskini wenyewe ni wa kipato. Umaskini wa kipato unakwenda kwenye tafsiri ya moja kwa moja, ni tatizo linalotokana na ukosefu wa ajira. Vijana wengi kila mwaka wanamaliza elimu zao na wengi wao kwa asilimia kubwa sana ingawa hatuna takwimu sahihi na naomba wizara inayohusika kila mwaka itupe taarifa ya watu wanaomaliza skuli na wanaoingia katika soko la ajira, ili tupate kupima uzito wa tatizo la ajira katika nchi yetu. Sisi kama wawakilishi hatuna takwimu hizo na ni muhimu sana.

Katika kuangalia maendeleo ya wizara hii na katika kuangalia tatizo la lililomo katika sekta ya ajira, ingekuwa ni vyema kila mwaka tukapatiwa uzito unaokabili sekta ya ajira. Kwa hivyo, Mhe. Spika, tatizo ni ajira na tatizo linalotokana na ajira, linatokana na ile dhana ya kujiajiri. Ni kweli kwamba serikali uwezo wa kuajiri ni mdogo na sasa hivi ni lazima tukubali kwamba ili vijana wetu wapate ajira ni lazima tuwaelekeze katika kujiajiri binafsi. Mimi

nadhani kwa asilimia 90 tuwaelekeze vijana wetu waelekee katika soko la ajira binafsi.

Mhe. Spika, ili vijana waelekee katika ajira binafsi mambo mawili ni muhimu sana kuzingatiwa na serikali. Kwanza kuna haja kubwa sana watu kupatiwa elimu, lazima watu wapatiwe elimu kwamba kuna umuhimu wa kujiajiri na kujiajiri binafsi kunaweza kukaleta tija zaidi kuliko kuajiriwa na sekta ya umma, hii ni elimu inahitajika kutambulika. Likishatambulika hilo kuwa kuna umuhimu wa vijana wetu kujiajiri katika sekta binafsi basi wapewe ile elimu hasa inayowafanya wakaweza kujiajiri katika sekta binafsi.

Baada ya kupata elimu hiyo katika kubwa katika sekta hii ni suala zima la mitaji. Watu wanaweza wakajiajiri lakini siku hizi kila kitu ni lazima upate mtaji. Unapoelekea kwenye kilimo ni lazima upate mtaji katika kukiendeleza kilimo, unapojielekeza kwenye biashara ni lazima upate mtaji katika kuelekea kwenye biashara na unapoelekea kwenye uzalishaji wa aina yoyote, iwe ni viwanda vidogo vidogo au vyovyote ni lazima upate mtaji. Kwa hivyo, katika dhana hii ya kujiajiri mambo mawili Mhe. Spika, ni muhimu sana na ni lazima serikali na wizara iyazingatie.

Mhe. Spika, suala la kuandaa programu ya kuwaelimisha vijana, vile vile kuwe na programu mahususi inayohusiana na suala la kuwawezesha vijana wetu na wananchi wetu kuweza kupata mitaji. Itakuwa ni dhana iliyokuwa sio sahihi kuwaambia watu wajiajiri lakini cha kujiajiria hakuna, kitu kinachoweza kuwafanya wajiajiri ikawa hawana uwezo, basi itakuwa serikali bado haijafanya kitu. Katika hili tunaweza tukaliangalia katika bajeti ya wizara hii. Maana yake tukizungumzia uwezo wa wizara katika kutekeleza mambo mawili ya elimu pamoja na mitaji, tutaangalie wizara imejiandaaje katika kufikia azma ya mambo hayo mawili. Katika hili tunaweza kuangalia katika bajeti ya maendeleo.

Mhe. Spika, bajeti ya maendeleo katika wizara hii imetengewa milioni 90. milioni 90 kila mmoja aziangalie, tuziangalie na tuzigawe. Soko la ajira mahitaji ni makubwa sana. Leo tunachukua milioni 90 kuifanya kuwa ndio bajeti ya maendeleo katika hii, kila mmoja aangalie kuwa ni namna gani tunafanya utani katika suala hili. Milioni 90 hizi milioni 40 zinakwenda katika maendeleo ya vyama vya ushirika na milioni 50 zinakwenda katika kuzijengea uwezo taasisi zinazosimamia sheria za kazi. Hizi milioni 50 sizihesabu, hizi hazimo kwa sababu hizi ni kujenga *capacity building* ya mambo ya sheria za kazi. Tunazoweza kuziangalia angalau kwa jicho la pembeni ni hizi milioni 40 ambazo zinaelekezwa katika vyama vya ushirika. Katika hizo milioni 40 kama zitatolewa basi zitakazopatikana ni milioni 20, sina hakika hata hizo milioni 40 kuwa zitapatikana kama tutakavyo dhihizinisha katika Baraza hili.

Kwa hivyo, kwa fikra zangu tumeunda wizara lakini bado hatujajiandaa. Mimi nadhani Mhe. Spika, kama serikali iko-*serious* na kupunguza suala zima la uwezeshaji wa wananchi na serikali itakapofika katika hatua ya kuweza kuiwezesha wizara hii. Basi Mhe. Spika, katika kipindi cha miaka mitano hatuwezi kuzungumzia suala la umaskini katika nchi. Kila mmoja atakapoweza kujiajiri mwenyewe, ama katika kilimo, biashara au katika uzalishaji wa aina yoyote ndani ya miaka mitano katika serikali hii ya Dk. Shein, suala hili tutakuja kuleta hadithi nyengine katika Baraza hili. Lakini kwa utani huu tunaoufanya wa kuweka milioni 90, mimi nasema huu ni ubishi ambao hatupaswi kuufanya kabisa katika suala hili.

Sasa tunachokitegemea ni nini, ikiwa wizara haina uwezo wa kuwawezesha wananchi, tunachokitegemea ni nini. Tunachokitegemea ni tukimbilie kwenye mifuko iliyoanzishwa, kuna mfuko ule wa kujitegemea, kuna na mifuko ile maarufu ya AK na JK, hapo ndipo penye kimbilio, pengine hapo ndipo panaweza kuwa na jawabu la Mhe. Waziri atakapokuja, kwamba tegemeo letu katika kuwawezesha wananchi ni kupitia mifuko hii ya JK na AK pamoja na mfuko wa kujitegemea.

Mhe. Spika, katika suala la mifuko hii mimi nanasihi sana kama utolewaji wake uwe ni wa uwazi, kuna tatizo kubwa sana na fedha nyingi sana zimeanishwa hapa kwamba mifuko imetoa mabilioni, lakini *reality* mabilioni haya tutayaangalia pahala gani. Mabilioni yamo katika vitabu, ngapi zimetolewa na ngapi zimo mikononi na ngapi zimesharejeshwa yote yameelezwa. Lakini sasa sisi tuliopo majimboni tunazitafuta zikowapi na sasa kuna dhana ambayo inawezekana sio sahihi kwamba fedha hizi zinachukuliwa na watu wachache tu ambao ndio wakubwa, hazifiki kwa walengwa. Sasa hili linatufanyia fitna katika majimbo. Maana yake wananchi wanaposikia kwamba kuna fedha za AK na JK basi hutuandama sisi viongozi wao. Mimi nikijiangalia nipate wapi au nizitowe wapi, muongozo uko wapi kama mwakilishi wa kuweza kuwasimamia wananchi kuweza kuzipata fedha hizi. Utasikia tu aah! Maana yake kuna huyu na huyu wamekwenda wilayani. Lakini ukweli ni kwamba hufiki pahala ukaziona kwamba fedha hizi ziko pahala gani.

Kwa hivyo, moja kati ya nasaha yangu kwa Mhe. Waziri, tunaomba kuwe na uwazi wa hali ya juu katika urejeshaji wa hizi pesa na uwazi wa kwanza kabisa, tunataka Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho basi atufanyie kazi moja. Atupe orodha asitupe *figure* ili na sisi tuweze kujenga hoja vizuri kwa wananchi wetu, nitakapofahamu mimi kama wananchi wa Chake Chake katika kijiji fulani au katika shehia fulani wamepewa watu hawa, hivyo nina uwezo mzuri wa kwenda kuwaeleza. Namuomba Mhe. Waziri hata nina uwezo wa kwenda kuwaambia jamani hizi fedha ni fedha za kuzunguka kwa hivyo ni lazima zirudishwe, nina uwezo wa kuwaambia hivyo. Lakini leo nikiwa sijui

chochote katika jimbo langu nitawezaje kuisaidia wizara, nitawezaje kumsaidia Mhe. Waziri.

Kwa hivyo, nadhani katika uwazi wa kwanza Mhe. Waziri atakapokuja atuletee orodha. Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati hapa wanatuletea orodha ya watu wote wanaodaiwa kila nyumba, fulani bin fulani huyu yuko nyumba nambari fulani anadaiwa kiasi fulani na deni lake la mwisho kalipa siku fulani na sasa anadaiwa kiasi fulani. Ikiwa Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati wanaweza kufanya hivyo, kwa nini na Mhe. Waziri asiweze kulifanya hilo.

Kwa hivyo, katika kumsaidia Mhe. Waziri pamoja na serikali katika kutekeleza azma nzuri hii, namuomba atakapokuja atupe orodha za kila mkoa, kila wilaya na kila shehia ili tuweze kujua ni nani na nani na nani katika jimbo langu kafaidika, nani na nani wanadaiwa kiasi fulani ili mwakilishi nipate nguvu ya kwenda kumuhimiza kurejesha mikopo ili na wengine nao waendelee kufaidika.

Mhe. Spika, jengine katika suala hili la mikopo, mimi nakubali kwa sababu sidhani AK sasa hivi. JK bado anaendelea katika madaraka sidhani kama atatoa fedha nyengine katika hili. AK sasa hivi hayupo, sijui nini hatima ya mfuko huu, kama utakuwa ni *sustain* au atakuja Ali Mohammed Shein na yeye ataanzisha wake sijui. Lalini kwa vyovyote vile itakavyokuwa tunategemea mifuko hii, fedha zilizomo katika mzunguko nzizo hizi hizi ambazo zitatumika kuiendeleza mifuko hii kwa fikra yangu.

Sasa kama hivi ndivyo, kuwe na suala zuri la fedha hizi kurejeshwa na hili Mhe. Waziri itatuwia ngumu ni lazima tukubali kama wawakilishi, wabunge na madiwani katika maeneo ndio wahimili wa mifuko hii, sisi ndio wenye wananchi. Kwa hivyo, ikiwa sisi ndio wenye wananchi ni lazima mtushirikishe katika hili ndio litawaondoshea shida nyingi katika suala hili. Mhe. Spika, kwa kadiri fedha zitakavyoongezwa lakini katika hali yoyote ile tunadhani kuwa mifuko hii fedha zilizomo katika mzunguko ndizo hizo hizo zitakazotumika katika kuwaendeleza wengine.

Ushauri wangu ni kwamba kwa vyovyote vile Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri atushirikishe wawakilishi katika utoaji wa mifuko hii, kwa sababu itatusaidia sisi wawakilishi binafsi, vile vile itamsaidia yeye katika kuirejesha mifuko hii ili na wananchi wengi zaidi waendelee kunufaika katika upatikanaji wake.

Mhe. Spika, jengine wizara hii kama ilivyo ni wizara ya uwezeshaji, tunaitegemea wizara hii iwe ndio *centralized* ya mambo yote ya ajira yanayohusiana na sekta binafsi, mambo yote ya kujiajiri yanayotokana na

kujiwezesha katika uzalishaji na mambo mengine ni wizara hii inayohusika. Kwa hivyo, kwa msingi huo mimi nadhani mambo yaliyokuwa yanahusiana na ajira katika *department* nyengine. Maalim Rashid jana alizungumza hapa, kuna taasisi nyengine ambazo mambo haya yanachukuliwa yanachomekwa katika wizara nyengine.

Kwa mfano vyuo vya elimu ya amali. Hivi vyuo vya elimu ya amali kwa sababu kule ndiko tunakowapata vijana katika suala lile kama mambo ya uvuvi, mambo ya mifugo na mengine, kwa nini vyuo vya amali visiwekwe katika wizara hii. Huku ndiko tunakotengeneza ajira, kwa hivyo ikiwa ndiko tunakotengeneza ajira hususan katika ajira binafsi, ilikuwa ni vyema kabisa vyuo vya elimu ya amali viwekwe huku, huku ndiko kwenye vijana na ndiko kunako kinamama na vitu vyengine. Kwa hivyo, ilikuwa ni sahihi kabisa kuzichukua hizi taasisi zote zinazohusika na mambo ya kuandaa vijana ili waweze kuingia katika soko la ajira, wangeingizwa katika wizara hii ingeweza kuwasaidia.

La mwisho Mhe. Spika, nimuombe sana Mhe. Waziri suala la elimu ambalo ni kitu muhimu sana, pahala pa kwanza pa kuanzia elimu mimi nadhani ni kupitia kwa wajumbe wako. Mhe. Waziri katika hili asiwe mbahili, usiwe mbahili kabisa. Sisi ndio wenye wawakilishi wa majimboni, majimbo yote 50 yamo humu, wanawake wote wa Zanzibar wamo humu kwa kupitia wawakilishi wao wa wilaya na mikoa. Kwa hivyo, pahala pa kwanza pa kuweza kutao elimu juu ya suala hili, nadhani ilikuwa uanze katika Baraza hili. Hivyo Mhe. Waziri naomba ukunjuwe mkono kidogo ili utuelimishe namna ya uanzishwaji wa vikundi vya ushirika. Hivi vikundi vya ushirika vinaanzishwaje pamoja na SACOSS. Sisi tutakapopata elimu hiyo basi inakuwa ni rahisi zaidi kwenda majimboni kwetu na kuweza kulielimisha hili na sisi ndio wasaidizi wako katika hili.

Vile vile Mhe. Waziri utuelezee namna ya kuwa na sifa ya kuweza kupata mikopo inakuwa vipi, ili na sisi tuweze kuendelea kuvihamasisha vikundi vyetu vilivyopo majimboni na wao waendelee kufaidika. Kwa sababu ikiwa hakuna usimamizi mzuri, mwisho wa siku tunaweza kujikuta ni majimbo machache tu ndio yamefaidika na mambo kama haya na majimbo mengine yakabakia hayana ufaidikaji wowote.

Kwa hivyo, mwisho kabisa naomba Mhe. Spika, Mhe. Waziri alizingatie hili la kuwaelimisha wajumbe wako, sisi ndio msaada kwake na sisi ndio msaada kwa serikali. Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii kwanza nimshukuru Mhe. Waziri kwa kuwasilisha bajeti yake mbele yetu. Pia

niwashukuru watendaji wake ambao wameshirikiana naye mpaka kufikia kutuletea bajeti yake hii.

Mhe. Spika, kwanza niwapongeze wizara kwa kuwapa mafunzo wafanyakazi wake. La kupongeza zaidi ni kwamba watu hawa waliopata mafunzo ni mchanganyiko wa jinsia, nipongeze tu kwamba kina mama sasa hivi wanasema hawako nyuma, nimeona idadi yao ni wafanyakazi 10 wanawake na 10 wanaume. Kwa hivyo, niseme kwamba tujipongeze sisi wanawake na tunasema ni wakati wetu na sisi kwenda sambamba na kinababa.

Mhe. Spika, nizungumzie suala la Mfuko wa AK na JK. Kama walivyokwisha kutangulia wajumbe wenzangu kwamba wizara hii ni ya uwezeshaji, na kama ni hivyo basi ni wakati wa kusema kwamba wizara hii itekeleze yale majukumu, isiwe kwamba ni mazungumzo tu au ikawa ni ndoto au kuwa ni chanzo cha wananchi wetu huko majimboni kutuuliza maswali mengi tu. Kwa kweli jana niliuliza swali hili kwa masheha wangu, lakini mpaka sasa hivi watu wanalisikia kwa masikioni tu, mpaka sasa hivi Jimbo la Amani halijapata kuwezeshwa kwa kupitia mfuko huu.

Kwa kweli watu wamehamasika sana na hasa kinamama wamehamasika sana na kuna vikundi vingi vimeanzishwa, ingawa vingine mpaka sasa hivi vimo katika mpango tu, hawajapata hata usajili na usajili pia ni kikwazo. Mara nyingi watu wakienda kwenye usajili wanapata maelekezo kuwa wanatakiwa waanzishe *SACOSS* za shehia, ambapo inakuwa ni ngumu kwao wao. Kwa sababu ukianzisha *SACOSS* ni watu tofauti na tabia tofauti kwa hivyo inakuwa ni tatizo kidogo na kwa sababu kwenye vyama vya ushirika inabidi mnatoa sheha zenu ili kujiwezesha wenyewe kama akiba zenu mnaweka. Kama mtu atakopa basi nyinyi wenyewe muwe mna aminiana ili pawe na ufanisi mzuri. Kwa hivyo, kwenye usajili inakuwa ni tatizo kidogo.

Mhe. Spika, nikiendelea nimeona hapa kuna huu mfuko wa JK na AK nikitizama hapa kwenye chati yake kuna milioni 17,112,186, lakini kufikia mwezi wa Mei, 2011 zimetoka bilioni 1,463,640, sasa sijui hii *figure* inai-*formulate figure*, sijui kama hapa imekosewa au ni matatizo ya uandishi sielewi. Kwa hivyo, Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho yake anifafanulie suala hili.

Vile vile kwenye chati hiyo hiyo nimetizama, kwa sababu nimekwenda na fani yangu ya Uhasibu. Nimetizama katika mikopo nimeona kuwa ile 2010/2011 vifungu vyote kulikuwa hakuna kitu, hii inanipa wasi wasi kwamba kama ni idara ilikuwa inahitaji iwe na vifungu vyote vile ambavyo vinastahiki iwe nayo imepata, lakini utaona kwamba hakuna isipokuwa kulikuwa na milioni 47,626,728 mfuko wa kujitegemea. Sasa hapa nilikuwa nina wasi wasi kwamba

hivi vifungu vyengine na hii ni idara kamili na kwa sababu tuna *triggering instruction*, ikiwa idara nzima haikuwa na fedha mambo mengineyo itayapata wapi. Kwa hivyo, hili nalo ni suala ambalo nimeliona hapa. Kwa hivyo, Mhe. Waziri atakapokuja hapa anifahamishe vizuri, pengine mimi sikufahamu au sikuielewa.

Mhe. Spika, idara hii inaongozwa na kijana Mkurugenzi Kamisheni ya Kazi. Kwa kweli ni idara ambayo imeonesha makadirio yao ya mapato hapa kwa mwaka wamevuka lengo. Idara hii ni muhimu na iangaliwe katika bajeti zake na iwezeshwe. Kwa sababu mtu akifanya vizuri basi na yeye atendewe vizuri. Idara hii hapa wamevuka lengo na kupata asilimia 142, niseme kwamba wamefanyakazi nzuri na hili ndio lengo, hapa panaonesha patakuwa na ufanisi mzuri.

Mhe. Spika, kwa kweli wananchi wamehamasika sana na wizara hii. Mhe. Waziri nikuombe sana na hasa kinamama wamehamasika sana, kwa sababu mambo mengi yanatusimamia sisi kinamama majumbani mwetu huko, watoto wetu wanataka kwenda mashule na tuna mambo chungu nzima. Kwa hivyo, Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri kwa sababu malengo yake ni kutuwezesha wananchi, matumaini yangu ni kwamba kama ilivyo wizara yenyewe jina lake. Mhe. Spika, naomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atueleze vizuri na njia ambazo tupite kama wawakilishi ili tufikie huko tunakokwenda.

Mhe. Spika, mimi pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Amani, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia, ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Ahsante sana Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kunipa fursa hii kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika.

Mhe. Spika, kwanza nichukuwe fursa hii kumshukuru kwa dhati Mhe. Waziri na watendaji wake kwa ujumla kwa kutuletea kitabu hiki ambacho kimejaa malengo na madhumuni hasa ya kuwawezesha wananchi wetu kiuchumi, hususan wale walio katika kipato cha chini.

Mhe. Spika, pia nichukuwe fursa hii kulishukuru sana Shirika la Kazi Duniani (*ILO*), pamoja na *NGOs* kwa jitihada zao kubwa wanazochukua za kuwapitia wananchi wetu na kutaka kuwawezesha kwenye mfumo mzima wa kujiondoa na umaskini.

Baada ya hayo Mhe. Spika, mimi nitakwenda moja kwa moja katika hayo hayo mambo ya vikundi vya *SACCOS*. Mhe. Spika, ninacho kilio kikubwa na *SACCOS* ambazo zipo na haziwi endelevu.

Lakini nashukuru kwenye kitabu chake Mhe. Waziri kuhusu malengo yake mwaka 2011/2012 kilio changu kidogo kimepungua kwa mambo mawili hapa. Kwanza kwa kuanzishwa *SACCOS* benki 14 nashukuru kwa hilo, pia kutaka maafisa wake kukagua mahesabu ya Vyama vya Ushirika ambavyo ni kilio kikubwa kwa Vyama hivi vya *SACCOS* havina uwezo huo na huwa zinafanyakazi zake kwa njia ya kubahatisha. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nataka nimueleze Mhe. Waziri kwa sababu siku moja nilimuuliza swali langu pale kuhusu *SACCOS* mbili ikiwemo Wadiri *SACCOS* na Pemba *SACCOS* ilioko Pemba. Kwa kweli nilimwambia kuwa hizi ni *SACCOS* kubwa ambazo zimejumisha vikundi vingi sana, vikundi ambavyo lengo lao ni kuwezeshwa. Kwa mfano, Kusini Mkoani, Kaskazini Wilaya ya Micheweni, Wilaya ya Wete wanashiriki katika kundi hili zima la Pemba *SACCOS*.

Lakini kutokana na matatizo vikundi hiki mwanzo vilianza uzuri tu, hivi sasa vimekabiliwa na matatizo na imefikia pahala vikundi hivi vimeshindwa kutoa mikopo kwa matatizo. Kwa hivyo, nataka nimueleze Mhe. Waziri tatizo ambalo kuwa linawakabili *SACCOS* hizi.

Kwanza ni kuhusu mkopo wa muda mfupi kwa wananchi wetu ambao ni wafanyabiashara wadogo wadogo huwa unawapa matatizo sana, ukilinganisha na wafanyakazi wa serikali ambao kuwa wao wanapata kipato kidogo, lakini wao wanaweza kwenda kuchukua mkopo pengine benki na kupangiwa mkataba kuwa alipe miaka mitatu.

Sasa kwa upande wa mfanyabiashara mdogo yeye anatakiwa alipe mkopo ule kwa muda wa mwaka mmoja na hili ni tatizo, suala hili ndilo lililopelekea vikundi hivi kufikia mpaka leo kushindwa hivi sasa kutoa mikopo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, tatizo jengine mabenki nazo zinachangia hasa hii benki ambayo watu wanachukua mkopo huu kama hiyo Waridi *SACCOS* na Pemba *SACCOS* ilikuwa wao mkataba wao ni mwaka mmoja.

Sasa inapofika mwaka mmoja huwataka viongozi wale wa kikundi kile wa-*renew* mkataba ule kwa kuwapa mkopo mwengine, jambo ambalo hawajamaliza mkopo wanaochukua na kuwalazimisha ku-*renew* mkataba ule, ili kuwapa mkopo mwengine na hatimaye kama unataka shilingi milioni 30, inamaana deni la nyuma lote linakatwa na kinachobakia huwa hakikidhi haja kwa kutoa mikopo kwa wanachama wengine.

Kutokana na hali hiyo, hupelekea vikundi hivyo badala ya kujiandaa na marejesho sasa wanajiandaa kukatwa fedha zile na huku wanawakopesha watu wengine ambao bado hawajapata mikopo fedha zile huwa hazikidhi haja.

Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, vikundi hivi aviimarishe kwa sababu ni vikundi vizuri tu, tatizo ni kwamba hawana pahala pa kuchukua mkopo ambao wataweza kukidhi haja zao.

Vile vile suala la ufuajiliaji ni tatizo kwa wale viongozi, kwa sababu wakati wale viongozi hawalipwi basi kufuatilia benki moja kwa moja kwa ajili ya kuzungumza matatizo yao na wale viongozi waliopo katika kikundi kile. Kwa kweli hili ni tatizo Mhe. Waziri, basi tunakuomba kupitia kwa Mhe. Spika, uvisimamie vikundi hivi au *SACCOS* hizi, ili ziweze kuwa endelevu na kupata mikopo.

Pamoja na hayo, nakuomba tena Mhe. Waziri sana kwani vikundi hivi bado viko hai ingawa baadhi wa wanachama wengine wameshakufa, lakini achukue jitihada ya kuvielimisha vikundi hivyo.

Mhe. Spika, ninalo ombi langu jengine kwa sababu najua anayewezeshwa ni kuwa mwenyewe anachokile chanzo, ili kifanye awezeshwe kwa ajili ya kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Katika Wilaya ya Micheweni kuna wananchi wengi sana ambao wanajishughulisha na upandaji wa mwani. Kwa kweli upandaji wa mwani tayari tumeshasikia kwamba unayo matumizi ya aina nyengine kama vile utengenezaji wa sabuni. Kwa hivyo, tunakuomba Mhe. Waziri kupitia wakulima hawa wa mwani uwawezeshe na lengo lako ni kuanzisha vikundi.

Kwa maana hiyo, nakuomba Mhe. Waziri, suala hili la uzalishaji wa mwani wananchi uwawezeshe kwa kuutumia mwani kwa mambo mengine, yaani badala ya kuuza wautumie mwani kwa kufanyia sabuni, ili kuweza kupata mahitaji yao mengine.

Kwa hayo machache Mhe. Spika, mimi pamoja na wananchi wangu wa Wilaya ya Micheweni naunga mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Abdalla Moh'd Ali: Ahsante Mhe. Spika, na mimi asubuhi hii kunipa fursa ya kuchangia kidogo katika hotuba ilioko mbele yetu. Kwa kweli kama walivyosema wenzangu waliotangulia kwamba wizara hii ni mpya na kwetu sisi ni ngeni na tumejenga matumaini makubwa kwamba mwaka ujao tutawaona wananchi wetu wengi wameshatononoka.

Mhe. Spika, nikianza na mchango wangu kuhusu masuala ya ajira na kwa taarifa wizara hii ndio shughuli zake hasa hizi ajira binafsi. Hivi karibuni katika majimbo yetu Mhe. Spika, tulipata kuulizwa mswali mengi kuhusiana na ajira ambazo labda zimetokea katika nje za kigeni.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, atueleze kidogo kwa sababu siku hizi kumeingia watu wa aina tofauti. Je, anajua kwamba kuna ajira ambazo vijana wetu labda wataondoka katika nchi hii na kwenda nchi ngeni kufanya ajira hizo? Vile vile vijana hawa watakuwa ni wangapi watakaokwenda hizo nchi za nje? Kuna utaratibu gani uliofanyika katika kuwapata vijana hao? Je, sijui vijana hao walitakiwa wawe na sifa gani mpaka wakapatiwa nafasi hizo?

Mhe. Spika, nikiendelea Rais Mstaafu alisema kwamba "Zanzibar ni Njema Atakaye Aje" kwa maana hiyo wakaingia wageni wengi katika nchi yetu. Kwa hivyo, wengi hao wakaingia katika Sekta ya Ajira Binafsi. Kutokana na hali hiyo, watu wetu wengi sana wakaanza kupoteza ajira kwa maana ya kuwa elimu yao ikawa ni ndogo haiwaruhusu kushindana na wale ambao walioiingia katika nchi yetu.

Katika suala hili napenda nimuombe Mhe. Waziri kwa miaka ambayo inayokuja tukawa na utaratibu maalum tukaweka au kila taasisi iwe inapata au inaruhusika kuajiri wazalendo wangapi na wageni wakapewa nafasi zao ngapi kutokana na pengine utaalamu wao walionao. Mhe. Spika, kama hatutofikia hatua hiyo nafikiri labda itafika wakati ajira nyingi zitakuwa zinachukuliwa na wageni tukijua kwamba sisi Wazanzibari kiwango chetu cha elimu bado kiko duni na wengi hatuna taaluma ambazo labda zinahitajika katika sekta tofauti.

Vile vile upo utaratibu wa kutafuta ajira nchi za nje na sisi vijana wetu wanataka waondoke kwa ajili ya kwenda kutafuta ajira nchi nyengine tofauti. Sasa inapotokea hivyo Mhe. Spika, ni lazima kuwe kuna Hati za Kusafiria na huwezi ukaondoka tu bila ya kupata Hati ya Kusafiria. Kwa mfano, tunao vijana ambao wamesomea mambo ya *Navigation* huwa wanataka labda wakimbilie nchi za Afrika ya Kusini au Ugiriki ama Egypt kwa ajili ya kwenda kujitafutia ajira.

Lakini wanapokwenda katika idara zinazohusika na kutoa Hati za Kusafiria wanasumbuka sana, kwa vile yeye hana udhibitisho kwamba anakwenda kufanyakazi sehemu fulani, yaani anakwenda kubahatisha tu hivyo inakuwa ni vigumu kwake kumpatia hati hiyo.

Kwa hivyo, ninaomba kuwe na utaratibu maalum ambao utahakikisha hawa vijana wenye viwango fulani vya elimu au amali fulani, basi wakapatiwa Hati

za Kusafiria bila ya usumbufu, ili na wao wakapata fursa ya kwenda kutafuta ajira hizo nchi tofauti ulimwenguni.

Mhe. Spika, hivi sasa mimi namuomba Mhe. Waziri abadilishe msimamo au mtazamo kuhusu mikopo na uwezeshaji wa wananchi. Mimi ninao uzoefu kidogo wa nchi ambazo zimefuata mfumo wa Ujamaa na tukisema tunaunda Vyama vya Ushirika basi huwa inanikumbusha mbali. Kwa kweli nilibahatika kusoma katika nchi ambayo ilifuata Mfumo wa Ujamaa na sisi ninavyofahamu kwamba nchi yetu ilifuata Mfumo wa Ujamaa kwa kipindi kirefu.

Mfumo huu mara nyingi haukuleta jita, kwa sababu mara nyingi watu waliofuta ujamaa au ushirika basi wali-*fail* njiani na sisi tumeshayaona hayo, kwa sababu tulikuwa na Maduka ya Ushirika, Vikundi vya Ushirika na vingi vili-*fail* kutokana na mitazamo ya wale wananchi waliokuwemo kwenye vikundi vile. Mhe. Spika, mpaka hivi sasa kuna baadhi ya vikundi vime-*fail* kwa sababu hiyo.

Kwa mfano, inawezekana ukamwambia mwananchi wewe leo ni zamu yako katika Kikundi cha Ushirika kwenda kukata majani kwa ajili ya huyu ng'ombe wetu, lakini akaona aa! Mimi siwezi kuacha kwenda baharini, kwa sababu ajira yangu hasa kuu ni ile ya kwenda kuvua ndio inayonipatia chochote na huyu ng'ombe ana miezi tisa au kumi pengine ndio apate tija fulani tena ni ya maziwa tu. Sasa ule umuhimu hauoni kwamba aende pale kwa ajili ya kutafuta yale majani. Kwa hivyo, vikundi vile vinavunjia njiani bila ya kufikia yale malengo.

Sasa ninaomba wizara ikaliangalia hilo Mhe. Spika, kwamba vikundi vyetu haviko na lengo moja. Kwa hivyo, ikiwa tunashikilia kila siku tuendee katika Vikundi vya Ushirika hatutofika mbali. Kwa maana hiyo, ni lazima tutafute mfumo mwengine hivi sasa, yaani tuwe na mwelekeo mwengine.

Katika hilo pia Mhe. Spika, ni kwamba leo tunao vijana wengi ambao wamejiajiri wenyewe na wao wanayo mitaji mikubwa sana yao binafsi. Kwa hiyo, hii mitaji ambayo tunavipatia vikundi vyetu ni midogo na wala hawawezi kuwa-*compete* katika soko liliopo.

Kwa mfano, tunawapatiwa watu au wananchi kuku 100 kwa kwenda pengine kuzalisha mayai, lakini utakuta tajiri fulani anao kuku 1,000. Kwa hivyo, yeye uwezekano wa kuliuza yai *tray* shilingi 5,000/= upo, lakini wetu sisi kutokana na zile gharama zilizopo utakuja kuona mwisho hawezi kuliuza yai lile chini ya shilingi 5,000/=.

Kwa hivyo, ule mtaji tunaowapa vikundi hautoshelezi kuweza kufanya *challenge* huko nje au na wananchi wengine. Kwa maana hiyo, lazima tuwe na mwelekeo mwengine, kwa sababu hizi shilingi 50,000/= au 100,000/= tunazowapa hazitoshelezi ni bora tukatafuta utaratibu mwengine.

Mhe. Spika, katika hilo niseme labda sisi lengo letu ni kumshughulisha yule mwananchi na wala sio kumpa ajira, yaani *occupation*. Kwa maana ya kwamba kama tunahesabu ajira, sawa wananchi wanashughulika kwa sababu kila mmoja utaona huyu anafuga mbuzi na yule anasuka ukili na huyu anafuga ng'ombe na yule anakwenda kwenye chaza.

Lakini matokeo yake ukienda kupiga hesabu za kiuchumi mtu yule hanufaiki chochote, yaani time *allocated*, *energy* iliyotumika, basi inatukia mwisho *result* baada ya mwaka yeye pengine yuko *minus*. Sasa mtu yule baada ya kumwambia *ok* endelea na kazi yako uliyokuwa nayo huko awali, basi anaacha kwa sababu akili yake haimruhusu kwenda mbali, yaani hafikiri sana kiasi akaweza kufanya uchambuzi wa kina kuhusu uwezeshaji tuliompa na matokeo yake tuna-*much time*.

Kwa hivyo, kwa mfumo huu tutatumia zaidi ya miaka 10 tunawapa watu pesa na sijui kama wanazirudisha, kwa sababu urudishaji wake ndio hivyo hivyo. Lakini lazima tubadilike katika hili si hivyo hatuwezi kwenda pahala, kwa maana hiyo tunawezeshana tunawa-*occupy* watu, ili wawe *busy*, lakini kama ni *business* wanayoifanya.

Mhe. Spika, mimi naona nimalizie hapo, isipokuwa namsubiri Mhe. Waziri nione na mimi katika Jimbo langu la Mkoani watu wangu wamepatiwa mkopo wa kutosheleza, ili kuweza kuendeleza shughuli zao za uvuvi.

Kwa hivyo, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mhe. Ashura Sharif Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, nami kunipata nafasi hii ya kuweza kuchangia hotuba ilioko mezani wakati huu. Awali ya yote sina budi nimshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu *Subuhanahu Wataala* aliyetujaalia uhai na uzima tukawepo hapa asubuhi hii kuweza kutekeleza majukumu yetu kwa maslahi ya taifa letu. *(Makofi)*

Vile vile sina budi nikushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunipatia na mimi nafasi hii ya kuweza kutoa mchango wangu mdogo.

Mhe. Spika, pia sina budi nitoe pongezi zangu za dhati kwa Mhe. Rais wa Zanzibar kwa kuunda wizara hii. Naamini kwamba Mhe. Rais ameona sasa

imefikiwa wakati wa kuwakwamua Wazanzibari katika hali ya umasiki uliokithiri. *(Makofi)*

Pamoja na pongezi hizi nimpongeze Mhe. Waziri kuteuliwa kwake kuishika nafasi hii. Naamini kwamba Mhe. Rais hakufanya kosa amejua kwa uhakika Mhe. Haroun Ali Suleiman kwa kucheza *center half* hii na kuweza kufunga magoli. *(Makofi)*

Hivyo basi Mhe. Spika, ningependa kumueleza Mhe. Waziri kwamba wanawake wengi wa Zanzibar wanaishi katika mazingira magumu kabisa ya umasikini uliokithiri, suala hili alifahamu kwamba wapo hususan walioko kwenye vijiji. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nimepata taarifa rasmi kwamba hivi sasa kuna watoto wengi wanaoishi katika mazingira magumu ambao wazazi wao wanashindwa kuwatimizia mahitaji yao. Kwa hivyo, ni imani yangu kwamba uwezeshaji kupitia wizara hii italiona hili na italifanya kwa moyo mkunjufu na ufanisi kwa kutizama hasa haki pale inapohusika ifike.

Baada ya utangulizi wangu huo Mhe. Spika, sasa nianze na mchango wangu. Kwa kweli nianze mchango wangu kwenye ukurasa wa 18 katika kifungu 24 kuhusu utekelezaji wa malengo ya Idara ya Uendeshaji na Utumishi. Mhe. Spika, hapa sikuwa na la kusema isipokuwa ni kuwapongeza sana kwa utaratibu mzuri uliotumika wa kuwapa mafunzo wafanyakazi wake ya kitaalamu wafanyakazi 20. Lakini katika 20 hao akigawa sawa kabisa wanawake 10 na wanaume 10, Mhe. Waziri huu ni mfano mzuri na unastahili kupewa pongezi ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nikiendelea kwenye ukurasa wa 24 kifungu cha 29 kuhusu Malengo ya Idara ya Uendeshaji na Utaratibu wa *Program* ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

Kwa kweli hapa Mhe. Waziri amezungumza malengo yake ya kiutafiti, malengo ambayo kama watayafanya kweli na kufanya utafiti katika maeneo muhimu ya kiuchumi na kubaini fursa ya eneo fulani, basi wanaweza kufanya kitu fulani kwa ajili ya kujikwamua kimaisha. Hivyo, naamini kwamba ni kweli kabisa *program* hiyo ikitekelezeka basi Wazanzibari tunaweza kufikia lengo.

Mhe. Spika, katika maeneo yetu tunatofautiana sana. Kwa mfano, huwezi kumlinganisha mwananchi wa kijijini akawa sawa na wa Mjini Magharibi, kwa sababu wa kijijini pengine miradi yake inaweza kuhusiana na kilimo na ufugaji, lakini wa Mjini Magharibi itahusiana sana na biashara.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri aichukue fursa hii kuweza kufanya utafiti wa kina na kuona ni kina nani? Wapi na eneo lipi linahitaji kuwezeshwa kwa utaratibu upi?

Nikiendelea na mchango wangu katika ukurasa wa 25 kifungu cha 31 kuhusu Idara ya Mikopo. Mhe. Spika, hapa ndipo ambapo ninao mchango kidogo, kwa sababu masharti ya mkopo kwa hakika yalikuwa magumu mno, kwani ni masharti ambayo wale wanaokwenda kukopa walikuwa hawaelewi hasa yale masharti, yaani wanaingia kichwa na miguu pengine fulani amekopa na mimi nikakope.

Kwa kweli hawakupata taaluma ambayo iliwaonesha wazi kwamba masharti haya itakuwa hivi na vile na hatimaye wakapewa taaluma, ili kuweza kuelewa na kuiendeleza ile mikopo waliyopatiwa. Mhe. Spika, kwa sababu imetolewa mikopo mingi, yaani fedha nyingi lakini urejeshaji wake umekuwa mgumu mno, kwa sababu miradi yao haikuwa endelevu na wala haikuwa na taaluma ya ubora wa uzalishaji na badala yake ilikuwa ni ya kufilisika na hatimaye kushindwa kurejesha mikopo hii na kufikia hatua ya kwamba wengine waweze kukosa kwa wakati.

Sasa niende kwenye Mikopo ya AK na JK. Mhe. Spika, mikopo hii ilitolewa lakini haikuzingatiwa ukubwa wa miradi yenyewe ya wale ambao wamekopeshwa au kukaguliwa kuonekana kwamba wanayo miradi gani na inahitaji nini, isipokuwa fedha hizo zilikuwa zinakwenda kuchukuliwa kwa utaratibu ambao haukuwa mzuri, kwani fedha hizi ukiziangalia hazikuenea kabisa. Kwa hivyo, wanawake wengi walikosa kupata fedha kupitia mikopo hii ya AK na JK kwa kukosa kabisa taaluma hiyo.

Mhe. Spika, mimi nilibahatika kwenda Pemba katika ziara za Kamati tuliwakuta wale ambao walikopeshwa, yaani wanaitwa wadaiwa sugu. Kwa kweli hawa kwa kutoelimishwa wameshindwa kulipa na wanasema hizo ni fedha za baba yetu Mhe. Rais ametupa wacha tutumie.

Kwa hivyo, ni dhahiri inaonesha hawakupewa taaluma mapema, kwamba huu ni mkopo unaowataka nyinyi uwawezeshe, ili muweze kujiendeleza kiuchumi pamoja na miradi yenu na hatimaye murejeshe na wenzenu waweze kutumia hili fungu na miradi yenu inahitaji utaalamu. Kwa maana hiyo, ubunifu wa miradi hawakupata taaluma hiyo na bila ya taaluma hakuna kinachoendelea.

Sasa nizungumzie kuhusu Idara ya Ushirika. Mhe. Spika, Vyama vya Ushirika ni vingi vilivyosajiliwa na amevitaja Mhe. Waziri. Lakini vyama vyote ambavyo vipo hapa haviko hai, isipokuwa ni vichache ndivyo vinavyoendesha shughuli zake za kiushirika na kwa manufaa ya wale wanachama wake. Kwa

kweli vingi havina manufaa kwa wanachama isipokuwa uongozi wa juu tu wa hivi Vyama vya Ushirika.

Kwa hiyo, hili aliangalie kwa kina aweze kujua kwamba aanze usajili mpya na kuvipitia hasa hivi Vyama vya Ushirika kuona vile vinavyofanyakazi ni vipi na vipi havipo pamoja na kutoa fursa nyengine kwa vile vikundi vipya vya wanachama kuona na wao wanafanyiwa usajili kwa ajili ya kuorodheshwa na kuweza kupata na wao mikopo ili kuendesha ushirika wao.

Mhe. Spika, sasa niende kwenye ukurasa wa 53 kifungu cha 65 kuhusu Idara ya Ajira. Mhe. Spika, kero kuu la Wazanzibari ni kusema kwamba vijana wetu wengi wamekosa ajira. Kwa hivyo, idara hii ingawa ni mpya, lakini jukumu lake ni zito tena ni muhimu, ambalo linahitaji kuangaliwa kitaalamu kabisa, kwani Wazanzibari wengi kwa sasa au nchi yetu imeingia katika kuwekeza katika masuala ya utalii.

Kwa kweli vijana wetu wengi sana wanajifunga kwenye kuingia katika ajira hizi, lakini wakiwa hawaelewi chochote kutokana na ajira hizi, kwa sababu ya dhiki ya maisha wanakwenda moja kwa moja bila hata ya kufunga mikataba ya kazi. Kwa hivyo, huwasababishia migogoro na matatizo mbali mbali kwenye mahoteli yetu wakafukuzwa na kukosa haki zao.

Mhe. Spika, naiomba Idara hii ya Ajira iwaangalie zaidi na kuwapa taaluma vijana, pale ambapo wanataka kuajiriwa wajue utaratibu wa kufunga mikataba. Nadhani wapo Wazanzibari wachache ambao wanafanyakazi katika mahoteli, lakini wananyanyasika sana kwa sababu hawakufunga mikataba, wanafukuzwa kiholela, wanakosa haki zao za msingi.

Kutokana na hali hiyo, inakuwa ni sawa, kwa sababu ni muda mfupi anaajiriwa kama vile kwa wiki, lakini hatimaye anafungwa na wala hakuna haki yake na pengine ametumikia miaka miwili au mwaka mmoja na kuondoka.

Lakini pia jengine ni kuangalia kwamba wakati wa ajira zinapotokea hapa kwetu nchini basi tuwaangalie hawa wanaoajiriwa ndio wazalendo, kwani wazalengo ndio wenye haki ya kuajiriwa kwanza kwa sababu hii nchi ndio yao, tofauti iliyopo sasa katika sekta hii ya ajira walivyoachiwa wenyewe tu wawekezaji basi muwekezaji akija anakuja na wafanyakazi wake wote katika mali. Wazanzibari mara nyingi kazi zao ni za bustani zile ambazo ndogo ndogo na hazina mikataba, hivyo huwapeleka kupata kipato kidogo na hatimae kufukuzwa na kukosa haki zao za msingi.

Mhe. Waziri kwa hili ninakuomba ulisimamie uzungumze na hawa wenye mahotali kwa sasa na ufanye usajili maalum kuwajua Wazanzibari ambao

wanafanya kazi katika mahoteli ambao hawakufungishwa mikataba uwaelewe, utakapowaelewa naamini kwamba wakapata na taaluma basi nadhani pia itakusaidia na wewe kuona kwamba vijana hawa wanaajiriwa kwa muda mrefu na kupata ajira endelevu na kuondoa ile kero yetu ambayo imetukabili hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo nimwambie Mhe. Waziri nimeangalia hapa katika hitimisho lake anasema ili Wizara yake ya Kazi na Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika, basi anataka aidhinishiwe Tanzania Shs. 1,080,000,000 kwa matumizi mengineyo. Kitabu chake kama nimekifahamu nililiona hilo, lakini anasema kwa kazi za maendeleo ninaomba niidhinishiwe Shs. 90,000,000 hapa kidogo nikapatwa na wasi wasi, nikajuliza Mhe. Waziri kwenye miradi ya maendeleo kuna hii 90 milioni lakini kwenye kazi za kawaida kuna bilioni moja. Hii ni idadi ndogo mno kazi za kawaida zina fedha kubwa lakini kazi za maendeleo kwa ajili ya kuwawezesha hawa wambao tunawakamua kiuchumi hiyo ni fedha ndogo sana.

Ningemuomba Mhe. Waziri pangine kwa kutokufahamu kwangu sikuelewa kulikoni lakini anipe maelezo ili niweze kufahamu utaratibu huu ili niweze kuona kweli hakika ile dhana na dhamira ya kuwakomoa wananchi kiuchumi inatimia. Baada ya kusema hayo ningemuomba Mhe. Waziri aviangalie vikundi vya vijijini vilivyopo, wanawake huko wamechoka sana na maisha wako taaban hali zao Wilaya ya Kaskazini (B) ni wilaya moja ambayo watu wake masikini lakini kiutaalam ukiiangalia ina uwezo mzuri wa kujikwamua lakini pengine kwa sababu nyenzo zilikuwa hazipo naamini kwamba kupitia kwako Mhe. Waziri utalifanya hilo na wanawake hao wanajenga matumaini kwako na tunakusubiri kwa hamu kubwa.

Hivyo basi kwa niaba ya wanawake wa Wilaya ya Kaskazini (B) naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Spika, kunipatia nafasi hii asubuhi hii kutoa mchango wangu mdogo katika Wizara hii ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika. Kwanza nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kutuwezesha asubuhi hii kukutana hapa kuendelea na kazi zetu za kawaida katika ukumbi huu.

Pili nimshukuru Mhe.Waziri kwa hotuba yake hii kwa vizuri na tumemuelewa vizuri, mawaziri wote ni waswahili wazuri kila aliyekuja anajua Kiswahili kutoka kwa mwezake, kila mmoja katunga kitabu chake vizuri kuliko mwenzake. Lakini Mhe. Waziri huyu katunga kitabu kizuri zaidi kuliko wengine wote waliopita, nimekisoma kitabu hiki kajiweka yeye mwenyewe

Waziri pamoja na watendaji wake wote wenzake wameweka kwa jina tu, kama ningekuwa mwalimu huyu ningempa maksi nyingi zaidi kuliko waliopita.

Mhe. Spika, kwa hivyo kwanza nimpongeze kwa muundo tu wa kitabu chake halafu nimpongeze kwa muda mfupi aliokaa katika Wizara hii na mapokezi ya nchi mbali mbali kutoka nchi mbali mbali, na taasisi mbali mbali za kimataifa kama alivyoweka katika kitabu chake kuwa katika afisi yake kapokea wageni kutoka nchi mbali mbali na taasisi mbali mbali za kimataifa. Hii ni kuonyeshea kuwa Wizara yake ina ua ambalo linavuta au linavutia watu waje kumuona, kwa sababu wanakuja kumuona imani yangu miongoni mwa mazungumzo yake ni kuwashawishi na kuwaomba kuweza kuisaidia wizara yake ili kuwakwamua wananchi wetu kiuchumi, yaani kuomba misaada kwa ajili yake na hatimae misaada hiyo iwafikie wananchi wetu nadhani hiyo ndio dhamira yake.

Kadhalika binafsi katika kipindi hicho kifupi pia umefanya ziara za nchi mbali mbali na kuhudhuria mikutano mbali mbali ya kimataifa, pia nadhani humu alimokwenda hendi kutalii lakini anakwenda kwa ajili ya kuitafutia uwezo wizara yake, kama dhana yangu ni ya kweli kwa hivyo nampongeza sana kwa hili, lakini kama sio ya kweli basi mara nyengine afanye ziara hizo kwa ajili kuitafutia uwezo zaidi wizara yake. Kwa sababu wizara yake inahusiana na mambo mengi kwa watu ama wale waliokuwa hawana kipato au wenye kipato cha chini.

Mhe. Spika, mimi nije katika Idara ya Mikopo na kwenye malengo yake, lengo lake moja ni kuratibu na kutoa mikopo ipatayo elfu moja, kwanza niwapongeze kwa hilo lengo tu kama itafikiwa au laa ni suala jengine, lakini kwa kuwa wajaribu kuweka lengo la kujaribu kutoa mikopo elfu moja wanaonyesha kuwa wamekusudia kuwakwamua wananchi wetu kutoka katika hali ngumu ya kiuchumi waliyokuwa nayo na kuwanyanyua kidogo. Lakini ningeomba huu mfumo wao wa mikopo kidogo ubadilike tutazame hali halisi ya matumizi ya nchi yalivyo, leo hii kumpa mtu kumsaidia shilingi hamsini elfu, au laki moja kwa wafanya biashara wadogo wadogo kwa kweli sio kumsaidia lakini ni kumdumaza na unamtaka baada ya mura mrupi aurejeshe.

Sijui shilingi hamsini elfu faida yake itakuwa kiasi gani kwa siku mpaka aweze kurejesha mkopo na mtaji ubakie, kwa kuwa hajimudu kimaisha pengine akifanya huo mradi aliokusudia akanunulia mapemba akakaa hafanyi lolote kwa sababu mradi wenyewe hauna kiwango cha kuweza kumkwamua kiuchumi, kwa hivyo tunavyotoa mikopo zaidi hii ya mtu mmoja mmoja hii sio vizuri sana kumsaidia mtu mmoja mmoja kwa sababu hafiki pahala. Lakini kama tunafanya hivyo uwe ni mkopo ambao utaweza kumuwezesha kama ilivyo Wizara yenyewe kuwawezesha wananchi Kiuchumi, kwa hivyo tumpe

mtu jambo ambalo litamuwezesha kujikwamua katika hali aliyo aendelee kidogo.

Mhe. Spika, nizungumze kidogo kwenye Idara ya Ushirika, lengo lake moja ni kusajili vyama vya ushirika, kuvifanyia ukaaguzi wa mahisabu hili ni jambo muhimu, kwa sababu kama kuna chama tumekikopesha na tukakaa kimya bila ya kukikagua hatimae ndio vyama vyetu vinakufa pole pole kwa sababu ndani yake huwa kuna wanachama wengine au wafanyakazi waliopewa dhamana wakapoteza imani au uhamisho kidogo badala ya ile fedha kuiendeleza katika ushirika husika wakaanza kupunguza kidogo kidogo na kuingiza katika mifuko yao na hatimae, chama unakikuta kimekufa. Kwa hivyo huu utaratibu wa kufanyia ukaguzi wa kimahisabu ni utaratibu mzuri na ningeomba ufanywe uhakika, ili ile dhana iliyokusudiwa na serikali ifikiwe.

Mhe. Spika, mimi kuna vitu hapa tunaviita vyama vya ushirika kuna vyengine tunaita *SACOSS* ningeomba mimi binafsi kwa sababu si mshirika lakini ni watu ambao washirika na wana *SACOSS* nichukue kidogo tofauti ya mambo yake mawili haya.

Mhe. Spika, idara hii ya ushirika katika mwaka huu wa fedha wa 2011/2012 imejipangia kuanzisha nafasi za ajira wamesema hapa watu 3,500 sijui ajira hizi wao watazitoa katika sehemu zipi, kutoka kwenye hizi *SACOSS* zetu au kwenye vikundi vya ushirika kiufupi nataka nijue hizi nafasi zilizotajwa watatengeneza katika nyanja zipi. Kwa sababu uzoefu uliopo kwenye vyama vyetu vya ushirika takribani vyote vilifika pahala vikafilisika, vilifika hapala vikapoteza uwezo wa kujiendesha wanajiendesha pale tu ambapo serikali au taasisi fulani imeweka mkono wake, mkono wa mtu huyo ukiondoka nao hali kadhalika vinaondoka.

Kuna miradi kadhaa ya *TASAF* miradi ya *PADEP* na hizi huingia katika njia za ushirika, mara tu wahisani hawa wanapoondoa mkono wao miradi hii takriban asilimia thamanini inakufa na ishirini tu pengine ndio inayweza kujiendeleza. Kwa hivyo tujue pale tunaposaidia watu tuwape elimu ya kuweza kuendesha hiyo taasisi ambazo tunataka ziwakwamue, vyenginevyo itakuwa tunatumia pesa anakuja mfadhili mwengine tunawapa wanatumia wala ile dhana iliyokubaliwa na serikali inabakia pale pale watu wanabakia katika umasikini.

Mhe. Spika, mikopo hii inayotolewa ningeomba ibakishe mfumo hapa nyuma ilikuwa inatolewa kwa watu maalum, kwengine unasikia tu kuna misaada afulani inatolewa kwa vikundi lakini hivi vikundi vilikuwa vinaundwa na watu maalum wanakusanyana kwa kuwa wamesikia kuna mfuko unataka kutumika watu wanakusanya wanapeyana hiyo mikopo, lakini kwa kuwa hapa tumebadilika Wazanzibari tumekuwa wamoja sasa misaada na mikopo hii Mhe.

Spika, ije kwa uwazi zaidi kuliko ilivyokuwa ikija hapo kabla ya tulivyokuwa hapa leo katika baraza hili, iwiwe kunong'onezana iwe fursa zije kwa wote. Kwa sababu mimi naamini haki sawa kwa wote.

Mhe. Spika, fursa yoyote ya serikali itakapokuja tugawane tuwache kugawana kwa nyuma lakini tugawane sote kwa sababu ni wamoja na ndio maana Mhe. Omar Ali Shehe hapa kasema kuwa tunapata masuala kwa sababu inakuja misaada katika vikundi ambavyo sisi havitujui wala hatuvijui, lakini sasa tunataka tujuane ni vikundi ambavyo vimo katika majimbo yetu. Kwa hivyo tungeomba mfumo wa ushirika ubadilike ili tuweze kushirikisha wazanzibari wote katika majimbo yetu mle ambamo tunatumikia.

Mhe. Spika, sasa nije kwenye kamisheni ya Kazi *point* yao moja waliyosema ni kuimarisha masuala ya usalama na afya sehemu ya kazi, wapo wafanyakazi wengi zaidi wale wanyonge waliojiajiri katika ajira binafsi kama kuchonga matofali watu wa Vitongoji na Mwambe wale wanafanya kazi katika mazingira magumu ya vumbi zito, sehemu wanayofanya hakuna usalama wa kutosha. Kwa sababu hapa tumetaja usalama wa kazi na afya zao tuwashawishi wafanyakazi hawa kila baada ya muda mfupi kupima afya zao kutokana na kazi ngumu na nzito wanazofanya.

Hata walimu kwa sababu bado mfumo wetu wa kusomesha ni ubao na chaki, mwalimu anafonza vimbi la chaki kila siku na Wazanzibari tulio wengi hasa sisi wa shamba mtu hatizami afya yake mpaka jioni ata kwenda hawezi, kwa hivyo tungewaelimisha wafanyakazi wetu kama dhamira ya idara hii ya kazi ilivyo kuweza kuwatizama afya zao na usalama wao wa kazi.

Mhe. Spika, pia kamisheni hii imezungumzia kutokomeza ajira za watoto, nashukuru kwa hili wameliona lakini mimi nataka nijue hizi ajira za watoto ni zipi na mtoto katika ajira ni yupi na akifanya nini itakuwa hii ni ajira, kwa mfano watoto wa pwani pwani ukenda watoto wadogo baada ya watu kununua samaki wao wanaomba kuchukua samaki wale kwenye kupata na kutengeneza, Je, ile ni aina fulani ya ajira.

Kuna sememu nyengine sijui mtoto ni mwenye umri wa miaka mingapi watoto wanakaa sehemu za masoko kudoea kubeba mizigo kupeleka hapa na pale ni ajira za aina hizi zinazokusudiwa au tunapozungumza ajira ya watoto ni ajira ya aina gani, kuna watoto kutokana na umasikini wa kule majumbani wazee wao wanatengeneza biashara ndogo ndogo wanamtwika mtoto kapu la badia,l kwenda skukli kuuza . Je, hii ni aina fulani ya ajira hii ajira ya watoto ningeomba nipatiwe tafsiri yake na wanaifanya katika mazingira yepi.

Lakini kwa kuwa kazi kubwa ya Idara hii ni kutokomeza kwa hivyo hawa watoto wenye mtindo huu au wale ambao wanaishi katika mazingira magumu zaidi, kama umri wao unatosha kupata ajira iwe hizi ajira ambazo wizara hii inakusudia kuzitengeneza zilengwe kwao au bado ni wadogo hawawezi kufanya kazi basi Idara hii iwashawishi waweze kurudi maskuli na kusoma. Vyenginevyo wataendelea kubakia mitaani na kufanya hizo ajira ambazo serikali haiku tayari kwa watoto hao wafanye ajira hizo.

Mhe. Spika, baada ya mchango huu mfupi kwa kuwa nimeanza kumsifu vizuri Mhe. Waziri kwa hivyo ningelimuomba kule Jimboni kwangu Mtambile viko vikundi kadhaa vya ushirika ningekuomba ukunjue mkono wako nami vikundi vyangu uvione, zaidi vile ambavyo viko katika shehia yangu mwenyewe Shehia ya Mkungu.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Spika, awali ya yote sina budi na mimi kumshukuru alla subuhana wataalla na kumtakia rehema Mtume wetu Muhammad S.A.W na mimi sina budi kutoa mchango wangu mfupi katika hotuba iliyoko mbele yetu ya Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika.

Mhe. Spika, wenzangu wengi wamesema kwamba hotuba hii imejaa fani mbali mbali imejieleza kwa kweli na kinachosubiriwa ni kupitishwa na kuanza kufanya kazi zake rasmi, kwa hivyo mimi nitaanza hapa kwenye ukurasa wa 20 Afisi ya Waziri amejieleza hapa kwamba baada ya kupatikana wizara alipata ugeni wa kutembelewa na nchi mbali mbali amezieleza nchi nyingi kabisa, pia na yeye binafsi akapata safari za kutembea nchi mbali mbali duniani. Kwanza niseme hiyo ni faraja kubwa kabisa na ni sehemu moja ya kuleta matumaini katika Wizara hii ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika.

Mhe. Spika, waswahili walisema kwamba mgeni tokea mwenyeji apone ni kweli baada ya wenzetu kuona wizara hii ni mpya, lakini aliyepewa hii nafasi ya uwaziri ni mkongwe tena mwenye heshima na kujulikana ugeni huu ukaja hafla kuonanana na Waziri, sasa wageni wameshafika. Kwa hivyo ningelimuomba sana Mhe. Waziri kusimama kidete na marafiki zake hawa ili tuweze kuwawezesha wananchi wetu kiuchumi, lakini akiachia tu kwamba katembelewa na katembea basi nao itakuwa basi.

Kwa hivyo ni vyema ndani ya kitabu chake hichi cha hotuba yeye na wafuasi wake wamepangana vizuri awatumilie hawa katika nchi mbali mbali ili uwezeshaji huu uwe wa ukweli, lakini kama tutawaacha tu hawa vijana wetu

malengo tuliyoyakusudia hatutoyafika. Kwa hivyo namnasihi sana Mhe. Waziri alione hilo tusibakie na maandiko tu vitabuni tuyafanyie kazi.

Mhe. Spika, nikitoka ukurasa huo wa ishirini naomba na mimi niruke kwenye ukurasa wa 25 kwenye idara ya Mikopo na mambo mengine, imeelekea kwamba mikopo waliyochukua wananchi wetu katika vikundi mbali mbali bado kabisa haijaleta tija kwa wananchi wetu, niwachache kabisa nadhani wamefaidika na mikopo hii. Lakini kwa taarifa tulizonazo na zinazozungumzwa hapa Barazani tija imekosekana na avikundi vingi vimekufa kutokana na ulipaji wa mikopo hii, nadhani pengine urejeshaji wa pesa hizi na hiyo riba ndogo inayoambiwa ipo pale imekuwa ni kikwazo. Kwa hivyo ni vyema kujipanga upya ili kuhakikisha awamu hii tunayokwenda wananchi wetu wamefaidika na mikopo hiyo, pia iongezwe kima kilichopo ni kidogo hakitoshi angalau itakapokuwa ni mikubwa kidogo basi wananchi wetu kile wanachokusudia kukifanya uwezekano wa kukifanya utakuwa upo.

Lakini pia hapo hapo Mhe. Spika, kuna mfuko wa Mhe. JK na AK mfuko huu kwa kweli ulieleweka vibaya katika maeneo yetu kwa wale waliofaidika, wengi walisema huu mfuko ni wetu na marais ni wetu wametutulia pesa hizi kilichobakia ni kuzitumia, halafu na ule mpangilio uliopangwa wa kupitisha mwananchi huyo kufaidika na pesa hizo nahisi pia utaratibu ulikua sio mzuri na urasimu ulikuwa mrefu pia mafunzo au elimu ya wale waliobahatika kuchukua zile fedha pia yalikuwa ni madogo sana.

Kwa hivyo namuomba sana Mhe. Waziri kuna pesa nyingi ambazo ziko mikononi mwa wananchi wetu, nadhani kwamba hizo sijui, lakini hizo zimeshakwenda na maji. Lakini wakati tunaendelea na haya mambo ni vyema tukajipanga upya tukaweka utaratibu mwengine upya ili pesa hii iweze kuzingilika na wananchi wetu mbali mbali waweze kufaidika nazo.

Mimi nahisi utaratibu wa mwanzo ulikuwa unaurasimu mkubwa. Kwa hivyo sasa tuwe na utaratibu ambao utakuwa ni mfupi lakini wa mafanikio. Kulikoni kuwa na urasimu mrefu lakini mafanikio ni madogo. Kwa hivyo tujaribu kuweka utaratibu utakaoleta tija haraka na uwezekano wa kurejesha ili wananchi wengine ambao hawajafaidika waweze kufaidika na mfuko huu.

Mhe. Spika, ni vyema awamu hii tunayoendelea nayo mifuko hii tuweze kuinusuru kwa kuweka utaratibu utakaowawezesha wale ambao watabahatika kuzipata fedha hizi. Kuna Idara hapa ya Ushirika, malengo yale. Mhe. Waziri ametaja kuna vikundi karibuni 117 Unguja 87 na Pemba 99. Hapa nilikuwa naomba kidogo nipate maelezo ni vikundi vingapi vimefaidika na fedha hizi na ni vikundi vingapi vimerejesha malipo hayo. kwa sababu tumetajiwa tu kwamba vikundi 117 vimesajiliwa. Lakini sijui ni vingapi ambavyo

vimefaidika kupata mikopo na wangapi wamerejesha katika mikopo hiyo. Ni vyema hapa Mhe. Waziri akatuwekea wazi ili tuweze kufahamu vizuri.

Mhe. Spika, ili makundi haya yaweze kwenda vizuri. Ningemuomba sana Mhe. Waziri awafanyie semina na warsha mbali mbali halafu awawezeshe vikundi kwa vikundi kwa vikundi kuweza kutembeleana na kubadilishana mawazo. Pengine inaweza ikawa kuna sababu ndogo tu kufeli kwa kundi hili, lakini watakapokuwa wanajifunza kwa wengine ikawa sababu makundi yale kuweza kunyanyuka haraka. Hili ningemuomba sana Mhe. Waziri ajaribu kuwapa elimu na kuwatayarisha waweze kutembeleana ili kubalishana mawazo.

Vikundi vyetu vya Ushirika na *SACOSS* zetu ziweze kudumu. Kwa sababu mawazo ya mtu mmoja tu au kundi moja tu ikawa hawapati mawazo na fikra ya makundi mengine ni njia moja ya kufa haraka. Lakini kama tutawashajihisha kuwakutanisha baina ya *SACOSS* na *SACOSS* nadhani kwamba maendeleo yanaweza kupatikana haraka.

Mhe. Spika, ni vyema bubadilike tutoke huko tulipoanza, huko tulipoanza tulianza vibaya wanakusanywa watu karibuni 25 wanapewa ng'ombe mmoja au mbuzi wawili, hebu tuangalie ng'ombe huyu mmoja watu 25 watamchunga miaka mingapi ili waweze kupata tija pale. Hapo kwa kweli sio kuwatoa watu katika umasikini ni kuwazidishia watu, kuwadidimiza watu ndani ya umasikini. Kama kweli tumekusudia kuwawezesha wananchi ni bora kuwe na makundi machache tukawawezesha wananchi wetu. Kulikoni kuwa na vikundi vingi lakini tukawazidishia zaidi umasikini wananchi wetu.

Mhe. Waziri nakuomba sana ni vyema ukapambana na makundi machache tu lakini tukayaona maendeleo yake. Kulikoni kuwa na makundi mengi lakini tukakosa kufaidi maendeleo yao. Kwa hivyo katika makundi haya jimbo langu la Tume tuna vikundi vingi na *SACOSS* nyingi. Mimi nadhani kama Mhe. Waziri atakuwa kama kilivyo kiwiliwili cha mwanadamu basi tunaweza tukapiga hatua. Kwa sababu kiwili wili ni viungo 360 lakini kikiumwa kimoja tu basi vyote vinavyobakia vinashirikiana kwa tatizo lile la kiungo kimoja.

Mhe. Waziri ningelimuomba sana Mhe. Waziri ashirikiane na wizara nyengine ili wizara zote ziwe kama kiwiliwili cha mwanadamu, ili tutakapokuwa hivyo tutaweza kuendesha na kuwasaidia wananchi wetu katika kutoka katika dimbwi hili kubwa la umasikini. Nasema kwamba jimbo langu la Tumbe tunavyovikundi vingi vya ushirika, tuna vikundi vya wavuvi, wafugaji na mambo mbali mbali.

Hivi sasa katika Jimbo hili tayari tumo katika harakati za ujengeji wa soko la samaki na wananchi wengi wa Tumbe ni wavuvi na tayari wameshajipanga.

Kwa hivyo nadhani kama utashirikiana na Waziri wa Uvivu na Mifugo, mkawapatia angalau meli moja, wananchi wale wa Tumbe, meli ambayo pengine itakuwa na uwezo wa kufanya kazi pengine watu 100 au 200 si kweli kabisa kama maendeleo hapo hatakosekana. Maendeleo yatapatikana na pesa itakuwa inazingilika na yule anayechoma samaki na naye fanya maandazi atakuwa na yeye anapata tija.

Mhe. Spika, kwa kusema uwape watu mashuwa ya mti mmoja halafu ndio tuseme tumeshawawezesha wananchi kimaendeleo, hapo bado itakuwa tunadanganyana. Lakini kama kweli tumekusudia hebu kwa mwaka huu 2011/2012, tuleteeni pale Tume angalau hiyo meli moja, mwaka mwengine mtakwenda sehemu nyengine. Muangalie Tumbe tumefanya nini. Sisi tunasema kwamba Tumbe kama tutawezeshwa basi tunaweza.

Mhe. Spika, nashukuru kama nilivyosema mwanzo mchangio wangu utakuwa ni mdogo. Kwa niaba ya Wananchi wangu wa Tumbe basi tunaunga mkono hoja mia juu ya mia. Ahsante.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nakushukuru Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ili niweze kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Uwezeshaji. Kwanza nianze kumshukuru Mhe. Waziri kwa hotuba yake hii inayoonesha nia na dhamira ya serikali ya kuwasaidia wananchi wake. Nimshukuru Mhe. Waziri yeye mwenyewe, watendaji wake wa wizara hii pamoja na wafanyakazi wenziwe kwa kazi nzuri waliyoiyonesha humu.

Mhe. Spika, nilikuwa nichangie mengi lakini naomba watanguliaji waliopita wameshanifilisi mengi sana. Sasa kama unavyotuhimiza mara zote tusiwe tunarejea yale kwa yale. Kwa hivyo nitajaribu kupita mule ambamo wenzangu wamepita lakini niongezee nyama tu kidogo ili kuweza kufanikisha vizuri.

Mhe. Spika, nianze kwenye ukurasa wa 10 kwenye Idara ya Mipango, Sera na Utafiti nisogee kwenye 12 aya ya 19 kwenye programu ya Ujenzi wa Kituo Cha Taarifa kwa waomba kazi na wajasiri amali. Mimi nilikuwa nataka kujua zaidi juu ya kitu hiki pale mahali kilipo na vipi wajasiri ambali watakavyokuwa wanaweza kupata taarifa ni utaratibu gani ambao utatumika kuweza kwenda kujua kupata hizo taarifa na wale ambao wanatafuta masoko na vitu kama hivyo. kile kituo chenyewe pale kilipo na namna gani kitakavyoweza kufanya shughuli zake.

Nilikuwa namuomba sana Mhe. Waziri atakapokuja hapa atusaidie kutuelekeza namna gani ili tuweze kufikisha ule ujumbe kwa wajasiri ambali wetu kule mitaani. Waweze kujua namna gani watakapokuwa wanahitaji zile taarifa watakwenda wapi na watazipata vipi.

Nikitoka hapo nisogee kwenye ukurasa wa 20 kwenye ofisi ya Mhe. Waziri. Katika maelezo yake Mhe. Waziri anaonekana ameruka sana hapa. Kuruka kwake huku inaonekana kuna faida kwa taifa. Namuomba sana Mhe. Waziri atakapokuja hebu atusaidie kidogo yale ambayo tutafaidika nayo katika ziara zake hizi. Maana yake ameshawahi kutoka kwenye vyombo vya habari kwamba kuna ajira zipo huko nje na mambo mengine. Namuomba hapa aje atueleze kwa kinaga ubaga ni vipi tutafaidika na safari zake hizi au yale ambayo ameyapata kule aje atupe kwa upana zaidi. Wananchi wetu waweze kujua na wajiweke tayari kwa ajili ya kujiandaa na zile ajira ambazo zipo kule kwa wenzetu na ule utaratibu mzima ambayo utakuwa unatumika kuweza kupata ajira zile.

Mhe. Spika, nirukie ukurasa wa 25 kwenye Idara ya Mikopo. Eneo hili kwa kweli Mhe. Omar Ali Shehe amelizungumza kwa kina sana. Nahisi mchango wa Mhe. Omar Ali Shehe na mimi uchukuliwa kama ni mchango wangu. Yale ambayo nilikuwa nataka kuyazungumza karibu yote ameyamaliza pale. Niongezee kwamba yale ambayo ameyazungumza kwa hivyo Mhe. Waziri yale ambayo yameelezwa pale mimi nauna nayo ukapokuja utatupa ufafanuzi zaidi katika lile.

Mhe. Spika, nisogee mbele kidogo kwenye ukurasa wa 25 kwenye Idara ya Ushirika nije kwenye aya ya 48 kwenye *SACOSS Banks*. Mimi nilikuwa nataka kujua hizi *SACOSS Banks* ambazo zimepata mikopo ya *CRDB* sijui ni zipi na zinatokea upande upi. Kwa sababu tunazo *SACOSS* na sisi kule katika majimbo yetu lakini hichi kitu kwetu hakijafika. Sasa utupe utaratibu ni namna gani wa *SACOSS* zetu na sisi zinaweza zikapata mikopo hii ya *CRDB*. Inaonekana ni mikopo minono hii inaweza ikazizaidi *SACOSS* zetu na sisi kule zikaweza kunufaika na mkopo huo wa *CRDB Bank*. Ningekuomba sana Mhe. Waziri utakapokuja tupe maelezo ya *SACOSS* hizi zilizofanikiwa na zile ambazo zimeomba hazijapata na zile ambazo zinahitaji utaratibu ambao utakaotumika ili tuweze na sisi kuwasilisha kule kwenye *SACOSS* zetu nazo ziweze kuomba mikopo hii ili ziweze kupata faida.

Kwa kweli ni jambo zuri sana hili ambalo Mhe. Waziri mmelianzisha kwa watu hawa wa *CRDB Bank* tena umelisema tawi la Zanzibar. Ningeomba sana hili na sisi utupatie maelezo ya ziasa ili tuweze kuwashajihisha wana *SACOSS* waweze kujiunga katika kupata mikopo hiyo.

Mhe. Spika, nikitoka hapo nisogee mbele kwenye ukurasa wa 45 kwenye Kamisheni ya kazi. Hapa kidogo mimi nilikuwa nataka kujua serikali imejiandaa vipi katika suala zima la mambo haya ya *East Africa Community* na masuala ya kazi hasa hizi ajira za kwenye sekta binafsi. Soko hili linaonekana kuvamiwa sana na wenzetu wanaotoka Afrika ya Mashariki. Inaonekana mpaka

vijana wetu ambao wapo hapa na wamesoma katika vyuo kama kile cha utalii, kinatoa wanafunzi wengi. Hata takwimu alizotuambia Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akijibu swali hapa alituonesha ni takwimu kubwa za watu ambao wanasoma pale. Sijui Kamisheni hii inawasaidiaje vijana wale ambao wamemaliza pale, lakini ukitizama asilimia kubwa ya waajiriwa katika mahoteli haya ya kitalii utakuta ni watu kutoka nje ya Zanzibar. Sijui hii kamisheni imeweka utaratibu gani ambao inaoutumia katika kuhakikisha kwamba inawasaidia wale vijana wetu wanaotoka katika vile vyuo vyetu vya ndani hapa kupata ajira katika maeneo yale. Kwa sababu wanaomba nafasi lakini kwa sababu wasimamizi wa maeneo yale au waajiri hasa katika zile hoteli. Mara nyingi sana wanakuwa ni watu kutoka nje ya Zanzibar na wao vile vile *priority* huwa wanaipeleka kwa wale watu wa kwao zaidi. Mhe. Waziri Idara yako au hii Kamisheni yako ikoje katika hili, ni utaratibu gani inaotumia kuweza kuwasaidia hawa.

Jengine kwenye hii Kamisheni ya Kazi nije kwenye suala la utoaji wa vibali vya kufanyia kazi. Kunaonekana kuna utoaji holela wa vibali hivi Mhe. Waziri. Kwa sababu unaweza kukuta watu wanaofanya kazi au wageni wanaofanya kazi kule hasa sekta ya utalii, kazi ambazo zinaweza kufanywa na Mzanzibari unazikuta anafanya mgeni kutoka nje ya Zanzibar au nje ya Tanzania. Usishangae leo hii Mhe. Waziri ukamkuta mtaliana ndio mtembezaji wageni kule, yeye mwenyewe mgeni na yeye anatembeza wageni. Huyu huoni kama atakuwa anaipotosha historia yetu. Maana hana cha kuwambia pale atakuwa anawadanganya kwa hivyo na wao hawajui watakuwa wanachukua kile wanachodanganywa.

Mhe. Waziri mimi nilikuwa naomba hii Kamisheni yako isiwe inatoa vibali ovyo ovyo. Mimi nasema hayo nikiwa na ushahidi kabisa wa haya ambayo yanafanyika. Inawezekana wametoa au hawajatoa lakini kuna watu wanafanya hizi kazi. Ningeiyomba Kamisheni yako ihakikishe inadhibiti wimbi hili. Kwa sababu kama wao wanashughulika na masuala haya ya kazi na vijana wetu wapo wenye taaluma ile. Mimi nafikiria ni vyema wakawa kwa kazi zile hawa wawekezaji nao tukawa tunawazuia, tuwape hawa vijana wetu ili na wao wapate ajira. Tukiendelea kuwaachia hawa kwa sababu tu labda huyu mtaliana akizungumza na mtaliana mwenziwe itakuwa karibu zaidi mimi nahisi Mhe. Waziri hapa kidogo tutakuwa tunakosea. Ni vyema tukajipanga vizuri katika hili kuhakikisha ajira hizi vijana wetu wa Zanzibar wanafaidika nazo.

Mhe. Spika, suala jengine nilikuwa nataka kuzungumzia kwenye hii Idara ya Usalama wa Afya Kazini. Hii ipo ukurasa wa 56. Kwa kweli Mhe. Spika, mimi nilikuwa najiuliza siku zote nani msimamizi wa suala hili, lakini niliposoma kitabu cha Mhe. Waziri hapa kinaonesha kumbe Wizara yake ndio msimamizi wa mambo haya ya usalama na afya katika kazi. Suala hili kwa kweli

linaonekana kama kidogo limepewa mgongo. Utawakuta wafanyakazi mimi naanza kenye hizi taasisi za kiserikali hasa wanafanya kazi hata zile kinga zenyewe wanakuwa hawana. Kwa mfano unaweza kwenda maeneo kama yale ya ubebaji wa vitu vizito watu wa namna ile hawana hata ile *safety shoes*. Kwa hivyo ni hatari kwa maisha yao.

Idara hii sijui inaisimamiaje serikali yenyewe katika kuhakikisha wale wafanyakazi katika zile taasisi wanapewa vyombo husika vya kuwasaidia kuweza kujikinga na maafa katika sehemu zao za kazi. Hata ukitizama Baraza la Manispaa utawakuta wafagiaji hata kiyatu mguuni hana, hana kile cha kuzuia vumbi ambalo lisimuuingie yeye. Hebu tuiyone idara hii ikifanya kazi zake. Iwasimamie hawa hasa hawa wakuu wa hizi taasisi, kuona kwamba inawajali wale wafanyakazi wao. Zile sehemu ambazo zinahusika kupata vifaa vya kufanyia kazi basi wawe wanapewa. Tusiwe tunakwenda kuziganda tasisi binafsi tu. Maana taasisi binafsi zinagandwa kweli kweli. Lakini na hizi taasisi za Kiserikali na taasisi za umma nazo vile vile tuhakikishe zinafata haya masharti. Yasiwe masharti haya ya upande mmoja tu, kwa sababu wote hawa ni wafanyakazi wa taasisi binafsi na hizi za umma. Tukiwa tunaendelea kuzikamata taasisi za binafsi tu kwamba wahakikishe kuna *fire extinguish*, kuwe na hichi kuna hichi katika sehemu za kazi. Wakati hizi taasisi zetu za Kiserikali hazina.

Mfano upo kama tukitembelea tutaenda taasisi nne, tano za serikali sasa hivi utakuta hakuna *fire extinguisher*, hakuna vitu chungumzima ambavyo ni muhimu kwa wafanyakazi kuwepo kwa ajili ya usalama wao. Kwa hiyo ningeiyomba sana idara hii ikalisimamia vizuri hili suala, kuhakikisha vifaa vya usalama kazini vinakuwepo katika taasisi zote za kiserikali na vile binafsi.

Mhe. Spika, mchango wangu ulikuwa zaidi katika hilo na nimezungumza kwa upole sana ili haya Mhe. Waziri atusaidie yaweze kutekelezwa. Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, kwa niaba ya wananchi wangu wa jimbo la Mkwajuni naiyunga mkono hoja ya Mhe. Waziri. Ahsante sana.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Spika, kwanza na mimi namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kuwepo hapa na nikapata fursa hii ya kuchangia hotuba ya Waziri wa Kazi, Uwezeshaji wa Wananchi kiuchumi na ushirika. Nampongeza sana Mhe. Waziri kwa jinsi alivyokipamba kitabu chake kama walivyosema wenzangu waliotangulia. Kitabu chake katuwekea watendaji wake hapa ili tuende nao sambamba pale watakapokwenda ndivyo sivyo, tuwe nao katika kuwakaba koo ili wizara yake ifanye kazi vizuri kwa wananchi wetu.

Pia nakupongeza Mhe. Spika, kuweza kukiongoza kikao hichi kwa muda mrefu sana na kwa umakini wa hali ya juu kabisa.

Katika kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Kazi, mchango wangu hautokuwa mkubwa sana. Wengi katika wajumbe waliopita wamechangia mengi ambayo labda na mimi ningekuwa na fursa kubwa ya kuyachangia. Kwa kuwa tunataka kuokoa muda na tusirejee hayo hayo, basi mchango wangu utakuwa wa kiasi tu. Kwanza nakwenda katika Idara ya Mikopo.

Mhe. Spika, Idara hii ya Mikopo ni idara muhimu sana katika kuwawezesha wananchi. Kwa sababu wananchi wetu wengi ni masikini. Kwa sababu ya umasikini wao wangetarajia sana kupata mikopo kutoka wizara hii ili waweze kujikwamua. Namuomba Mhe. Waziri kwanza watu wa idara hii awawezeshe kuwapa vipandio ili wapite katika maeneo mbali mbali ya Zanzibar, mijini na vijijini na mashamba ili wawaelekeze watu juu utaratibu mzima wa kupokea mikopo hiyo.

Mhe. Spika, pamoja na hivyo naiyomba Idara hii iwe na uwadilifu wa kutosha katika utoaji wa mikopo, kwani kuna malalamiko mengi tu katika shehia mbali mbali kwamba mikopo hii haifiki haifiki.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri katika kipindi hichi cha mwaka 2011/2012 ajikite sana katika kutoa mikopo hasa katika maeneo ya vijijini na mashamba. Kwa sababu watu wanaoishi katika maeneo ya mashamba umasikini kwa kweli umewaelemea sana kwa kweli na hii sio siri. Kwa mantiki hii namuomba Mhe. Waziri akite kutoa taaluma ya kutosha na kutoa huruma maalum kwa watu wanaoishi shamba ili na wao wajisikie kwamba wizara hii imewaona na kuwawezesha kuwakwamua katika hali duni ambayo wanayo.

Mhe. Spika, miongoni mwa vijiji ambavyo vinakuwa na umasikini mkubwa lakini wakiwezeshwa wanaweza ni watu wa jimbo langu la Chambani. Namuomba Mhe. Waziri afanye ziara ya makusudi alitembelee jimbo langu la Chambani kwa sababu jimbo hili linavikundi mbali mbali, lakini nyenzo za kufanyia kazi, taaluma ya kufanyia kazi, uwezo wa kufanya kazi ni mdogo mno. Eneo hili kama litawezeshwa basi linaweza likafanya kazi nzuri na linaweza likajikwamua na umasikini. Eneo hili lina ardhi nzuri kwa kilimo cha mboga mboga, lakini kuna usumbufu mkubwa wa miundombinu ya kufikilia vile vitendea kazi, miundombinu ya kuweza kufanya kazi vizuri. Mhe. Waziri labda awawezeshe watu hawa. Basi ajipange vizuri ili awafikishie watu wangu wa jimbo langu la Chambani miundombinu ambayo itawasaidia, hasa kwa vile ina ardhi nzuri.

Mhe. Spika, kuna eneo tunaliita Makaani kule kwa mboga mboga huko ndio kwao. Lakini mboga zinashindikana kustawi kwa sababu ya ukosefu wa maji. Kwa hivyo Mheshimiwa katika kuliwezesha jimbo langu kiuchumi na kuwaondolea wananchi wangu umasikini. Nakuomba unifanyie ziara makusudi uwe nao bega kwa bega ili kuepukana na umasikini huu ambao kwa kiasi fulani imekuwa ni kero kubwa. Kwani kila mwananchi anahitaji ajiendeleze lakini njia za kujiendeleza zimekuwa ni tete.

Mhe. Spika, nikenda katika kitabu chako Nam. 69 katika kiambatisho kinasema nani awezeshwe? Hapa kuna maelezo yanasema, Wawezeshwe wale wenye kipato cha chini wakiwemo wakulima, wavuvi na wafugaji wadogo wadogo.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri katika hili aliangalie kwa kina, kwa sababu inasikitisha sana kuona wafugaji mtu anapewa ng'ombe mmoja anaambiwa huyu atakuwezesha labda baada ya muda na wewe utajisikia kiuchumi.

Mhe. Spika, wafugaji wetu watakuwa bado hawajafaidika bali watakuwa wafugaji wetu wamerudishwa katika umasikini kwa kupewa ng'ombe mmoja au mbuzi mmoja kwa kikundi cha ushirika. Kwa hivyo namuomba Mheshimiwa abadilishe mbinu mbadala, badala ya ng'ombe mmoja kupewa kikundi cha watu 25 au 20 aangalie njia gani ambayo itawawezesha wafugaji hawa kuwakwamua katika umasikini badala ya kupewa ng'ombe mmoja. Halafu vile vile sehemu ya pili anasema katika sekta isiyo rasmi na biashara ndogo ndogo sana na zile za kati.

Mhe. Spika, watu wanaoishi vijijini sekta hizi wanazo lakini wamekwama kutokana na hali duni ya maisha. Mimi namuomba Mhe. Waziri awe na mbinu mbadala ya kutoa misaada hii isikite katika maeneo yale ya mjini moja kwa moja bali na maeneo ya shamba ayaangalie kwa kina sana.

Mhe. Spika, baada ya maelezo yangu haya kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Chambani naiunga mkono hoja hii mia kwa mia. Nashukuru sana kunipa nafasi hii, ahsante sana.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, nianze kama ilivyo ada yetu kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu kwa kutujaalia neema hii ya pumzi zilizotuwezesha kusimama hapa tukaichangia bajeti ya Mhe. Haroun Ali Suleiman Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika.

Pili, Mhe. Spika, nikushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii na niendelee kukushukuru na kukupongeza sana jinsi unavyoliongoza Baraza letu. Mhe. Spika, Baraza limejenga heshima kubwa sana mbele ya macho ya wananchi wa

Zanzibar na si kwa sababu ya michango yetu sisi, lakini ni kwa sababu ya wewe anavyoliongoza na kutupa nafasi ya kutoa michango kwa niaba ya wananchi wetu na hivyo kulijengea heshima na hadhi mbele ya wale ambao tunawawakilisha hapa.

Mhe. Spika, tatu nimpongeze Mhe. Waziri kwa dhati kwa kuteuliwa kuongoza wizara hii, naamini atatumia uzoefu wake kutuonesha mabadiliko katika sekta hizi ambazo anazisimamia.

Mhe. Spika, baada ya pongezi na shukurani hizo sasa naomba nigusie maeneo ambayo yameguswa na wizara hii nikitoa mchango wangu unaowakilisha wananchi wa Jimbo la Mji Mkongwe. Nianze na suala la ajira.

Mhe. Spika, ajira ni kilio cha kila mwananchi wa Zanzibar kwa sababu kama unavyojua kwamba kutokana na hali ya umasikini tuliokuwa nao kutokuwa na ajira inapelekea hali kuwa mbaya zaidi, na hali inakuwa mbaya zaidi kwa sababu mara moja alitwambia hapa Mhe. Waziri wa Fedha kwamba bahati mbaya sekta binafsi katika nchi yetu bado haijakuwa. Kwa hivyo, tegemeo pekee lilobakia la watu kwa ajira limebakia kuwa katika serikali, sasa katika hali hiyo tuna changamoto kubwa sana ya vipi kushajihisha ukuaji wa uchumi ambao utapelekea kukua kwa sekta binafsi, na hapo ndipo tutapoweza kutoa nafasi za ajira kwa watu wetu.

Mhe. Spika, mipango mingi iliyoelezwa na wizara mbali mbali katika hotuba zao za bajeti. Hapa naamini zinaelekea huko na hata bajeti yetu kubwa ambayo ilisomwa hapa inajaribu kutuelekeza huko kwa kuimarisha viwanja vyetu vya ndege, kutaka kujenga kiwanja kipya Pemba, bandari mpya ya Mpiga Duri ambayo inatafutiwa mwekezaji, suala la kuimarisha barabara, suala la kuweka malengo yanayopelekea kuitangaza Zanzibar kuwa bandari huru. Mhe. Spika, yote hayo lengo lake ni kuhakikisha tunazifungua hizi fursa za kiuchumi katika nchi yetu ili vijana wetu waweze kupata ajira.

Mhe. Spika, wakati tunakabili changamoto hiyo na bila shaka tuna safari ndefu hadi tufike huko inshaallah Mwenyezi Mungu atatufikisha, lakini hizi tulizonazo ajira tunapaswa kuzilinda ili ziweze kuwanufaisha Wazanzibari wetu. Mhe. Spika, hapa ndio nataka nianze kusema kwanza Mhe. Waziri ana changamoto ya kuona hili kwamba ajira tulizonazo na hasa katika sekta binafsi hasa sekta ya utalii ambayo sasa hivi imechukua nafasi kubwa uchumi wetu ni kuona kwamba zile nafasi ambazo zipo pale kwanza wanazipata Wazanzibari.

Mhe. Spika, kidogo tuna tatizo katika kutekeleza sheria ya katika eneo hili. Mhe. Spika, ukenda kwenye mahoteli mengi hutaki hata utafiti wowote utakuta kazi nyingi zimeshikwa na wageni sio Wazanzibari. Mhe. Spika, kuna sheria

hapa kwa mfano katika sekta ya utalii kwa mfano kazi hizi za kutembeza watalii hayapaswi kufanywa na wasiokuwa Wazanzibari lakini leo kuna kampuni za kigeni hapa Zanzibar zinaendesha biashara hii. Kwa hivyo, matokeo yake hata vijana wetu wanaojishughulisha na kazi hizi ndogo ndogo tu, basi huwa wanazikosa.

Mhe. Spika, hivi karibuni nimekwenda kuonana na vijana wetu pale katika eneo la Forodha Mchanga wameniambia kazi yakupeleka wageni katika visiwa vile vidogo vidogo zimedhibitiwa na wenye mahoteli fulani huku Mji Mkongwe. Kwa hivyo, wanaekeza katika hoteli lakini pia wameweka na kazi za kupeleka wageni kule. Mhe. Spika, kwa hivyo, tunahitaji kuona kwamba huku tunaandaa sheria ili kuona kuwa kazi za Wazanzibari zinatunzwa na wanazipata wao. Mara nyingi tunasema kwamba vijana wetu hawajapata mafunzo, lakini Mhe. Spika, mimi siamini kama Mzanzibari amekosa mafunzo hata ya kutandika kitanda au hata ya kutunza bustani. Lakini huko tunakokwenda naona hata kazi za walinzi pia vijana wetu wanazikosa. Kwa hivyo, nilikuwa nataka hili tulitazame kwa ukaribu sana.

Mhe. Spika, lakini mara nyingi mimi huwa napiga kelele katika bajeti nyingi zilizozungumzwa hapa, tusitazame katika kazi hizi za *unskills labour*, tutazame hata katika hizi kazi za ngazi za kati juu ya nafasi za utawala na *management* sehemu nyingi ukenda unakuta vijana wasiokuwa Wakizanzibari wameshika nafasi hizi. Mhe. Spika, bahati nzuri moja katika maeneo ambayo Vyuo Vikuu vilivyoanzishwa hapa Zanzibar vinajitahidi kutoa watu ni katika fani kama hizi za *management* tunao vijana wanasoma hapa. Mhe. Spika, sasa kwa nini vijana kama hawa hawapati kazi katika sekta hizi nadhani kuna tatizo katika kuwa-*enforce laws* na nadhani hapa tuna haja ya kusimamia vizuri kuona ajira hizi zinawafikia Wazanzibari.

Mhe. Spika, lakini hapo hapo niseme wakati natetea Wazanzibari kuhakikisha wanalindiwa ajira zao hizi, lakini na ndani ya Zanzibar Mhe. Haroun Ali Suleiman nakumbuka aliwahi kuchangia siku moja na akanipongeza pembeni kwamba tulipopitisha sheria ile ya utumishi wa umma tulizungumzia suala la *composition* ya utumishi wa umma i-*reflect diversity* ya Zanzibar *Population*. Ni kwamba ule mchanganyiko wa watu wa Zanzibar uonekane katika ajira na kazi. Mhe. Spika, nikasema hili kwamba huko nyuma hasa katika vyombo vya ulinzi kulikuwa na jamii fulani hazikubaliki katika kazi za aina fulani. Kwa hivyo, hapa tulipofika Mhe. Spika, tunajenga umoja wa kitaifa tunataka kuona mambo kama haya yanaondoka. Nataka tuone kwamba zile nafasi za ajira kwa ujumla wake ziwe zina-*reflect* ule mchanganyiko na mjumuiko wa jamii ya Kizanzibari. Naomba hili Mhe. Waziri alisimamie sana.

Mhe. Spika, katika hilo la ajira nizungumze kwa ufupi tu kwamba hatujakuza *private sector*, lakini iko hii *informal sector,* watu hawa wa jua kali, akina mama ntilie wanaofanya shughuli kama hizi. Mhe. Spika, eneo la Mji Mkongwe ni katika eneo moja ambalo shughuli hizi nyingi zimejikita hasa kwa wasio wakaazi wa Mji Mkongwe wanakuja kufanya shughuli zao pale. Mhe. Spika, sio tatizo na ndio ilivyo kwa nchi zote pale kati kati ya Mji wenye harakati ndio humo tunamokimbilia. Lakini kumekuwa na tatizo la kuwabughudhi watu hao wanaofanya shughuli hizi Mhe. Spika.

Mhe. Spika, nadhani Mhe. Waziri anayeshughulika na masuala ya kazi na kuwawezesha wananchi pia alisimamie hili ili tuone hatuwabughudhi wananchi wetu. Mhe. Spika, na mimi natofautiana na wengine, mimi sio katika wale wanaounga mkono kwamba tuwaachie tu wafanye biashara holela ikawa nchi kama vile haina mwenyewe. Hapana, mimi siko katika huko wala mimi sio muumini wa siasa hizi za kusema maneno au nifurahishe watu kwa kupigwa makofi, hapana. Nasema tudhibiti lakini tusiwabughudhi tuwawezeshe kufanya shughuli zao, na yale maeneo tunayohakikisha tunawahamishia kuona kwamba je, mazingira yamewekwa yakuwafanya waende pale. Kwa mfano, pale Jua Kali tunasema wajiajiri watu sisi tumeshindwa kuwapa ajira, wende Saateni lakini hebu tukaitazame hali ya Saateni ilivyo ni vumbi tupu ukenda. Mhe. Spika, yale maduka yaliyojengwa pale wakubwa wamegawana wenyewe.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, vitu kama hivi nadhani wizara hii ivisimamie kwamba tuwe na nidhamu ya Mji wetu kwa sababu sasa hivi ukenda kila pahala mtu akiona pana upenyu anaweza kwenda pale akaweka kiduka na wengine wanafunga mpaka njia. Hii ni kwa sababu hatujaweka mpangilio mzuri wa maeneo yetu. Mhe. Spika, mimi nasema wizara hii isimamie hii *informal sectors* ili tuwasaidie na mimi nadhani Mhe. Waziri katika hili akilitizama tunahitaji labda yeye asaidie kuratibu na wizara nyengine zinazohusika na masuala haya kama ni Baraza la Manispaa na Halmashauri nyengine za Miji tuweze kuwashirikisha.

Mhe. Spika, tatizo linakuja pale tunapokuja kufanya maamuzi sisi halafu tukapeleka tukawa tunaamua tu yale maamuzi ndio wanapokuwa wana-*resist* vijana wale, lakini tukiwa tunawashirikisha tangu mapema na wao wakatoa mawazo yao watajihisi na wao ni sehemu ya maamuzi ambayo tunayafanya na hivyo watatusaidia kutoa ushirikiano kwa kule tunakotaka twende. Kwa hivyo, nasema Mhe. Spika, hili kero ambalo liko pale naomba sana tulitazame na tu-*plan* vizuri tuhakikishe *participation* yao halafu ndio tu-*execute* zile *plans* zetu.

Mhe. Spika, kuna watu wengi wameuliza uliza suala hapa lakini walikuwa wanaogopa kutaja nchi mimi nilimtajia hasa Mhe. Waziri. Kuna maneno huko mitaani kwamba kuna nafasi za ajira Qatar na imekuja kutokana na hotuba ya

Mhe. Waziri na Waziri mwenzake wa Tanzania Bara waliporudi katika mkutano ule wa kimataifa. Kwa hivyo, hii imeleta maneno mengi huko mitaani, tunaulizwa na kila mtu kwamba kuna watu wanajazishwa fomu, sasa sijui kama kuna ukweli wa kiasi gani. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri akija atusaidie hili ili wananchi wetu wanaotuuliza kila wakati wasikie hasa ukweli juu ya suala hili la ajira ambazo Mhe. Waziri alizitangaza baada ya kurudi safari yake.

Mhe. Spika, katika hilo hilo la ajira jana yalizungumza hapa kwamba wizara hii ina sheria gani atusaidie Mhe. Waziri katika kusimamia ajira zetu katika Serikali ya Muungano. Mhe. Spika, tuna *quaters* yetu katika jeshi, tuna *quaters* yetu katika polisi naamini tuna *quaters* yetu hata katika idara ambayo haitajwi Idara ya Usalama, tunapaswa tuwe na *quaters* yetu katika Wizara ya Mambo ya Nje.

Mhe. Spika, juzi ilitokea kesi Bungeni pale, Mhe. Yahya Kassim Issa nampongeza sana Mbunge wa Chwaka ali-*challenge* pale ndani ya Bunge wakati inasomwa hotuba ya Wizara ya Ulinzi aka-*query* waliletwa wale wakuu wote wa vikosi pale na magenerali. Mhe. Spika, Mhe. Yahya aka-*challenge* akasema hebu kama yuko mmoja katika wale mlotuletea anyanyuke Mzanzibari. Mhe. Spika, hajakuwepo hata mmoja ame-*challenge* ndani ya Bunge na ndio hivyo hivyo ukenda katika Wizara ya Mambo ya Ndani kwenye Jeshi la Polisi na katika sehemu nyingi. Kwa hivyo, Mhe. Spika, unapokuwa katika viongozi huna Wazanzibari hawawezi hawa kusimamia katika ajira wakapata Wazanzibari. Ndio haya yaliyokuja mpaka wakifika huku nafasi za Zanzibar pia wakachukua wakachomeka watu wao.

Mhe. Spika, ilitokea kadhia moja hivi karibuni alikufa askari jeshi mmoja kule Bara, basi kutizamwa *particulars* zake akaonekana ameajiriwa Pemba basi maiti ikaletwa Pemba. Mhe. Spika, alipofikishwa maiti kule Pemba kumbe hana mtu, kumbe ni mtu wa Munduli ameajiriwa kupitia Pemba. Kwa hivyo, Mhe. Spika, mambo kama haya yapo hebu Mhe. Waziri akija katika hili atusaidie.

Mhe. Spika, katika hilo hilo alisimama kule Mbunge wa Ziwani Mhe. Ahmed Juma Ngwali akatoa kitabu alichopewa pale pale Bungeni cha *BoT* katika wale Maafisa wa ngazi ya juu 80 basi Mzanzibari ni mmoja. Mhe. Spika, ni kwamba ziko ajira zetu nyingi huku kwa hiyo Mhe. Waziri akija atusaidie katika hili nini *role* ya wizara yake katika kusimamia ajira hizi kwa upande wetu.

Mhe. Spika, pia katika hotuba ya Mhe. Waziri ukurasa wa 45-46 alikuwa anazungumzia hii itifaki ya Soko la Pamoja la Afrika ya Mashariki. Mhe. Spika, nakumbuka kuna baadhi ya mambo na nimpongeze sana Mhe. Abubakar Khamis Bakary akiwa Mbunge wa upinzani katika Bunge wakati ule alisimama

kidete kuna baadhi ya mambo ya maslahi ya Zanzibar yanalindwa. Kwa mfano, walipokuwa wanaeka sheria yakupiga marufuku ya uingizaji wa mchele ili kulinda mchele wa ndani, akasema sisi Zanzibar hatulimi tunategemea mchele kutoka nje.

Kwa hivyo, kifungu hiki kisi-*apply* Zanzibar. Mhe. Spika, nilitaka nisaidiwe tutapokuja katika hii itifaki ya soko la pamoja hasa katika *free movement of labour* hatutokuja kuzidiwa hapa ikawa sisi wenyewe zile ajira ambazo tunazigombania chache hazipo zisije zikachukuliwa na watu kutoka nchi nyengine za Afrika ya Mashariki. Nilikuwa naomba hili Mhe. Waziri akija pia anisaidie hii itifaki ya soko la pamoja tumejipanga kiasi gani Zanzibar kulinda ajira zetu katika kipindi hiki ambacho sisi sote tumekuwa ni *victims* tu.

Mhe. Spika, hapo hapo pia nilikuwa nataka Mhe. Waziri anisaidie amezungumzia katika sehemu hiyo hiyo ya ukurasa wa 45 kwenda mbele juu ya nafasi ya Zanzibar katika *ILO* Shirika la Kazi Duniani. Hivi hatuna fursa sisi kwa sababu masuala ya kazi sio masuala ya Muungano Zanzibar kuwa mwanachama wa *ILO*, hata kama mwanachama mshiriki. Nakumbuka kulikuwa na kesi kama hiyo kwa upande *wa International Meritime Organization IMO*. Bara walipitisha *Marchant Shipping Act* yake Baraza hili ikaikataa sheria hii ikapitisha *Meritime Transported* hatimae labda ilipata nafasi yakuwa kama mshiriki kupitia *IMO*, sio kwa kuwakilisha katika ujumbe tu wa Tanzania lakini ina nafasi yake. Hebu katika hili suala la *ILO* Mhe. Waziri tusaidie hatuwezi tukafaidika katika fursa ambazo zinapatikana katika Shirika hili la Kazi Duniani.

Mhe. Spika, nije katika Idara ya Mikopo. Kwanza nilikuwa naomba maelezo katika buku lile la *votes* idara hii iliombewa ruzuku. Mhe. Spika, nilikuwa najiuliza hii ni idara kwa nini ipewe ruzuku, ikiwa ni kwa sababu ya mikopo nilitegemea kulikuwa na fungu la mikopo mbali lakini lile fungu la utawala lingelikuwa linaonekana na *vote* zake ndogo ndogo kama ilivyokuwa idara nyengine za serikali. Lakini hapa itakuwa Idara ya Mikopo kwa ujumla wake tu imeekewa ruzuku katika mambo ya uendeshaji na katika mambo ya mifuko ya mikopo. Kwa hivyo, kama ni idara nadhani *status* yake hii ingepaswa ionekane na serikali, nilikuwa naomba maelezo katika *vote* hiyo ya 0502 ambayo iko ukurasa wa 433 ya buku lile la *expenditure.*

Mhe. Spika, niseme kwamba hii mikopo tukiitoa kwa staili tunayokwenda Mhe. Spika, haitasaidia kupunguza umasikini, kwamba utakuwa na fedha chache halafu unaigawa 20, 000 au 30,000 Mhe. Spika, hii haiwezi kuondosha matatizo. Mimi nataka nikubaliane kabisa na mapendekezo waliyotoa wenzangu hebu tujikite kuchagua vikundi vichache tuvipe nguvu ili kweli viweze kujikwamua kutokana na umasikini. Hivi vikisimama ndio vitazalisha

ajira kwa wengine kuliko kuwa unagawa 20,000 au 30,000 itakuwa kila siku mtu anaendelea kuwa tegemezi.

Mhe. Spika, nilikuwa naomba tujitahidi ku-*review policy* hii hasa kwa sababu Mhe. Waziri anakumbuka nilimuuliza na akanisaidia akaniletea kwa maandishi hapa, kwamba asilimia 40 ya wananchi wetu wanaishi chini ya dola 1 kwa siku. Kwa hivyo, katika hali kama hiyo hawa hatuwakwamuwi kwa kuwakopesha shilingi 30, 000 au 40,000. Mhe. Spika, nilikuwa naomba hili Mhe. Waziri alitazame kwa makini.

Mhe. Spika, hapo hapo katika ukurasa wa 29 wa kitabu chake amezungumzia huu mfuko wa AK na JK na pia ule mfuko wa kujitegemea. Hapa nilitaka kuzungumzia zaidi mfuko wa kujitegemea tuna tatizo kubwa katika mfuko wa AK na JK kwa kurejesha mikopo na hapa napata wasi wasi kwa sababu kunakuwa na hoja utoaji wa mikopo hii tuihamishie wizarani na tuiondowe benki. Mimi najiuliza ikiwa kwenye benki hailipwi kwa sababu kuna *site rules* za ku-*apply* ili kuhakikisha kwamba watu wanalipa je, tukiipeleka katika wizara ndio wananchi hao watarudisha mikopo hii. Mhe. Spika, hebu naomba tulitazame hilo kwa makini.

Mhe. Spika, nilikuwa nasema katika mfuko wa kujitegemea kidogo nimepata wasi wasi namuomba Mhe. Waziri akija anipe maelezo ukurasa wa 30 mpaka 31 wa hotuba yake. Mhe. Spika, kwanza katika hili napongeza kwa sababu kuna uwiano mzuri zaidi baina ya Unguja na Pemba katika ugawaji wa mikopo kuliko ule katika mfuko wa AK na JK. Mhe. Spika, katika mfuko wa AK na JK unakuta Unguja ni asilimia 69.17 na Pemba ina asilimia 30 wakati katika hii *House of Budget Survey* Wilaya za Pemba ziko nyuma zaidi kwa umasikini kuliko Wilaya za Unguja. Nadhani tulitazame hilo kwa mwaka unaokuja, lakini hoja yangu mimi ni katika huu mfuko wa kujitegemea.

Mhe. Spika, mfuko wa kujitegemea ukitizama hapa hizi namba kidogo zimenipiga chenga na mimi Mhe. Haroun anajua kama nilikuwa pocho sana wa Hesabu nilipokuwa skuli kwa sababu yeye alinisomesha Hesabu *form four* alipokuja akanikuta nafikiri nilikuwa nikimpa shida sana kwa sababu ilikuwa hazipandi kabisa katika kichwa changu. Kwa hivyo, na hapa ndi zimenichanganya kabisa Mhe. Spika, kwa sababu katika kifungu hiki kasema kwamba mfuko wa kujitegemea umetoa mikopo 83,800,000. Ukitizama ukurasa wa 31 zilizorejeshwa ni 83,288,250, lakini Pemba inaonekana imerejesha 27,900,000 kati ya zilizokopeshwa 35,100,000 nimefanya hesabu ni kama asilimia 79.

Mhe. Spika, tatizo la kihesabu limenipiga kwenye Unguja, Unguja anasema Mhe. Waziri imetolewa mikopo 48,700,000 kwenye ukurasa wa 30, lakini

zilizorejeshwa ni milioni 55,128,000 sasa nikajiuliza wamerejesha na faida hawa Mhe. Spika? Hebu naomba hili atusaidie maelezo kwa sababu kama nilivyosema Pemba kidogo kuna upungufu Unguja imezidi kile kiwango walichokopeshwa, nilikuwa naomba maelezo katika hili.

Mhe. Spika, la mwisho kabisa nije katika Kamisheni ya Kazi niligusia kidogo pale mwanzo katika kusimamia masuala haya ya ajira, lakini sasa nataka kuja katika suala la kazi. Mhe. Spika, inaonekana tuna tatizo katika kusimamia haki za wafanyakazi wetu, na hili limezungumzwa katika ripoti ya haki za binadamu iliyotolewa na Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar kupitia *Tanzania Human Rights Reports 2010*, ambayo pia ndani yake kunakuwa na *Zanzibar Human Rights Report.* Namuomba Mhe. Waziri aiangalie ripoti hii ukurasa wa 376-377 imezungumzia *discrimination government employment,* imezungumzia *no advantage government opportunities, law salaries* huko naweza kujua pengine tuna kazi ya kufanya mpaka tufike tupate usahihi. Lakini nilipo mimi ni kwenye *the rise of labour disputes* naomba kidogo niisome *paragraph* hii.

Mhe. Spika, inasema, '*acording to report of the labour commission is that more than hundred and seven cases concerning the rights to work has be reported to the commission from January till September 2010. 92 cases from urban region of Unguja and 50 are from south district of Unguja. Main of them are concerned with the improper dismissal from work which involve public and private sectors. The power to entertain matters relating to workers rights is rested to labour tribunal. This tribunal is presided by chairman appointed by the President for the term of five years. The tribunal handled all the cases from Unguja and Pemba'.*

According to the record obtained shows that nine cases has been instituted in this tribunal work to 2010. But in general the speed to disposal cases to this tribunal is very slow. This is cause due to insufficiant stuff to this tribunal. The tribunal is presided by the High Court Judge with been attending tribunal once in a week. However, the year 2010 ended without the judge of the tribunal and the respective judge has been transferred to another post. It is recommended that the permanent judge to be appointed and the court be stuffed.

Kwa hivyo, nilikuwa naomba Mhe. Waziri pana mambo mengi hapa kwanza kuna hii Mahakama ya Kazi kwamba ina maelezo yake kama ilivyoelezwa hapo, lakini pili inaonekana kuna tatizo la kusimamia haki zetu za wafanyakazi katika maeneo mengi. Katika hilo Mhe. Spika, nina kesi asubuhi nimeletewa namuomba Mhe. Waziri nitampa hizi nyaraka azipitie kuna kesi ya Zantel Mhe. Spika, ilizungumzwa hapa. Mhe. Spika, kuna walinzi hawa 111 wameajiriwa kwa *temporary* na kama ni temporary stuff na mkataba wao wameingiza humu

mfano. Lakini hawa wameshamaliza *probation* ya miezi sita mpaka leo Zantel inashindwa kuwapa ajira.

Mhe. Spika, wamekwenda mbio wameandika barua kwa Katibu Mkuu Wizara ya Mawasiliano wameniletea kopi, wamemuandikia Waziri wa Katiba na Sheria wanasema pia waliiandikia Kamisheni ya Kazi. Kwa hivyo, nilikuwa naomba hili Mhe. Waziri apewe ili azipitie aone kiasi gani anaweza kesi kama hizo ambazo nimezitaja hapo.

Mhe. Spika, la mwisho katika hiyo sehemu ya kazi lilikuwa ni suala ambalo ameshalizungumza kwa urefu sina haja ya kulirejea Mhe. Mtando ni suala zima la usalama kazini. Mhe. Spika, ni kwamba wafanyakazi wetu wengi wanafanya kazi lakini zile standard za ku-*ensure safety work* hazipatikani. Kwa hivyo, nilikuwa naomba Mhe. Waziri alisimamie hili kwa ujumla wake ili na sisi tupige hatua tutoke kule tulikozea kufanya kazi kwa mazoea kama alivyosema Mhe. Waziri isiwe tu katika kujituma. Lakini hata katika kuweka vile viwango jinsi tunavyofanya kazi. Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, naomba niseme naiunga mkono bajeti hii kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mji Mkongwe mia kwa mia na namtakia kila la kheri Mhe. Waziri, ahsante sana.

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Nakushukuru Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa hii yakuchangia bajeti ya Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wananchi Kiuchumi na Ushirika. Awali ya yote kwanza naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye ametujaalia leo tukiwa hapa wazima na afya na uwezo wa kuweza kulitumikia na kulijenga taifa letu.

Mhe. Spika, la pili nakushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunipa na mimi fursa hii, mimi nitaanza moja kwa moja ukurasa wa 67.

Mhe. Spika, nimeanza na ukurasa wa 67 kwa sababu nimeona kwamba katika hotuba hii mbali ya kuwa ametupa mwelekeo wake wa mwaka 2011, lakini vile vile ametueleze dhana nzima ya uwezeshaji wa wananchi kiuchumi. Na hii amejaribu kufafanua vipi wananchi watawezeshwa kiuchumi.

Mhe. Spika, mimi nimeshukuru sana kwanza nimeshukuru kwa sababu wizara hii kwa kweli itawasaidia sana wananchi wa Zanzibar kuanzia mmoja mmoja, vikundi vidogo vidogo hata wale wazalishaji wakuu. Kwa kweli nashukuru sana na vile vile nimeona kwamba wizara hii ni wizara ambayo itaweza kujumuisha wizara nyengine zote, wizara hii lazima ifanye kazi kwa kweli na watu wote. Kwa maana hiyo nampongeza Mhe. Rais sana kwa kumteua Waziri wa Wizara hii Mhe. Haroun Ali Suleiman kwa sababu amejua kwamba Mhe. Waziri ana uwezo mkubwa wa kufanya kazi na wenzake vizuri. Mhe. Spika, mimi nampongeza sana Mhe. Rais kwa hilo.

Mhe. Spika, vile vile Mhe. Rais amewateua Makatibu na Wakurugenzi ambao hawa pia tunawafahamu wamekuwa watendaji kwa muda mrefu na ni watendaji wazuri. Kwa kweli nampongeza sana Mhe. Rais.

Mhe. Spika, nataka kuanza kwa ile dhana yakusaidia mtu mmoja mmoja pamoja na vikundi. Mhe. Spika, vyama vya ushirika havikuanza leo wala jana, mimi miaka kama 32 iliyopita nimejiunga na Jumuiya ya Vyama vya Ushirika na katika kujiunga huko nilibahatika kupata nafasi za kuhamasisha wanawake wenzangu kuingia katika vyama vya ushirika. Hiyo ni miaka 32 iliyopita na nimebahatika kwa kweli mpaka leo kuna vikundi ambavyo bado vina-*exist* na wanazalisha.

Mhe. Spika, nashukuru sana kwa hiyo kipindi chote hicho kumekuwa kunahamasishwa wanawake vijana kuingia katika vikundi vya ushirika. Kwa hivyo, mimi hofu yangu ni kwamba bado hatujatathmini, hatujatizama wangapi ambao wamefaidika na vikundi vya ushirika. Mhe. Spika, ili kuhakikisha kwamba huu mwelekeo ambao sasa Mhe. Rais ameitengeneza wizara hii ili kuhakikisha kwamba mwelekeo huu utatendeka vizuri lazima tutathmini nyuma ni kitu gani ambacho katika masuala ya ushirika labda tumekosea, au wapi ambapo tumefanya vizuri.

Mhe. Spika, vyama vya ushirika ndio njia pekee yakumnasua masikini kiuchumi, mwananchi wa kawaida ambaye anategemea kupata riziki yake katika biashara ndogo ndogo anaihitaji hii wizara imsaidie. Kwa hivyo, sasa wizara ina kazi kubwa tena sana kwa sababu elimu inahitajika, inabidi wizara ijikite katika kutoa elimi kwa hawa wahusika. Watu wengi na mwenyewe Mhe. Waziri katika hotuba yake amesema kuna asasi na vikundi mbali mbali vimekuwa vikisaidia katika kutoa elimu hasa za ujasiriamali lakini bado vile vile haijafanyiwa tathmini kujua hii elimu iliyotolewa imewasaidia wangapi. Sisi sasa hivi tunataka kuziunda sera, lakini sera hatuwezi kuunda bila ya kufanya utafiti wa kina, ili tuhakikishe tunatengeneza sera nzuri, tuna mikakati mizuri kuna umuhimu mkubwa wa kufanyia utafiti wa kina. Hilo moja.

Lakini la pili vile vile kama walivyotangulia wenzangu wamesema kuhusu hawa wanaofanya shughuli za vyama vya ushirika wamekuwa hawana uwezo wa kiuchumi, mtu anaanza biashara yake akiwa labda na shilingi 50 elfu hana uwezo wa kuiendeleza, biashara ya shilingi 50 elfu haiwezi kufika popote. Sasa hawa wameambiwa kwamba wanatiwa tama, ukianzisha ushirika utapewa hiki na mtapata mikopo mtapata nafasi, lakini hiyo haikufanyika hivyo. Kwa sababu hawa ambao wanaahidi kutoa mikopo kwa kweli wana vizingiti vingi sana mpaka kikundi kupata kusaidiwa na benki lazima kiwe kikundi ambacho kinajiweza vizuri sana.

Taasisi zetu nyingi ambazo ni za kifedha zinakataa kusaidia vikundi hivyo. Sasa mimi ningemuomba Mhe. Waziri aliangalie sana, ikiwa kama serikali yenyewe basi nashukuru kwamba kuna Mfuko wa AK na JK ambao mfuko huo mpaka sasa hivi ukiuliza sana katika sehemu mbali mbali wengi wanakuwa hawajui nani umemsaidia. Ingawa tunaambwia umesaidia watu, lakini wachache mno. Mimi ningeomba angalau utengenezwe Mfuko mwengine, sasa hivi utakuwa Mfuko wa JK na AS, huu tunaumaliza tuanze na Mfuko mwengine ili kuhakikisha kwamba wajasiriamali wetu nao wanafaidika katika kupata mikopo na misaada ya kifedha ili waweze kujiinua kiuchumi.

Mhe. Spika, mimi nafikiria kwamba kuna haja kubwa sana ya kuwasaidia vijana, vijana wengi wao hawana ajira na tatizo lenyewe tunasema kwamba ajira serikalini hazipo, lakini basi, hakuna ajira serikali lakini za kujiajiri wenyewe uwezekano huo upo. Vijana wetu wengi hawana elimu, hawajui waanzie wapi, wanataka kufanya kazi na wana ujuzi tunao vijana wengi ambao wamepata elimu mbali mbali lakini hawajui waanzie wapi.

Mimi nafikiri umeshafika wakati sasa hivi wizara kufanya kazi na Serikali za Mitaa, ku-*fetch data* za vijana ambao wako katika majimbo yote ili kujua vipi wataweza kuwachukuwa wale vijana na kuwasaidia katika kuwapa elimu ya kuanzisha vikundi vyao ambavyo vitawasaidia kiuchumi. Lazima tuwe na mpango thabiti ambao utahakikisha kwamba *data* zote za vijana hawa zipo na zile nafasi ambazo tunasema tunataka kuwapa vijana basi tuwape vijana wenyewe.

Mhe. Spika, naomba vile vile nichukue fursa hii kumuomba Waziri wet wa Uwezeshaji atusaidie kinamama. Nimetoka hapo nje Mhe. Spika, nimewakuta kinamama watupu ambao wamezalisha bidhaa mbali mbali ambazo ni nzuri na *quality*. Naishukuru wizara kwa sababu nimekwenda pale wameniambia kuwa wizara imewawezesha, ile hatua ambayo wameifikia sasa hivi wanaishukuru sana wizara kwa sababu imewawezesha ni kipindi kifupi sana alichokaa waziri lakini leo wananchi wanasema kwamba wanashukuru. Kwa kweli hiyo ni hatua, lakini tusiwaachie hapo mkono.

Nafikiria kwamba tuwe tunajaribu ku-*focus* mfano tukisema tunataka kueneza elimu, lakini hebu tu-*focus* kwenye makundi Fulani. Nasema hivyo kwa sababu hii elimu tunaitaka iende kwa kila mtu sio kila mtu ambaye anawezakuwa mjasiria mali. Sasa hivi vikundi ambavyo vimeanzishwa tayari wameanzisha shughuli za kiuchumi hawa wawezeshwe zaidi wao wanaweza kuajiri wenzao. Sijui Mhe. Waziri kama ananielewa. Hivi vikundi vya akinamama ambavyo vinazalisha mali ambazo zinatumika kila siku katika maisha yetu.

Kuna vikundi nimevikuta hapo vinazalisha achari, pilipili, mboga ya mayugwa na nyenginezo hawa wawezeshwe zaidi, hawa wanaweza kuajiri wenzao, vijana wetu wanaweza kupata ajira *through* hawa wazalishaji. Kwa sababu wengine hawana uwezo huo kabisa.

Halafu Mhe. Waziri nakuomba watendaji wako nao wawasaidie hawa wafanyabiashara wadogo wadogo kuwa wabunifu. Kuna umuhimu mkubwa sana wa kuwa wabunifu, wawawezeshe ili waweze kuwa wabunifu. Kwa sababu nimeona mama ametengeneza *vase* za kuwekea maua kwa kutumia chupa ya *plastic*, leo tunazungumzia mazingira yanaharibika na moja kinachoharibu mazingira ni chupa za *plastic*. Lakini mama kwa ubunifu wake mwenyewe kazichukua akazitengeneza na kufanya *vase* za *gold* za kuwekea mauwa za kupambia nyumbani. Uwezo mkubwa sana Mhe. Spika. Watu wabunifu kama hawa tuwaengeenge, watu hawa wanaweza kuanzisha kiwanda kidogo ambacho kitaajiri vijana wetu, hawa wanaweza kulipa kodi tukapata fedha zitakazosaidia katika afya, elimu na masuala mengine ya huduma.

Kwa hivyo Mhe. Spika, mimi nasisitiza zaidi katika kuwawezesha vikundi ambavyo tayari viko katika shughuli hizi za kiuchumi, vikundi vya akinamama pamoja na vikundi vya vijana. Tukiweza hapo kwa kweli tutakuwa tumejikwamua kwa asilimia kubwa sana ya kiuchumi.

Mhe. Spika, sasa kidogo nizungumzie masuala ya ajira na kazi. Mhe. Ismail Jussa alizungumza hapa na nilimuunga mkono, amezungumzia suala la ajira, kuna mwakilishi mwengine amezungumzia suala la mikataba, yote hayo ni haki za watu ambao wanatafuta ajira. Mara nyingi sana hawa watu wanakuwa hawana elimu au hawana ujuzi wa kujua kwamba ile ni haki yake kupewa mkataba wa kazi. Kwa sababu mkataba wa kazi mara nyingi anayeajiri anaukimbia ili asimpe mfanyakazi haki zake, hawa tunaowazungumza zaidi ni wale *investors* wakubwa wakubwa, wanakimbia sana kuweka mikataba, yoto hayo ili wahakikishe kwamba wanawabinya wale wazalendo haki zao na wao waweze kujirundikia zaidi. Sasa Mhe. Waziri nakuomba suala hili ulishughulikie sana.

Lakini jengine Mhe. Jussa alizungumzia kuhusu muajiri kutoa haki za afya. Wafanyakazi wengi ambao wanafanya kazi sehemu mbali mbali hata serikalini basi kwa kweli huduma ambazo zitakuwa zinawaweka katika afya nzuri hazipo. Mfano mdogo tu, tukitizama hata hawa wafagiaji barabarani wanakosa vifaa muhimu ambavyo vitawasaidia katika kujikinga wao kiafya, wanakosa hata zile *musk* za kujifunika kwa sababu ya vumbi na hawa baada ya miaka fulani watakuwa wagonjwa. Wizara ya Afya inachukua jukumu tutasema Wizara ya Afya hawafanyi kazi zao vizuri lakini tumeanzia huku.

Mhe. Waziri kweli na umasikini wetu lakini tujikaze tuangalie yale mambo muhimu, tupunguze kwengine tuongeze kwengine, tunataka taifa lenye afya, tunataka wafanyakazi wenye afya. Ili wazalishe vizuri na wafanye kazi zao vizuri basi tuhakikishe kwamba tunalinda afya zao.

Mhe. Spika, baada ya hapo nachukua tena fursa hii kumpongeza sana Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika na nakutakia mafanikio mema na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atakujaalia utatimiza kazi yako vizuri. Mimi nakufahamu Maalim Haroun Ali Suleiman tumetoka mbali, tumeanza kazi tukiwa wadogo, tukiwa na miaka 17 pamoja na Bi Fatma Abdulihabib Fereji tulikuwa pamoja. Kwa hivyo, uwezo wa Maalim Haroun naufahamu na naamini kwamba ataweza kufanya kazi yake vizuri. Nakushukuru Mhe. Spika, naunga mkono hoja.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe jana wakati wa kuahirisha kikao nilipata maombi kama mawili au matatu hivi, lakini sikuwahi kuyaandika. Sasa sina hakika kama ilikuwa ni maombi ya kutaka kuchangia au laa. Kwa hivyo, kama kuna wajumbe ambapo tayari nimeshamuona Mhe. Hija Hassan Hija basi walete maombo hayo na tupate kufunga mjadala huu.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nachukua nafasi hii kwanza kukushukuru na kwa kweli nikupongeze sana kwa sababu umekuwa makini na bado kumbukumbu unazo nzuri sana. Miongoni mwa watu ambao walipeleka maombi hayo mwisho ni mimi na Mhe. Ismail Jussa, nikupongeze kwamba bado uko makini na una kumbukumbu nzuri sana.

Mhe. Spika, nianze na mimi kumpongeza Mhe. Waziri kwa jinsi ambavyo ametoa kitabu kizuri akatuwekea mpaka picha za watendaji wake. Hii ni dhahiri kwamba wizara hii inajali uwazi na uajibikaji. Kwa sababu bila shaka wengine tulikuwa hatuwajui wakurugenzi wake na leo ametuonesha kwamba hawa ndio watendaji wangu chini ya wizara yangu.

Mhe. Spika, nianze na ukurasa wa sita Mhe. Waziri amekusudia kutuonesha dhana ya uwezeshaji na akatwambia kwamba kuna kiambatanisho Nam. 1 ingawa nimepekua ndani ya kitabu hiki sikukiona, pengine kimesahauliwa au labda akija anifahamishe kiko wapi kiambatanisho hicho ambacho kinafafanua dhana ya uwezeshaji kwa wawakilishi.

Mhe. Spika, jengine ambalo nilizungumze Mhe. Waziri ukurasa wa 7 amezungumzia Dira ya Wizara ambapo ni kuona jamii ya Wazanzibari wenye fursa ya kutosha ya ajira na vipato endelevu. Mhe. Spika, nadhani hii ni dira nzuri na ni malengo haya ya wizara chini ya Mhe. Waziri ni mazuri na yanahitaji kusimamiwa. Lakini kwa mtazamo wangu ili malengo na dira hizi

zifikiwe lazima kuwe na uwazi, kuwe na ukuaji wa soko la ajira, kuwe na uboreshaji wa vipaumbele na kuwe na msingi wa fedha imara. Wanaweza wakaona dira nzuri lakini bila ya mambo hayo manne ambayo yatasimamie malengo hayo ya wizara kwa kweli itakuwa hatuna mafanikio mazuri. Kwa hivyo, Mhe. Spika, serikali sasa izingatie dira hii ya wizara waweze kuwapatia fedha za kutosha kwa ajili ya kufikia malengo ambayo Mhe. Waziri ametueleza kwenye hotuba hii.

Mhe. Spika, vile vile Mhe. Waziri ametuonesha kwamba kuna kitengo cha kupokea taarifa kuhusu soko la ajira, ametwambia kwamba tayari kuna wafanyakazi sita ambao wamepata mafunzo. Mimi kwa niaba yangu na wananchi wa Kiwani nimpongeze Mhe. Waziri kwa kuwapatia mafunzo watendaji hao sita. Nimuombe tu kwamba, ikiwa kuna uwezekano basi watendaji hao waongezwe kwa sababu wasiwasi wangu ni kwamba watendaji sita watakuwa hawatoshi.

Sambamba na hili Mhe. Spika, nimuombe Mhe. Waziri kuwapatia mafunzo ni sehemu moja lakini vitendea kazi ni sehemu nyengine muhimu ambayo nadhani inahitajika kuwapatia watendaji hawa.

Suala jengine niende kwenye Idara Utumishi na Uendeshaji. Mhe. Waziri ametuonesha hapa kwamba kuna wafanyakazi 20 amewapatia mafunzo ya muda mrefu katika vyuo mbali mbali tena kwa fani mbali mbali za elimu. Mhe. Spika, kati ya hao wafanyakazi 20, 19 ni kutoka idarani sikujua ni maeneo gani, lakini mmoja ni kutoka Pemba. Lakini Mhe. Spika, bahati mbaya Mhe. Waziri hakutuonesha kuwa wafanyakazi hawa 20 wametumia shilingi ngapi na wamesoma katika vyuo gani nje na ndani ya nchi. Kwa hivyo, Mhe. Waziri labda akija anambie kwamba mafunzo ya wafanyakazi hawa yamegharimu shilingi ngapi za kitanzania na yamefanyika katika nchi gani ndani na nje ya nchi.

Mhe. Spika, jengine Mhe. Waziri amezungumzia Afisi ya Waziri na amezungumza habari ya safari ambazo amefanya Mhe. Waziri. Mimi nataka nimpongeze binafsi, lakini nirejee pale ambapo Mhe. Jussa amesema kwenye safari za nchini Qatar. Aliporejea bila shaka aliwatangazia Wazanzibari juu ya nafasi za kazi mbali mbali na nimwambie tu kwamba hivi sasa shehia mbali mbali au wilaya mbali mbali Wazanzibari wamejaza fomu kwa gharama ya shilingi laki moja na ishirini na tano kwa ajili ya safari nchini Qatar halafu Mhe. Waziri atwambie, kwanza ujazaji huu wa fomu ni halali. Kwa sababu wasiwasi wangu isije ikatokea kama ile mipango ya Desi au Miradi wa Malaria kule Pemba, ambayo Wazanzibari walijaza fomu kwa ajili ya kupatiwa kazi za malaria lakini hadi hii leo fedha hazikupatikana.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, labda Mhe. Waziri anambie utaratibu huu wa serikali upo kihalali na kwamba wizara yake inajua? Je, ili Mzanzibari apate nafasi ya kwenda nchini Qatar masharti gani ambayo yamepangwa na serikali ili tuweze kuyajua.

Mhe. Spika, sambamba na hilo ningetaka Mhe. Waziri anambie basi nini kigezo cha kupatiwa nafasi hizo? Kwa sababu zipo taarifa kwamba baadhi ya wilaya zimefanyiwa utaratibu huo lakini hadi hii leo kuna wilaya na majimbo hayajapatiwa fursa hizo. Kwa hivyo, labda safari za Qatar Mhe. Waziri amezigawa kwa utaratibu gani.

Mhe. Spika, nikiendelea na suala hilo kwenye idara hii Mhe. Waziri ameomba shilingi 300,082, 000 kwa ajili ya kazi za kawaida na maendeleo, lakini ametenga shilingi milioni 53 kwa ajili ya safari za ndani na nje ya nchi na vile vile ametenga shilingi 47.5 milioni kwa ajili ya mafunzo. Naomba kujua tu, fedha hizo za mafunzo shilingi 47..5 amelenga kuwasomesha watendaji wangapi kwenye idara hii. Kwa sababu unaweza ukaweka fedha lakini usitwambie watu wangapi umewalenga mwisho wa mwaka ukatwambia nimesomesha watu wanne. Naomba kujua ni watu wangapi amelenga kuwasomesha kwa fedha hizo na ni maeneo gani nje ya nchi au ndani ya nchi.

Mhe. Spika, jengine ni suala zima la mikopo na nianze kwenye Mfuko wa Kujitegemea. Mhe. Spika, mwaka jana Mhe. Waziri ametwambia Mfuko wa Kujitegemea umetoa mikopo shilingi 83,800,000/- kwa watu 131. tukisema hivi maana yake ametoa mikopo hii kwa kila mtu mmoja kwenye thamani ya shilingi 639,694/- na kwa maana hiyo ametoa mkopo kwa kila mtu mmooja kwa mwezi shilingi 53 elfu, na kwa maana hiyo ametoa mkopo kwa mtu mmoja kwa siku shilingi 1,700. Mhe. Spika, tukizungumza mkopo wa Wazanzibari shilingi 1,700 kwa siku maana yake unampa mwanamke au mwanamme kiasi hicho cha pesa kwa ajili ya kufanya biashara ajikwamue kwenye mazingira magumu, kwenye viashirio vya madawa ya kulevya, UKIMWI na umasikini.

Mhe. Spika, kwa hivyo, nawaomba wawakilishi wenzangu kwamba wakizungumza shilingi 83,800,000 maana yake wanazungumza shilingi 1,700 kwa siku, Wazanzibari ndio pesa walizopewa kwa ajili ya kutafuta maisha yao ajiondoshee umasikini na matatizo. Nadhani Mhe. Spika, bado ni mzaha, fedha ndogo na kama serikali imeunda wizara hii kwa nia yakuwaondoshea umasikini Wazanzibari basi nadhani fedha hapa iongezwe sana.

Mhe. Spika, katika hilo wanawake ambao wamefaidika na mikopo hii ni wanawake 78 ambao wamepatiwa shilingi 32.5 milioni sawa sawa na shilingi 1,159 kwa siku. Mzanzibari mwanamke tumemkopesha kwa siku shilingi 1,159

maana yake tunamwambia mwanamke akafanye maandazi, akauze matunda, mihogo kwa shilingi 1,159. Mhe. Spika, nadhani bado wananchi wetu hatujawafanyia haki na ndio maana kipimo cha umasikini kuondoka hatukioni maisha. Kwa sababu hakuna mtaalamu wa uchumi atakauyemuwezesha mwanamke shilingi elfu moja akamuendeleza akatajirika akaondosha umasikini wa kipato.

Mimi nsema tusisahau kwamba wanawake ndio ambao wanabeba jukumu kubwa la kulea watoto, tumeambiwa takwimu za Idara ya Ustawi kwamba, watoto wenye mazingira magumu Zanzibar ni laki moja ambao hawana kipato, wanakabiliwa na matatizo ya UKIMWI, wanakabiliwa na mtapia mlo, leo unampa mwanamke shilingi 1,159 kwamba ndio hizo sasa afanye biashara ajiondoshee matatizo na aondokane na masuala ya vitendo visivyo halali kama uasharati, madawa ya kulevya na mambo mengine.

Mhe. Spika, nadhani hili ni dogo, lakini ukiangalia takwimu hii bado wanaume wamekuwa mbele. Wanaume wamepewa shilingi 80 milioni sawasawa na shilingi 2,686 kwa mwanamme mmoja. Mhe. Spika, bado idara hii kuna mfumo dume na wanaume bado wanapata tatizo kubwa la mkopo na wanawake wako nyuma sana kwa mkopo. Nasema kwamba mimi ningependelea wanawake wakapewa kipaumbele kwa sababu ndio wanaoishi na watoto majumbani kwa faida ya kuwasaidia skuli na masuala mengine.

Mhe. Spika, jengine ambalo limezungumzwa hapa ni Mfuko wa AK na JK. Wazanzibari wanapoambiwa Mfuko wa AK na JK wanadhani kwamba ile fedha ni kutoka kwa Rais Karume na Rais Kikwete ndani ya mfuko wake. Kwa upande wangu nadhani ni idhini ya marais wetu kwa benki kuwa wakopesheni Wazanzibari kama *guarantee* kutoka kwa Rais wa Zanzibar na Rais wa Tanzania. Sasa hapo ni tatizo Mhe. Spika, Mzanzibari ukimwambia ni Mfuko wa AK na JK anadhani ni pesa sadaka kutoka kwa rais, Mhe. Spika, tuwe wazi tuwaambie kwamba hizi ni fedha za benki ambayo *guarantee* yake ni kutokana na marais wawili na ndio maana ukiona Pemba wamepewa 0.5 bilioni kwa asilimia 88.8 ya mkopo, lakini marejesho yake ni asilimia 31. Watu wamesahau kwamba hii fedha ni ya benki, ni *public money* irejeshwe.

Mimi nilipokuwa kwenye kamati walitwambia hasa Micheweni kwamba hii fedha ni ya baba rais kwa hivyo usitudai. Kwa hivyo, nadhani Mhe. Spika, serikali sasa ijenge hoja na ielimishe kwamba hii fedha ni fedha ya umma, unakopeshwa wewe leo kesho uirejeshe apate mwenzako, lakini kuiachia fedha hii bila ya usimamizi mzuri nadhani fedha hii itapotea na niseme tu kwamba si wazo zuri kabisa kurejesha fedha hii wizarani. Kwa sbabau ikiwa benki hairejeshwi kama Mhe. Jussa alivyosema nadhani na wizarani ndio itazidi kupotea.

Mhe. Spika, jengine ambalo ningelisema la mwisho kabisa kuna wenzangu wameseme ni vyema sasa kwamba Vyuo vya Amali virejeshwe Wizara ya Kazi. Mhe. Spika, nataka niwakumbushe wenzangu kwamba vyuo hivi kabla ya kwenda Wizara ya Elimu vilikuwa Wizara ya Kazi, baadae Mhe. Haroun watendaji wake wakajenga hoja kwamba vyuo hivi vipelekwe Wizara ya Elimu ni hoja sahihi, leo tukijenga hoja virejee kwa Mhe. Waziri wa Kazi maana yake itakuwa vyuo hivi vinamfuata Mhe. Haroun.

Mhe. Spika, hili naomba nirejee, vyuo hivi vilikuwa Wizara ya Kazi. Mhe. Waziri kwa busara za kitaalamu akajenga hoja kwamba vyuo hivi viende Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, tukampelekea vyuo hivi leo tukisema tuvirejeshe Wizara ya Elimu viende Wizara ya Kazi maana yake vyuo hivi vinamfuata Mhe. Haroun kila anapokwenda, kesho akiwa rais maana yake tumpelekee Ikulu vyuo hivi. Mimi nadhani hivyo vyuo bado vibakie Wizara ya Elimu na Wizara ya Kazi kama kuna *component* ambayo wanahusika waendelee kuvilea lakini si busara kabisa kuvitoa Wizara ya Elimu kuvipeleka Wizara ya Kazi itakuwa hatujafanya la maana Mhe. Spika.

Mwisho kabisa niseme tu kwamba, serikali lazima itafute fedha kwa ajili ya kuwapanga Wazanzibari kuwakopesha na tuachane kabisa na mtindo wa kuwapa shilingi mia mbili za andazi. Wazanzibari ni masikini wanahitaji kusaidiwa, kutetewa na watetezi wa Wazanzibari ni sisi Wawakilishi.

Mhe. Spika, baada ya hayo niunge mkono hoja hii na niwaombe wenzangu kwamba leo hakuna buti tumpitishie mwenzetu ili aanze kufanya hii kazi. Mhe. Spika, ahsante.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Spika, kunipa nafasi hii nami nikaweza kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika, (Maalim Haroun Ali Suleiman).

Mhe. Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia mchana huu wa leo kukutana hapa katika Baraza lako tukufu kwa madhumuni ya kuendeleza michango mbali mbali inayohusu bajeti mbali mbali za serikali. Lakini kwanza nitumie nafasi hii kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na Katibu Mkuu na wasaidizi wake ambao Mhe. Waziri bahati nzuri ametuwekea hapa katika sura ya kitabu chake ili tuwaone kwa kuandaa hotuba hii nzuri, imefahamika, imeeleweka, ikiwa pamoja na kitabu chake kizuri, kinasomeka vizuri kwa hivyo tunampongeza sana Mhe. Waziri.

Lakini pili nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuanzisha wizara hii mpya, wiazra hii muhimu kwa ajili ya mustakabali mzuri wa wananchi wetu. Ni wizara muhimu sana kama

ilivyoelezwa humu kwenye kitabu. Lakini pia nimshukuru kwa kumchagua Mhe. Waziri, Haroun Ali Suleiman kuiongoza wizara hii na sisi tunaamini kwamba uteuzi wake huu wa wizara hii utasaidia sana kuinyanyua hali ya wananchi wetu kiuchumi.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri hapa ametueleza kwamba moja kati ya jukumu lake kubwa ni kusimamia na kuratibu program zinazolenga katika kukuza ajira na kunyanyua kipato cha wananchi hususan wale wenye kipato cha chini ili waweze kumudu maisha yao ya kila siku.

Mhe. Spika, kwa kweli hili ni jukumu kubwa sana ambalo Mhe. Waziri amepewa na serikali. Kama tunavyofahamu kwamba wananchi wetu sasa hivi walio wengi kipato chao ni kidogo ukilinganisha na matumizi. Hii ndio changamoto kubwa ambayo serikali yetu inakabiliana nayo. Kwa kuwa Mhe. Rais ameamua kwa makusudi kumpa Mhe. Waziri jukumu hili, tunaamini kwamba ataifanya hiyo kazi ili wananchi wetu waweze kuishi katika maisha yaliyokuwa afadhali kidogo.

Mhe. Spika, kwa kweli suala la kuwanyanyua wananchi wetu kiuchumi ni suala zito na linahitaji kuratibiwa na kuwa na mipango iliyokuwa madhubuti kabisa. Kwa sababu tumeanzisha hapa mambo mengi na mambo haya lengo kuu ni kuona kwamba wananchi wetu wanaondokana na umaskini. Tumeanzisha mifuko kama hii ya JK na AK, kuna Mfuko huu wa Kujitegemea, tumeanzisha Idara ya Vyama vya Ushirika, hivi vyote vikiwa na lengo kwamba wananchi waweze kupata nafasi ya kuitumia fursa ya mifuko hii pamoja na Idara hii ya Vyama vya Ushirika kwa ajili ya kujikwamua na umaskini.

Lakini Mhe. Spika, pamoja na lengo zuri ambalo serikali imeweka kwa ajili ya kuanzisha mifuko hii, bado inaonekana kwamba haijaweza kukidhi kiu ya watu wetu. Kwa mfano, mfuko huu wa JK na AK ambapo kwa mujibu wa takwimu ambazo Mhe. Waziri ametueleza hapa katika Wilaya ya Mjini wananchi waliofaidika na mkopo huu ni 141. Mhe. Spika, kiwango hichi ni kidogo mno. Ukiangalia idadi halisi ya wananchi wanaoishi katika wilaya hii na wale wanaoishi katika hali isiyoridhisha ni kiwango kidogo ambacho kwa kweli hakiwezi kukidhi ile haja ambayo imekusudiwa.

Kwa hivyo, kama serikali ina azma ya kupambana na jambo hili, ni lazima wizara hii iwezeshwe na kuwe na mipango madhubuti kuona kwamba wananchi wetu wanaondokana na tatizo la umaskini.

Mhe. Spika, mimi katika jimbo langu katika mfuko huu wa JK na AK kuna fomu zisizopungua 300 ambazo zimetolewa katika shehia 6, kila shehia ni fomu 50. Lakini kwa mujibu wa taarifa za masheha wangu wa shehia zote

hakuna mtu hata mmoja aliyeweza kufaidika na mkopo huu. Sasa kwa kweli taarifa hizi haziridhishi na inaonesha dhahiri ni namna gani hakukuwa na utaratibu madhubuti wa kugawana rasilimali hii. Haiwezekani kwamba jimbo zima hakuna hata mwananchi mmoja aliyefaidika na mkopo huu. Pia haiwezekani katika wananchi 300 waliokuwa wameomba waliopewa fomu kwamba wote hawakufikia vile viwango vya kupata mkopo.

Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri, yeye ni waziri mpya katika wizara hii asimamie hili kuona kwamba hii rasilimali ndogo tuliyokuwanayo basi inagawiwa na inamfika kila mtu kwa kadri hali inavyokuwa. Si vyema kwamba rasilimali hii wakafaidika watu wachache na wengine wakashindwa kufaidika. Ndio maana hata Mhe. Omar Ali Shehe hapa wakati akichangia alizungumzia haja ya kuona wazi katika mikopo hii badala ya kupata zile takwimu zilizokuwa zimejibana. Pengine tunazungumzia takwimu za fedha zilizotolewa lakini wale waliofaidika wakawa hawaonekani panaweza kuwa pana sura ambayo sio ya kiadilifu.

Kwa hivyo, tungemuomba sana Mhe. Waziri na mimi niungane na Mhe. Omar Ali Shehe kwamba sasa wakati umefika wale ambao wamepewa ile mikopo waonekane kwa majina yao na shehia zao ili tuone kweli fedha hizi ambazo zinaelezwa humu zimewafikia walengwa.

Mhe. Spika, suala la kuwawezesha wananchi ni suala muhimu sana. Juzi tulikuwa kwenye semina Nungwi ambayo ilikuwa ina madhumuni ya kuonesha jinsi takwimu za watoto wetu wanaoishi katika mazingira hatarishi au magumu. Takwimu zinaonesha kwamba kati ya watoto wenye umri wa miaka mitano hadi miaka 17 ambao ni asilimia 44, ni asilimia 10 ya watoto wetu wanaishi katika mazingira hatarishi. Kwa hivyo, hii ni changamoto kubwa sana ambayo Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika inahitaji kushirikiana na Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Wanawake na Watoto kuona watoto wetu hawa ambao ndio rasilimali ya kesho na wao wanaishi katika mazingira mazuri.

Mhe. Spika, tunapozungumzia mazingira hatarishi maana yake watoto hao hawapati chakula cha kutosha, watoto hao hawapati elimu inayostahiki, lakini pia wanaishi katika makaazi yasiyokuwa bora na mambo mengine. Lakini hii yote inatokana na hali ya umaskini wa watu wetu. Unamkuta mama kachukua vitoto vyake kavibeba huku na huku anahangaika anakwenda huku na kule ili awatafutie chakula. Sasa kama tutawawezesha wananchi watakuwa na uwezo idadi hii ya watoto ambao wanaishi katika mazingira magumu kwa kiasi fulani itapungua.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri amepewa jukumu kubwa la kusimamia hilo na sisi tuna imani sana na wewe uwezo wako utautumia katika kuona kwamba hali hii inapungua. Kwa hivyo, tuna matarajio makubwa sana uwezo wako, usimamizi wako, ufuatiliaji wako, utasaidia sana kuondosha hali hii juu ya watoto pamoja na wazee wao kwa sababu hawa watoto wana na wazee wao. Lakini sisi tunazungumzia zaidi watoto kwa sababu hili ndio taifa la kesho.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo nije katika Kamisheni ya Kazi. Mhe. Spika, kumekuwa na malalamiko mengi juu ya wafanyakazi wetu ambao wanafanya kazi hasa hasa katika sekta ya mahoteli. Hata leo hii kwenye kipindi cha Mawio tuliwasikia Kaskazini "A" wakilalamika. Kumekuwa hakuna utaratibu mzuri wa watu wanaoajiriwa ndani ya mahoteli, hakuna utaratibu mzuri juu ya nani anafanya kazi wapi, anastahiki wapi, imekuwa ni vurugu tupu.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri hii ni changamoto kubwa na inastahiki uifanyie kazi ipasavyo kwa sababu bado malalamiko haya yapo mengi. Kama sheria zetu zipo lakini inaonekana bado hazijakidhi. Pamoja na kwamba umezungumza humu kwamba mnafanya utaratibu wa kufanya mapitio ya Sheria Nam. 4 ya mwaka 2005 kama sikosei, ili kuona sheria yetu inayosimamia masuala ya kazi basi inaendana na wakati.

Mhe. Spika, kumekuwa na malalamiko mengi ya wafanyakazi, kumekuwa na malalamiko mengi juu ya wananchi wetu wanavyonyanyaswa na wale wawekezaji wanaowekeza katika sekta ya utalii. Wamekuwa wanafanya shughuli hizi hawana wasi wasi. Kwa hivyo, ni lazima Mhe. Waziri wizara yake isimamie jambo hili kikamilifu ili manung'uniko kwa wananchi yapungue.

Mhe. Spika, kuna malalamiko ambayo Mhe. Ismail Jussa Ladhu ameyazungumza hapa na sisi wawakilishi wengine tunayapata kwamba sasa hivi mahoteli yamekuwa na taratibu ya kufanya *tours* zao. Hoteli zina magari yao wanayaweka pale yanafanya kazi kwa ajili ya *tour guide* katika maeneo mbali mbali, kazi ambayo ingeweza kufanywa na wazalendo. Kwa hivyo, hili ni jambo ambalo linahitaji kusimamiwa kwa karibu sana, wala si jambo la kubuni, ni jambo ambalo lipo na linahitaji uangalizi wa kutosha.

Mhe. Spika, la mwisho ni suala la Idara ya Vyama vya Ushirika. Mhe. Spika, idara hii ipo na maana yake ni kusimamia watu wetu kujiunga katika vikundi vya ushirika, lengo ni lile lile la kujiunga pamoja na kupanga mipango yao ili waweze kuondokana na umaskini. Lakini idara hii inahitaji kusaidiwa, kipindi kirefu imekuwa katika hali duni, ilikuwa chini ya Wizara ya Kilimo lakini idara hii ilikuwa duni, ilikuwa yatima nathubutu kusema hivyo, ilikuwa haina nyenzo, haina ofisi sijui siku hizi iko wapi.

Mhe. Spika, kama Mhe. Waziri atatembelea lile jengo walilokuwa wakilitumia ambalo labda wamehama sasa hivi basi utashindwa hata kufika katika jengo lao, jengo haliko katika hali nzuri. Tunapozungumzia Idara ya Vyama vya Ushirika maana yake idara hii iko karibu mikoa yote, wanahitaji kusimamia vikundi hivi vya ushirika katika wilaya zote. Kwa hivyo, wanahitaji kuwa na nyenzo za kufanyia kazi, wanahitaji kuwa na bajeti ya kutosha katika kufanikisha lengo lao. Lakini bado inaonekana bajeti ya idara hii si ya kuridhisha na haiwezi kukidhi haja.

Kwa hivyo Mhe. Spika, tuna matumaini kwamba wizara hii mpya ambayo imepewa kusimamia Idara ya Vyama vya Ushirika itaiangalia sana idara hii muhimu sana. Kwa sababu kama nilivyotangulia kusema lengo na madhumuni ya kuanzishwa idara hii ni kusaidia wananchi wetu kukaa pamoja na kuanzisha vikundi hivi vya ushirika ili kuona wanajikwamua kutokana na umaskini.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri aiangalie idara hii kwa jicho la huruma, vitendea kazi pamoja na majengo, jengo lao liko katika hali hatarishi kama walivyokuwa hawa watoto tuliowazungumza. Pia ikiwezekana Mhe. Waziri afanye ziara aende kuwatembelea akajionee mwenyewe hali yao sio nzuri kama hajapata nafasi ya kwenda.

Mhe. Spika, kwa hayo machache, naunga mkono hoja ya Mhe. Waziri, namtakia kila la kheri na baraka ili aweze kutusaidia katika kuondokana na huu umaskini uliokithiri kwa wananchi wetu. Ahsante sana.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Subhanahu Wataala ambaye ametujaalia kukutana hapa mchana huu tukiwa katika hali ya uzima na afya njema. Lakini pia nichukue fursa hii kukushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunipatia muda niweze kuzungumza machache katika kuchangia hotuba hii.

Mhe. Spika, tatu nimshukuru na kumpongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohammed Shein kwa uteuzi wake wa kutuchagulia Mhe. Haroun Ali Suleiman ili aweze kutuongoza katika Wizara hii ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika. Nasema Mhe. Rais hakupotea wala hakutia mkono kizani, ametuopolea waziri ambaye kweli anaweza kuyatekeleza majukumu haya hasa anaposhirikiana na watendaji wake hawa ambao ametuwekea hapa kutuonesha katika kitabu chake.

Mhe. Spika, nichukue fursa hii kumpongeza Katibu Mkuu wake ambaye ni mwanamama mahiri sana na mchapa kazi ambaye anaweza akashirikiana na Mhe. Waziri na viongozi wengine wote waliobaki wakatufikisha pahala pazuri.

Mhe. Spika, nianze mchango wangu katika ukurasa wa 27 Utekelezaji wa Malengo ya Mfuko wa JK na AK. Mhe. Spika, wenzangu wameeleza mengi kuhusu mfuko huu na mimi nimuombe Mhe. Waziri aweze kunieleza katika mkoa wangu ni vikundi vingapi ambavyo vimefaidika na mkopo huu na ni kiasi gani cha fedha ambacho kilitolewa ili tuweze na sisi kuzisimamia fedha zile kule. Wakishakuwajua hawa ambao wamepata katika vikundi tuweze kumsaidia yeye kazi kusimamia marejesho ya mikopo hii, lakini pia kuweza kudhibiti pale yatakapokuja maombi mengine kuweza kuwajua hawa tayari wamepata na tuwape fursa wengine ambao hawajapata hata kidogo.

Mhe. Spika, kusema kweli Unguja na Pemba vikundi vya ushirika tunavyo vingi sana pamoja na *SACCOSS* zake. Lakini Mhe. Spika, vikundi vyetu hivi vya wajasiriamali ni vyema kama walivyoeleza wenzangu kuweza kuvipatia elimu ili vikaweza kufanya kazi zake vizuri. Vikundi vipo na kwa sasa vinajitahidi sana lakini elimu yao inakuwa ni ndogo sana.

Mhe. Spika, nimuombe Mhe. Waziri pale anapovipatia elimu vikundi hivi basi aweze kuhakikisha hawaachi mkono kwa muda mfupi ili kuviendeleza kuhakikisha ile elimu anayopata na mafanikio yanapatikana.

Mhe. Spika, katika kuboresha hili basi kuweza kuweka hata wakaguzi ili waweze kufanya ukaguzi mzuri kwa yale mahesabu ya wanavikundi wetu, ili kuhakikisha zile fedha zinatunzwa vizuri na kupatikana marejesho ya mikopo ili na wengine wafaidike.

Mhe. Spika, vikundi hivi tunazalisha lakini bado uzalishaji wetu unaonekana tunao mitaani tu huko na hatuna fursa ya pahala pakuweza kupeleka vitu vyetu hivi ili tukaweza kujitangaza zaidi. Ni kama leo asubuhi hapa Mhe. Spika, umetutangazia kwamba wajasiriamali wapo nje hapo na wameleta bidhaa tukazione na pengine zitatuvutia tuweze kununua. Nimuombe Mhe. Waziri kutumia fursa hii tulikuwa na jengo letu la maonesho pale Tunguu, basi ni vizuri jengo lile tukalifufua na baadae tukaweza kulitumia kama wanavyotumia wenzetu Saba Saba, tukawa na sehemu yetu ya kwenda kuona tunaonesha bidhaa zetu na kujipatia soko.

Kwa sababu mfano tunao kama walivyoweka wafanyabiashara wetu minada pale siku ya Jumatano na Jumapili, wakati vinapopelekwa vifaa vile basi huweza kupatikana soko wakajiuzia na wakapata rizki zao. Kwa hivyo, wajasiriamali wetu ni vizuri wawe na pahala wanajitangaza na tunaweza tukapata hata wageni kuja kututembelea katika maonesho yetu hayo.

Mhe. Spika, niende katika Idara ya Ajira ambayo iko ukurasa wa 54. Mhe. Spika, wenzangu wamechangia sana katika idara hii na mimi naomba nichangie

kidogo hasa niende katika kifungu cha 2 naomba ninukuu kinasema "Kuongeza fursa zaidi za ajira kwa wazalendo."

Hili Mhe. Spika, nimuombe Mhe. Waziri aliangalie sana kwa sababu huwa tunasema tu wafanyakazi wetu hawana elimu na nafasi zinachukuliwa lakini ziko nafasi ambazo watu wetu wanaweza wakafanya kazi. Kwa mfano, wenzangu wameeleza hapa, basi hata kukata bustani ndio pia tupate mtu mwenye elimu kubwa, hata kusafisha meza na kuondosha vikombe pale wanapotumia wageni pia tupate wenye elimu kubwa na hizi zote tumenyang'anywa hatuna. Mhe. Spika, nimuombe Mhe. Waziri ajali sana.

Lakini Mhe. Spika, hata tukilinganisha wenye elimu hivi sasa watoto wetu wamejitahidi sana kusoma katika fani hii ya utalii. Mhe. Spika, Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali jana alipokuwa akifanya majumuisho yake hapa aliweza kutueleza kwamba alitoa wanafunzi katika Chuo cha Amali na wamekwenda kufanya majaribio mahotelini na wakapokewa na wakaweza kupata ajira. Huu ni mfano mzuri kwa hiyo Mhe. Waziri watu wetu tusiwabeze tunao na nafasi tuwapatie.

Mhe. Spika, niende katika vikundi hivi vya *SACCOSS.* Nimuombe Mhe. Waziri *SACCOSS Bank* hizi kama kweli zitawezeshwa zitaweza kutusaidia sana sisi watu wa vijijini na zitatupunguzia masafa ya kwenda mjini na kurudi, baadae huduma muhimu tutakuwa tunazipata kule kule vijijini.

Mhe. Spika, *SACCOSS Bank* kama zitawezeshwa na zikaweza kutoa mikopo kwa vikundi vya wakulima ambavyo vinalima mboga mboga na matunda, basi tunaweza tukasema tumezalisha na tunaweza tukapata fedha nzuri tu kuliko hata zile biashara ndogo ndogo ambazo hatuna uhakika nazo. Lakini kama tutawekeza kwenye kilimo tukaweza kuwakopesha wakulima wakalima vizuri mboga mboga na wewe mwenyewe ukatusimamia kupata soko vizuri, tusiagize nje baadae mboga mboga tueneze sisi wenyewe katika mahoteli tunaweza tukauza na fedha tukarejesha vizuri.

Mhe. Spika, nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa sababu hapa imeonesha zilitakiwa *SACCOSS Bank* zipatikane 14 kati ya Unguja na Pemba lakini tumefikia kwenye 11 ni hatua nzuri sana na naipongeza na nakutakia kila la kheri.

Mhe. Spika, nampongeza sana Mhe. Waziri kwa juhudi zake na utaratibu wake ambao ameuandaa katika kitabu hichi. Lakini pia huwa napenda kutumia fursa hii kuwakumbusha na wale wananchi ambao ndio sisi tunaohitaji mikopo. Ni vizuri niikumbushe jamii tuwe waaminifu, pale Mhe. Waziri anapotukopesha fedha hizi basi tuelewe kwamba tunakopeshwa kwa sababu ya kujikwamua na

umaskini. Kwa hivyo, twende moja kwa moja katika lengo ambalo tumekusudia la kukopa fedha kwa ajili ya kuimarisha vikundi vyetu. Tuache kwenda kukata masare na kununua vitu ambavyo havina maana baadae tukapoteza msingi mkuu ambao umekusudiwa hapa wa kutukwamua sisi kiuchumi.

Mhe. Spika, kinamama ni wajasiriamali wakubwa namuomba Mhe. Waziri awaone kwa jicho la huruma, ukiwawezesha kinamama maana yake umeiwezesha jamii nzima. Nakuomba utusaidie sana tuna vijana wetu ambao wapo kweli hawana kazi, kwa hiyo wape elimu ya kutosha vijana waweze kujiajiri tuweze kuupunguza umaskini katika nchi yetu.

Mhe. Spika, hii ni wizara mpya lakini mimi kwa mtazamo wangu ninavyoona na wenzangu wengi wataunga mkono hilo au wameshaunga mkono, Maalim Haroun Ali Suleiman ni mtu mtendaji, msikivu sana na anapokea ushauri sana wenye maana kutoka kwa wenzake.

Mhe. Spika, tulikuwa nae katika Wizara ya Elimu ambayo tunaiita WEMA na wema kawaida yake huwa hauozi milele unabakia. Naamini Mhe. Waziri juu ya hili atatufikisha pahala pazuri ambapo tunapakusudia, nasi tunakuunga mkono huko peke yako tutakusaidia kwa kila pale unapokwama tushauri, tuulize na sisi tutakupatia majibu.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia juu ya mia pamoja na wanawake wote wa Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, nakushukuru sana kupata fursa na mimi kusema maneno mawili matatu katika hotuba hii ya Bajeti ya Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika.

Mhe. Spika, sitaki nitoe shukrani sana kwa sababu muda utapotea kwa hiyo niende moja kwa moja kwenye pointi zangu. Lakini hata hivyo, namshukuru sana Mhe. Waziri kwa kupata fursa hii na imekuja wakati muafaka. Kwa sababu wizara yake ni wizara mpya na wakati huo huo tukiwa tuna Serikali ya Umoja wa Kitaifa wananchi wana matumaini mapya. Kwa hiyo, ikiwa wananchi wana matumaini mapya basi naamini na Mhe. Waziri kwa sababu wizara yake ni mpya basi na yeye atatufanyia mambo mapya yale mazuri tunayoyahitaji. Namuomba Mwenyezi Mungu amuwezeshe ili matumaini ya wananchi yaende pale palipokuwa ndipo.

Mhe. Spika, kwanza napenda nimwambie Mhe. Waziri kwamba mfuko huu ulioletwa wa JK na AK kwa kweli kipindi kilichopita fedha hizi zilitumika kwa ajili ya kupewa wananchi na nia ya mfuko ni ile ile ya kuwawezesha wananchi

kiuchumi. Lakini kwa bahati mbaya hizi fedha zilikuwa hazitolewi kwa utaratibu mzuri na hazifiki kule kwa walengwa. Kwa sababu wale wakubwa waliokuwa na hii mifuko basi ilikuwa wao ndio wanaozitumia hizi fedha, maana ilikuwa aidha anazipata mtu kwa urafiki au ujirani.

Mhe. Spika, katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba Wilaya ya Micheweni ni wilaya inayoongoza kwa umaskini. Mhe. Spika, naomba Mhe. Waziri anambie kule wilaya yetu ya Micheweni alitoa kipaumbele gani kutokana na mfuko huu. Kwa sababu ikiwa wananchi ni maskini na huu mfuko ulitolewa kwa ajili ya kuwawezesha watu kuwapunguzia huo ukali wa umaskini. Je, wilaya yangu ya Micheweni ilifaidika vipi na huu mfuko. Halafu atueleze kwamba utaratibu wake ulikuwa unakwenda vipi.

Kwa sababu kama alivyosema Mhe. Salmin Awadh Salmin kwamba mfuko huu kama haukutolewa kwa utaratibu maalum basi kuna uwezekano wa majimbo mengine wasifaidike kabisa. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kama nilivyozungumza wizara yake ni mpya, basi apange utaratibu ambao itakuwa kila jimbo la Zanzibar wanafaidika na mfuko huu. Namuomba pia atoe kipaumbele kwa Wilaya yangu ya Micheweni kwa sababu ni wilaya inayoongoza kwa umaskini.

Mhe. Spika, jambo jengine ni kwamba Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar ilifungua milango kwa ajili ya kuwakaribisha wawekezaji waje kuwekeza katika nchi yetu. Lengo na madhumuni ni kwamba wale walengwa wananchi wa visiwa hivi wapate faida na moja ni kupata ajira na kujikwamua na huo umaskini. Namuomba Mhe. Waziri na hili pia alisimamie vizuri ili kuhakikisha yale malengo ya serikali yanatimia.

Mhe. Spika, kwa mfano wawekezaji wanaokuja kuanzisha mahoteli basi wale walengwa hasa wananchi wa Zanzibar sio wanaofaidika na hizo ajira, wageni ndio wengi wanaofaidika na hizo ajira, ukizingatia zile ajira ambazo zina nafasi nzuri zote zinachukuliwa na wageni na wale wenyeji wanabakia na umaskini wao. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri asimamie kuhakikisha kama walengwa wanapata hizo ajira na pia ahakikishe kwamba hili suala la watu kufukuzwa kazi kiholela bila ya mkataba wowote ule basi wanalisimamia ili kupata ufumbuzi.

Kwa sababu wawekezaji wana tabia ya kuwafukuza watu kiholela na wakishawafukuza basi inakuwa ile kazi aliyofanya huku nyuma yote kama aliyejenga taifa hapati kitu chochote.

Mhe. Spika, kwa mfano hivi karibuni nimesikia kuna hoteli moja huku Nungwi kuna watu walifukuzwa kazi zaidi ya 70 kwa wakati mmoja. Mhe. Spika, hivi

kweli watu 70 wote wamefanya makosa kwa wakati mmoja, inaonesha huyu mwekezaji ni mkorofi. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri na hili nalo kupitia wizara yake asimamie kwa sababu yeye ana jukumu la kusimamia watu kuhusu suala hili kazi na mambo mengine.

Mhe. Spika, jengine lengo na madhumuni ni kusimamia uwezeshaji wananchi kiuchumi ili waweze kujikwamua. Sasa namuomba Mhe. Waziri aone kama watu wetu wanaojiajiri wenyewe na wao wanataka msukumo, msukumo wenyewe ni kuwasaidia kimawazo, kifikra, kinyenzo za kufanyia kazi. Kwa sababu wizara yake itakapowasimamia wananchi wetu vizuri kwa kuwapa maelekezo, elimu na fikra ya kufanya kazi, ile dhana ya kusimamia ajira binafsi na kujikwamua katika umaskini ambapo ni kutekeleza dira ya MKUZA itakuwa imefikiwa.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri awasimamie watu wetu na aone kama kuna haja ya kuchukua vikundi mbali mbali na kuwapa elimu kama vile wavuvi, wajasiriamali na wengineo, halafu yeye mwenyewe asimamie kuwawezesha. Mhe. Spika, ili kupata lengo maalum na kusimamia hili suala namuomba Mhe. Waziri awe na mtazamo wa kuwasaidia watu wetu.

Mhe. Spika, nitoe mfano, wale vijana waliopo Darajani tuseme na wao wajasiriamali japo kama hawana vikundi maalum lakini wamejiajri na lengo wanatoa msukumo kwa serikali kwa sababu wanalipa kodi kwa ajili ya serikali.

Sasa namuomba Mhe. Waziri wale vijana wasifukuzwe tu kiholela isipokuwa yeye kupitia kwake awatafutie sehemu nyengine nzuri ambayo wataweza kukaa kwa utulivu. Lakini wanaondoshwa hapa wanawekwa hapa, tuache ule mtindo wa kwenda wakisukumwa tu wakichukuliwa mali zao. Kwa sababu pale Darajani watu wa Baraza la Manispaa wanakwenda wanawafukuza halafu wanachukua mali zao, maskini ya Mungu wameshakwenda kukopa vitu vya watu Manispaa wanavichukua wanaanza tena alif kwa ujiti. Badala ya kuwa yeye akalipe vile vitu vya watu vimeshachukuliwa hana cha kulipa.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri wale watu awatafutie sehemu wawekwe wafanye biashara zao bila ya kubughudhiwa kwa sababu ile kusukumana kila mara haileti picha nzuri. Nchi yetu sasa hivi kama tunavyozungumza imo katika mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa, ina amani na utulivu, sasa ile kusukumana kila mara, watu kufukuzana, askari mkamate rudisha huko haileti picha nzuri. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia wizara yake wale vijana akae nao awashirikishe, awape elimu nzuri, awafahamishe kwa utaratibu. Wale ni binadamu na binadamu yeyote yule anapopewa elimu au maarifa yoyote yale basi anakuwa ni msikivu.

Mhe. Spika, kwa kuheshimu wakati wako naomba nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa sababu vitabu vyote tulivyopewa hakuna waziri hata mmoja aliyefanya kama hivi. Kwa hivyo, yeye katuletea kitabu hichi na watendaji wake wote, naomba na wenzake wengine waende kama hivi.

Mhe. Spika: Nakushukuru Mhe. Subeit Khamis Faki kwa mchango wako huo na kwa kujaribu kuokoa muda. Waheshimiwa Wajumbe kuna matangazo mawili. Tangazo la kwanza Mhe. Haji Omar Kheir Katibu wa Timu yetu ya Baraza la Wawakilishi ameniomba niwape taarifa kwamba mara baada ya kikao hichi kutakuwa na sherehe fupi ya kupokea vifaa vya michezo kutoka kwa rafiki zetu Kampuni ya Vinywaji Baridi ya Malta na shughuli hiyo itafanyika kwenye ukumbi wa hapo juu. Waheshimiwa wote tunaombwa tuhudhurie kwenye sherehe hiyo ya kupokea vifaa.

Lakini pili Waheshimiwa Wajumbe tumeshakaa muda mrefu kidogo katika ukumbi wetu na mahudhurio yetu jioni kidogo yanakuwa hayafurahishi hatufiki kwa wingi na mapema. Niwaombe basi jioni tufike mapema ili tumsikilize Mhe. Waziri ambaye ameniahidi atatumia muda mfupi kutoa majumuisho vizuri na baadae tupitishe vifungu vya wizara hii. Hapo hapo baadae tumuombe Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo nae awasilishe hotuba yake.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuijadili Bajeti ya Wizara ya Kazi,Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika kwa hali ya usalama na utulivu. Naomba nichukue nafasi hii Mhe. Spika, kukushukuru kwa dhati kabisa kwa namna ulivyowapa nafasi Waheshimiwa Wajumbe wakachangia bajeti hii, awali nilikuwa na matarajio hii ni wizara mpya nitapata michango kidogo, lakini kumbe kipya kinyemi. Alhamdulillah watu wamechangia kwa nguvu zao zote nashukuru sana.

Bajeti hii ilipata nafasi ya kuchangiwa na Waheshimiwa Wajumbe 29. Wajumbe 24 walichangia moja kwa moja na waliobakia watano walichangiwa kwa maandishi. Naomba kwa ruhusa yako Mhe. Spika, niwataje wale wote ambao wamechangia bajeti yetu hii ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika. Waliochangia ni kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Salim Abdalla Hamad (Kny: Mhe. Asha Bakari Makame, Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari)
2. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
3. Mhe. Rashid Seif Suleiman
4. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa
5. Mhe. Mussa Ali Hassan
6. Mhe. Nassor Salim Ali
7. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi
8. Mhe. Suleiman Hemed Khamis
9. Mhe. Abdi Mosi Kombo
10. Mhe. Omar Ali shehe
11. Mhe. Fatma Mbarouk Said
12. Mhe. Bikame Yussuf Hamad
13. Mhe. Abdalla Moh'd Ali
14. Mhe. Ashura Sharif Ali
15. Mhe. Mohammed Haji Khalid
16. Mhe. Rufai Said Rufai
17. Mhe. Mbarouk Wadi Mussa
18. Mhe. Mohammed Mbwana Hamad
19. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
20. Mhe. Mgeni Hassan Juma
21. Mhe. Hija Hassan Hija
22. Mhe. Salmin Awadh Salmin
23. Mhe. Panya Ali Abdalla
24. Mhe. Subeit Khamis Faki

Hao wote walichangia moja kwa moja na waliochangia kwa maandishi ni:-

1. Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano
2. Mhe. Ali Abdalla Ali
3. Mhe. Salum Amour Mtondoo
4. Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali pamoja na
5. Mhe. Shadya Mohammed Suleiman.

Mhe. Spika, kwana nitoe shukursani za dhati kabisa kwa namna ya michango ilivyotolewa. Kwa kweli michango yao itakuwa ni dira na itakuwa ni sehemu ya utekelezaji wa majukumu yetu ya kiwizara. Naomba nichukue nafasi hii Mhe. Spika, kuwahakikishia Wajumbe Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika tumekusudia katika kipindi cha miaka mitano ijayo kwa kiasi kikubwa kuwawezesha wananchi wetu kiuchumi ili waondokane na tatizo kubwa sana la umasikini na hilo litawezekana kwa mashirikiano ya pamoja kati ya wizara na jamii wakiwemo Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu.

Napenda niwahakikishie upande wangu nitatoa mashirikiano ya aina zote pamoja na watendaji wote ambao waliwaona kwenye picha na wale ambao hawakuwemo kwenye picha lakini wanasaidia shughuli zetu kwa njia moja au nyengine.

Mhe. Spika, mengi yamezungumzwa lakini mimi nitazungumzia yale ambayo kwa ujumla na sitoweza kwenda kwa mtu mmoja mmoja na pale itapobidi kumtaja Mheshimiwa…

Mhe. Spika, samahani, kama hizo karatasi zinazogawiwa zinahusu Wizara ya Kazi naomba utoe agizo kuwa zizuwiwe kugawiwa kwa sababu nitazozieleza. Zote zikusanywe naomba Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Kama hizo karatasi zinazogawiwa zinahusu Wizara ya Kazi mwenyewe ambaye alizileta anasema usizigawe. Kwa hivyo, msizigawe na zilizogawiwa tukuombeni basi mzikusanye kwanza, pengine kuna makoseo fulani.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, zikusanywe na ukabidhiwe kwenye meza yako halafu nitasikiliza muongozo wako baadae. Ahsante.

Mhe. Spika, nakushukuru na nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe na nawaomba sana hizo karatasi wazirejeshe haraka huko kwa sababu ya mambo Fulani.

Mhe. Spika, jambo kubwa ambalo limejitokeza katika suala zima la mjadala wa bajeti yetu ni masuala ya Mifuko ya AK na JK, masuala ya ajira na namna gani tunaweza kuwawezesha wananchi kwa ujumla.

Kwa hivyo, nitatowa kwa muhutasari yale yote ambayo nitajaaliwa kuyawasilisha kwa muda huu ambao nataka *Inshaallah* isizidi saa moja. Mhe. Spika, suala la mikopo ya AK na JK lilizungumzwa sana. Waheshimiwa wananchi huko mitaani wana hamu ya kusikia majibu ambayo yatatolewa na waziri na niko tayari kufanya hivyo.

Mhe. Spika, pia nataka niwatowe wasi wasi Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu, kwamba mifuko hii haikutolewa kwa upendeleo wa aina yoyote, hilo la kwanza. La pili mifuko hii haikuangalia jinsia, eneo au jambo lolote lile linaweza kubagua kwa sehemu moja au sehemu nyengine. Hata hivyo, nakiri kwamba kulikuwa kuna kasoro za hapa na pale ambazo haziwezi kuathiri jamii yetu ya Kizanzibari. Ni utaratibu wa wawatowaji wa mikopo yenyewe.

Mhe. Spika, utaratibu wa mikopo ya AK na JK huwa inaanza vijijini, halafu inapitia kwa masheha. Kuna kamati zile za masheha ambazo ziko chini ya shehia ndizo zinazoratibu mikopo hii, baadae mikopo ile inapelekwa kwa Mkuu wa Wilaya. Baada ya kutoka kwa Mkuu wa Wilaya mikopo ile sasa inapelekwa moja kwa moja kunakohusika yaani benki.

Mhe. Spika, wizara yangu kwa kiasi fulani ilikuwa haijajiingiza moja kwa moja katika kulisimamia suala hili, kwa sababu maamuzi ya serikali ni kuwa mikopo hii itolewe na benki moja kwa moja. Hata hivyo, Mhe. Spika, wanaoomba wanaweza kuwa ni 50, wanaopata wanaweza kuwa ni 5, kwa sababu hawakidhi mahitaji ya kibenki.

Kwa mfano, unaweza ukaomba. Mikopo hii ilikuwa inatolewa kwa viwango tofauti, unaweza kuanza 50,000/= ikenda mpaka milioni 5 pia ni AK na JK. Lakini kama hukidhi vigezo vya kupata mkopo si rahisi kupewa. Kuna watu ambao waliomba mikopo na moja katika *condition* ya mikopo ile ni lazima uwe *base* ya kitu au mradi ambao unaufanya. Huwezi kwenda kuomba mkopo wa milioni 2 au milioni 3 ndio ukaanzie kitu chenyewe. Moja katika *condition* za benki ilikuwa kwanza uwe na *base.*

Mhe. Spika, kosa ambalo lilitendeka au pengine kupitikiwa kwa watendaji wakati huo, hawakuanza kutoa mafunzo ambayo yalikuwa ni muhimu sana na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako walihimiza sana kwamba wapatiwe mafunzo na elimu, ili waweze kujua utaratibu wa kupata mikopo hiyo.

Mhe. Spika, wizara yangu imejipanga sasa hivi na tumepadilisha utaratibu wa kupata mikopo hiyo. Sasa hivi ikipita kwa sheha, wilayani kisha inakuja wizarani kwetu, tuna ihakiki na kama ina matatizo, yule mwenye matatizo tunamwita tunamfahamisha, akisharekebisha tunampa fomu nyengine anaileta na tunahakikisha kwamba wote wanapata mikopo hiyo bila usumbufu wowote sasa hivi. Hilo tumejipanga wala lisiwe na mashaka yoyote.

Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe, walieleza *concern* zao kuwa mikopo hii inatolewa kimya kimya wao hawana habari. Waheshimiwa wengi walilalamika katika majimbo yao hawawajui waliopewa mikopo. Hizi karatasi ambazo Mhe. Spika, nimesema zikusanywe, ambapo nadhani umeletewa mezani kwako, inaonesha karibu wilaya zote, majimbo yote karibu yamepata mikopo hiyo. Mimi hapa ninayo kopi hiyo, mpaka mwezi Juni, 2011.

Mhe. Spika, katika Wilaya mbayo ilifaidika sana ni wilaya ya Mhe Subeit ya Micheweni. Baadae Mhe. Spika, nitakuomba muongozo wako utanisaidia. Majimbo mawili ambayo hayakupata mikopo hii ya AK na JK ni Jimbo la Magomeni na Jimbo la Makunduchi. Mwakilishi wa Jimbo la Makunduchi

anajua kama hakupata hayo. Lakini wizara safari hii itafanya juhudi ili na yeye tumuwezesha Mwakilishi wa Jimbo la Makunduchi kwa kupata mkopo huo wa AK na JK, pamoja na Mwakilishi wa Jimbo la Magomeni. Isipokuwa tumefaidika kama majimbo mengine yote yamefaidika kwa mifuko ya AK na JK, lakini pia ilifaidika na mfuko ule wa kujitegemea. Jimbo la Magomeni pia walifaidika katika mfuko ule wa kujitegemea kama vile Jimbo la Makunduchi walivyofaidika vile vile. Kwa hivyo, sisi tumefaidika kwa upande mmoja, lakini karibu majimbo yote wamefaidika.

Mhe. Spika, tatizo lililokuwepo ni kwamba wanaoomba wanaomba moja kwa moja kupitia kwa masheha, hatukutaka viongozi wa kisiasa wajiingize moja kwa moja kwa sababu ingeleta *interest*, tunawapiga debe wetu au tuna watu wetu huko, sio vibaya na msimu ukija ndio umekuja. Lakini sisi wizara tumesema ni vizuri inapofika kwa sheha, mwakilishi wa jimbo lile au mbunge wa jimbo lile, aarifiwe kwamba kuna maombi yameletwa na wananchi wanaomba mikopo ili ajuwe kwamba angalau katika jimbo lake wananchi wangapi wanaomba mikopo hiyo. Tunafanya hivyo makusudi ili wawakilishi na wabunge wajuwe.

Pia tujitahidini sana kufuatilia kwenye majimbo yetu kwa sababu inaelekea kwamba wananchi wanaomba mikopo wengi katika majimbo yetu na tunawapa, lakini sisi waheshimiwa hatuna habari, kwa sababu tunaona kwamba ama hawatopata au kwa sababu ya utaratibu uliokuwepo hamkushirikishwa. Sasa *Inshaallah* tutakushirikisheni kwa njia moja au nyengine, lakini tunaomba nia ya mikopo hii ni kuwasaidia wale ambao hawana uwezo. Wale wote ambao walipata mikopo ile, tunahakikisha kwamba ni watu ambao wana sifa hizo hakuna upendeleo.

Isipokuwa kumetokea malalamiko ya hapa na pale, kuna baadhi ya watu waliomba mikopo ile kwa kwenda kufanya mambo yao binafsi. Sasa mambo ya binafsi madamu huzalishi basi pesa huwezi kuzilipa hizo. Lakini kwa juhudi kubwa zilizofanywa na watendaji wa wizara, sasa hivi mikopo ile inarejeshwa na tunahakikisha kwamba wale wote waliopata kwa njia iwe kwa utaratibu ule walikuwa na *investment* walizianzisha au kwa njia ile ambayo walianzisha tu kwamba wapate kwanza halafu ndio wafanye, basi mikopo ile italiwa kwa utaratibu ambao tumeuweka na tunahakikisha kwamba tutafanikisha zoezi hilo.

Waheshimiwa Wawakilishi, tunawaombeni sana na wengi mmeniomba nifanye ziara majimboni. Nitapanga ratiba nitakwenda kwenye majimbo yote 50. Moja ambalo nawaombeni, kwa sababu wakati mwengine naweza nikawaarifu nakuja kwenye majimbo, lakini Waheshimiwa Wajumbe, hamuhudhurii mnakuwa na majukumu mengi. Kwa hivyo, nitaipanga ratiba kama utadharurika bora niahirishe, lakini tuhakikishe pale tutakapofanya ziara na

watendaji wangu basi na wewe uwepo ili ushuhudie yale tunayoyasema, halafu tuwahimize wananchi walipe mikopo ile tuweze kufanya hivyo.

Mhe. Spika, njia hii itatusaidia sana na wananchi wetu wako tayari, wajasiriamali mmewaona hapo nje na wengi wamekwenda kununua pale pamoja na mimi. Tena wanauza vitu vizuri, vya kujenga afya na mambo mengine.

Mhe. Spika, karatasi hizi ni siri. Nahofia isije yakatokea yale ambayo yametokea huko, mambo ya *hack* na mambo mengine. Hii ni siri kati ya benki na aliyekopa, hatuwezi kutoa siri hizi tukawapa wote, hasa kwa matumizi mengine. Lakini Waheshimiwa Wajumbe, nakala za *copy* hizi zitakuwepo kwa Mhe. Spika, nawaombeni yeyote yule ambaye atakuwa nayo, au Mhe. Spika, ataandaa utaratibu ambao mwenyewe atauona atatoa muongozo, kwa sababu haya ni mambo ya kati ya mteja na yule wa benki aliyekopesha, yaani aliyekopa na aliyekopeshwa ni siri za kibenki. Sio utaratibu mzuri kutoa siri hizi tukawapa kila watu, kwa sababu kuna hatari vikaja vikaingia kwenye vyombo vya habari na sehemu nyenginezo, halafu akaja akakamatwa waziri sasa ametoa siri za wateja wanaokopa na kukopa jamani ni unyonge, lakini ndio tunakopa, haifai kutoa siri.

Kwa hivyo, naomba Mhe. Spika, baadae kwa utaratibu wako na busara zako uje utupe muongozo namna gani, lakini tutaweka kumbukumbu hizi kwako wewe na yeyote ambaye atahitajia kuja kuona, naomba ende akacheki wajumbe wake na wananchi wake wangapi wamefaidika. Mji Mkongwe Mhe. Ismail Jussa wamefaidika, watu wa Micheweni wamefaidika, watu wa wilaya ya mjini na wilaya zote wamefaidika, nawahakikishieni kwamba mambo yamekwenda vizuri sana, lakini tunajipanga upya ili kuhakikisha sasa upeo wa kuweza kulifahamu jambo hili kwa uwazi zaidi kama alivyoniambia Mhe. Rashid Seif.

Mhe. Rashid Seif Suleiman, kanipa nguzo nne za uwazi ambazo ya kwanza ni katika masuala yetu haya ya utekelezaji wa kazi, hakuna cha kuficha Mhe. Spika, bajeti hii imewekwa ya uwazi na tutahakikisha kwamba hatufichi na pale ambapo pana taarifa za kutolewa basi tutazitowa hadharani. Lakini nawaombeni waheshimiwa tatizo lililokuwepo ni kwamba wananchi wenyewe wanapolalamika na masula ya kuwa hawapati mikopo, basi nawaombeni sana pale pale wanapowalalamikieni wapeni vikaratasi tu mpelekee Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wanachi Kiuchumi, mimi nitavipokea na nitavifanyia kazi. Tukingojea vikao kama hivi wakati mwengine itakuwa sio vizuri sana kwa sababu watakuja kulalamika kuwa waheshimiwa tupelekee ni malalamiko kumbe hakuna jambo zito la kulilalamikia jambo lile.

Mhe. Spika, katika watu 45 au 50 ambao alisema Mhe. Mjumbe mmoja hapa kwamba hawakupata 45, walipata watano. Wale 45 hawakukidhi zile sifa ndio wakapata watano. Lakini wamerudi wakapata mafunzo baadhi yao sasa hivi wameshaanza kupata. Mhe. Spika, kuhusu jambo hili la mikopo naomba tukubaliane kwamba tunajiandaa vizuri pamoja na wananchi wote na waheshimiwa wote watakuwa wanaelewa yale ambayo yanatendeka majimboni kwao. Yale majimbo mawili ya Magomeni na Makunduchi ambao hawajapata naomba wakae mkao wa kupata mkopo huo *Inshaallah.*

Tatizo lililojitokeza jengine Mhe. Spika, ni suala la ajira. Nakiri na nakubali kuwa wawekezaji wengi hasa wa mahoteli wamechukua wafanyakazi kutoka nje ya Zanzibar. Hilo sio jambo ambalo linapendeza na mimi mwenyewe linanikereketa na nimeanza kuchukua hatua. Kwa taarifa ya Waheshimiwa Wajumbe Mhe. Spika, tumeanza sasa kupokea barua kutoka mahotelini, wanatuletea barua kwamba tuna nafasi za kazi moja, mbili, tatu jambo ambalo miaka sita au saba nyuma halikutendeka. Tunafanya utaratibu sasa hivi katika sheria zetu au katika kanuni zetu tutarekebisha ili kuhakikisha kwamba tunawaambia kipaumbele kwanza ni wazalendo, halafu kama hakuna watu wenye sifa hizo basi watuletee sisi ili tusitangazie, kama hawaji wenyewe na kama hakujitokeza hapo tuta-*endow* kwamba sasa wanaweza kutafuta watu kutoka nje ya Zanzibar. Lakini kipaumbele ni lazima wapewe wazalendo. Ni kweli.

Mhe. Panya Ali Abdalla kalizungumzia hili pamoja na Mhe. Ismail Jussa na wajumbe wengine wamezungumza. Suala la kutandika kitanda, kufyagia, bustani. Lakini waheshimiwa wajumbe hata haya ya kutandika vitanda na bustani yanasomewa. Sasa kitakachotendeka ni nini, kama wanahitaji watu kama hao watuambie. Tunashukuru sana mashirikiano tunayopata kutoka Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo, chuo kile cha utalii tunashirikiana vizuri na wapo vijana wamepata mafunzo mazuri. Wakituletea sisi tunawapelekea na tunahakikisha wanapata fursa hizo. Hilo la kwanza.

La pili, kumekuwa na taarifa za ajira za Qatar. Mimi nilikwenda Qatar nashukuru, nilipata bahati na fursa ya kumuona Mfalme mwenyewe. Nilikuwa nimevaa tai hivi hivi. Mhe. Spika, moja katika kazi ambayo nimeifanya katika mazungumzo yale pamoja na kumpongeza Mfalme kwa kuandaa kombe la dunia mwaka 2020/22. nilimueleza maeneo mbali mbali ambayo tunayahitajia kupata msaada, akamtuma msaidizi wake maalum, akaja Zanzibar. Timu hiyo ni kwa kushirikiana na wenzetu wa Oman, kwa heshima nasema kazi hiyo imefanyika kwa uangalifu mkubwa na imeshirikisha wizara tatu, Wizara ya Afya, Mhe. Juma Duni namshukuru sana na nampongeza. Kwa sababu yeye mwenyewe kalisimamia jambo hili. Mhe Waziri wa Elimu na Mafunzo ya

Amali, Mhe. Ramadhan Abdallah Shaaban na Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika alikuwepo kwenye kikao hicho.

Mhe. Spika, tulizungumza na kwa bahati nzuri ujumbe huo ulikubata na Makamo wa kwanza wa Rais, Makamo wa Pili wa Rais na Rais mwenyewe walizungumza naye. Kwa hivyo, kule Qatar kuna taasisi inaitwa Qatar Foundation. Mama Moza mke wa Mfalme ndio mwenyekiti. Kwa hivyo, kuna kitu kama hicho ndio tunakizungumza kuanzisha Zanzibar, kinaitwa *Zanzibar Foundation* ambayo itakuwa inachukua maeneo kama hayo.

Pia suala zima lililozungumzwa ni uwezeshaji wa wananchi. Katika mkutano huo vile vile tulisema tunahitaji wafanyakazi na vijana waje hapa kuja kufanyakazi. Nililileta hapa tukalizungumza, nikaviarifu vyombo vinavyohusika. Kwa bahati nzuri nilipopata nafasi kwenye mkutano wa kazi duniani ILO Geneva. Suala hili najibu zile hoja zilizouliza kwamba ulipokwenda ulituletea faida gani, kwa wale walioiuliza majibu ndio yanakuja hapa hapa.

Mhe. Spika, nilipokwenda nilikutana na Waziri anayehusika na mambo ya *Social Welfare* ambaye ndio Waziri wa *Labor* wa Qatar. Akaniambia mimi na waziri mwenzangu wa Tanzania Bara, tunahitajia Zanzibar na Tanzania kwa jumla kuleta vijana waje kufanya kazi Qatar. Kwa hivyo, tumo kwenye *process* ya mawasilino kati yetu sisi na wao. Lakini sisi upande wa Zanzibar tunafanya yetu na Bara tunatarajia na wao watafanya kwa mujibu wa wanavyohisi wao inafaa.

Mhe. Spika, tunafanya mazungumzo na tunatarajia ku-*draft* MU, baadae tunapeleka serikalini na serikali ikisha-*endows* tunawapelekea kwa kupitia kwa Mwanasheria Mkuu tutawapelekea wenzetu wa Qatar waitizame, ikiwa muafaka basi hapo ndipo tutakapoanza utaratibu wa kuwatafuta vijana wa kuwapeleka huko. Wamesema ni kwa kazi zote bila kujali kiwango cha elimu cha yule kijana ambaye atakwenda huko. Hilo liliwekwa bayana na kule kweli wanahitajia wafanyakazi wengi. Lakini lile lililotangaziwa sio la Qatar, lililotangaziwa ni la Saudi Arabia.

Mhe. Spika, kuna taasisi yetu moja hapa ambayo tunafanya nao kazi na wizara inajua hivyo kwamba ndio waliotangaza. Sasa kuna Waheshimiwa Wajumbe fulani walisema hebu tueleze kuna pesa zinakusanywa. Maombi yaliyotumwa yote kwa Unguja ni 182, Pemba ni 200 na malipo yanakuwa hivi. Shs. 50,000 kwa ajili ya fomu, chanjo, *finger print* ambazo polisi wanatusaidia na mengineyo. Halafu dola 50 kwa ile taasisi ambayo inasimamia suala hili la ku *cordination* kati ya Zanzibar na Saudi Arabia. Hili ni jambo ambalo linatakikana kisheria kabisa yaani linafuata taratibu zote.

Mhe. Spika, hivi sasa ninavyosema wananchi wetu wa Zanzibar wako tayari, kuna madereva wamekwenda huko. Maana nimesema hata daraja za chini kabisa wamekwenda, baadhi ya ma-*nurse* wetu wamekwenda huko wanatoa huduma katika nyumba kubwa kubwa huko, kwa mshahara mzuri wanalipwa kwa mujibu wa makubaliano na mkataba. Jambo moja ambalo tunalifanya wizara yetu, tunaipitia mikataba yote ambayo iko nje na ya ndani ili kuhakikisha kwamba mikataba ile inawafanya wafanyakazi wetu na wananchi wetu wa Zanzibar, kwanza kutambua usalama wao, kutambua haki zao na fursa zao zote. Wawe na uwezo wa kukaa kule kufanya kazi kwa mwaka mmoja au miaka miwili na baadae wakaweza kurudi na kuendelea na shughuli zao kuja nyumbani na wakarudi tena. Tunajaribu kuiangalia mikataba hiyo. Sasa hivi tumeshaanza ku-*draft* mkataba kati ya Zanzibar na Oman ambayo tunaifanyia kazi, Zanzibar na UAE tunaufanyia kazi na Qatar tunaufanyia kazi na *Inshaallah* nchi nyengine zitakapojitokeza kufanya hivyo, basi tutafanya hivyo.

Mhe. Spika, hata Iran tulipata bahati vile vile ya kukutana na Waziri anayehusika na mambo ya *Labor* wa Iran, na yeye ameonesha *interest* ya kutaka kushirikiana na Zanzibar na kuona kwa kiasi gani wanaweza kuwachukua vijana kutoka Zanzibar wakenda kufanya kazi huko. Lakini jambo hili tunataka kulifanya kwa tahadhari kubwa sana, hatuwezi kuwachukuwa Wazanzibari tukawapeleka nje kwa kwenda kunyanyaswa hilo hatulikubali. Tunataka tuhakikishe taratibu zote tumezifuata, kanuni zote tumezitekeleza, tuwe na makubaliana na uhakika na usalama wa vijana wetu wanaokwenda kufanyakazi huko. Hilo wenzetu tumezungumza nao na wametuhakikishia kwamba halina matatizo yoyote. Kwa hivyo, naomba suala hilo la ajira za nje lieleweke hivyo.

Mhe. Spika, bado tunataka wawekezaji wanaowekeza Zanzibar wajuwe kwamba kipaumbele kwanza ni kwa wazalendo Wazanzibari wapewe nafasi hiyo. Lakini wakati mwengine tunalalamika hatupati ajira, yanakuja malalamiko, wanasema hao wenye mahoteli makubwa wakati mwengine wanasema kidogo tunakuwa wazito katika utekelezaji wa kazi. Sijui kama kuna kiji-*element* cha kutegea tegea au vipi.

Mhe. Spika, mimi nimepata bahati ya kusafiri kwenda Dubai. Pale Dubai kama unakwenda kujisaidia kwenye *lavatory* zile za *first class* au *business class*, kabla hujatoka huyo msafishaji yuko ndani anakufungulia mlango, ukitoka unaona keshaingia anakwenda kusafisha pale pale. Kwenye mahoteli unakwenda unapata huduma pale, ukishamaliza kula au pengine umemaliza lakini sahani ziko pale pale, basi sahani zile zinaondoshwa zinasafishwa zinawekwa nyengine pale pale. Sasa kuna hatari pengine sahani za asubuhi zikakutana na za mchana. Kwa hivyo, wenye mahoteli mambo kama yale hawayakubali.

Mimi nina imani kubwa kwamba Wazanzibari hawana tabia hizo na *Inshaallah* naomba wajitokeze, tusilalamike wajitokeza. Pale ambapo wameomba wamekosa fursa ile basi waje watuletee taarifa hizo na sisi tutazishughulikia kikamilifu tusiwe na wasi wasi wowote.

Mhe. Spika, tatizo jengine lililozungumzwa kwa urefu ni usalama wa kazi. Lakini hili hili liliongeze na ajira ya watoto. Suala la ajira za watoto wizara yetu inahusika na Wizara ya Wanawake na Watoto inahusika. Kumewekwa vigezo maalum vya watoto kuwapa kazi. Tusione kupara samaki kwamba tunamzalilisha mtoto, zile ni kazi ambazo tunahitaji kuwafundisha watoto wetu kujua kupara samaki, kuuza mandazi na biashara nyengine za nyumbani. Kazi zile sio kumdhalilisha mtoto ni kazi za kusaidia hutuma za nyumbani.

Mhe. Spika, linalokatazwa hapa ni kwamba unawachukua watoto watano, sita au saba hawendi skuli unawapeleka pwani kwenda kufanya kazi kama zile au unawapeleka katika maeneo ya kubanja kokoto wanakwenda kupasua kokoto zile, suala hili halikubaliki na ni kinyume na utaratibu wa haki za binadamu na haki za mtoto. Mtoto apate fursa ya kusoma, huduma za afya na huduma zote muhimu. Tunatoa wito kwa wale wote ambao wanawatumia watoto kwa njia hizo, basi waache mara moja kwa sababu hilo halitasaidia na wanaweza wakashtakiwa kwa mujibu wa sheria zetu tulizokuwanazo.

Mhe. Spika, mtoto yeyote ambaye ana umri wa miaka kuanzia 6 na kuendelea, anawajibu wa kupelekwa skuli na kwa mujibu wa sera mpya ya elimu sasa hivi elimu ya lazima inaanza ya maandalizi akiwa na umri wa miaka 3, 4 au 5 na mwaka wa 6 anaingia *primary*. Kama hakuwahi kubahatika kwenda *nursery school*, basi anaanza *standard one* akiwa na umri wa miaka 7 au 6 wakati mwengine. Wako watoto ambao wako nje ya skuli na wameshafika umri huo, ndio maana yake wizara ikaanzisha utaratibu wa elimu mbadala. Miaka 13 pengine mpaka miaka 20 wakarejeshwa tena kwenye vituo vile. Tunamshukuru Mwenyezi Mungu vituo vile vimeendelea vizuri na vinatoa vijana wazuri. Vijana wale wamemaliza na wengine wako sekondari sasa hivi wanaendelea vizuri.

Mhe. Spika, kuhusu suala la usalama wa afya. Suala hili nataka tulisikilize kwa makini, kwa sababu linatugusa sote tuliokuwemo humu ndani. Afya ya wafanyakazi na usalama wao ni muhimu sana. Sisi mawizarani kuna wafanyakazi wetu wale matarishi, wanaosafisha kwenye maeneo mbali mbali, basi tunahitajia kuwapa vifaa vya kuwakinga. Naomba Mhe. Spika, kwa kupitia kwako kutoa wito kwa waheshimiwa wote waliokuwa na wafanyakazi nyumbani, waliokuwa na wafanyakazi maofisini na wengineo, basi tuhakikishe tunawapatia vifaa vya kinga wale vijana wanaofanyakazi za usafi. Kwa mfano,

bustani wapatiwe *gloves*, viatu vya *rain boots, overall* kwa ajili ya shughuli za pale na sio tena anatembelea mitaani.

Vile vile kama wafanyakazi wa *washroom* basi wapatiwe vifaa kama vile *glows*, viatu vya sio vya kanda mbili vile wanavyovaa kwenye mswala na halafu anatoka navyo na kuingia ofisini kwako, yaani kuwe na vifaa maalum vinawekwa kule.

Kwa hivyo, hayo ni majukumu yetu sote tuhakikishe kwamba tunatekeleza, tusipofanya hivyo tunakwenda kinyume na utaratibu wa Sheria moja ya *ILO* kuwapatia Haki, Fursa na Kazi za Staha wafanyakazi wetu. Kwa maana hiyo, tujitahidi na nitaanza kule wizarani kwangu kurekebisha kama bado na halafu nikimaliza sasa nitakutangazieni kwamba sasa naanza kufanya ziara ya kutembelea maofisini kwa ajili ya kuona kazi hiyo, kwa sababu kazi hiyo iko kwenye wizara yetu ni vyema tujitahidi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, tatizo jengine ambalo limejitokeza kwanza kuna kitu hiki tunachokiita kazi za staha na heshima. Kwa kweli kazi yoyote ile ambayo ni halali inayokupatia riziki ni kazi ya staha na heshima, kwa hiyo tusimdharau mtu kwamba anafyagia au anapeleka barua tukaona ile ni kama kazi ya kutumwa tumwa tu, ile ni kazi safi ya heshima na staha tena anapata haki yake kwa mujibu wa utaratibu ulivyo.

Sasa tusione kwamba wale wako *level* ya chini basi tukaona kuwa hawa si wafanyakazi ambao tunaweza kuwapatia fursa fulani (a), (b), (c) na (d), kwa kweli wale wanastahiki kupatiwa fursa zote.

Masuala haya yamegusia sana wizara yetu pamoja na Wizara ya Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Kwa mfano, kuna Mhe. Mjumbe mmoja aliuliza nani anayehusika na mambo haya sasa ya kupanga kazi na ajira utumishi wa umma.

Kwa kweli Sheria ile ya Utumishi wa Umma imeeleza na kipengele hicho kwamba watahusika katika masuala mazima ya ajira. Vile vile kwenye Sheria yetu ya Kazi pia inasema suala la ajira linasimamiwa na wizara yetu, kwa hiyo hapa kuna muingiliano wa kisheria.

Kwa hivyo, itabidi serikali tukae na wizara inayohusika na utumishi kwa ajili ya kuli-*sort-out*, ili tujue taasisi gani ndio itakayokuwa ina-*regulate* na nani ambao watakuwa wanatekeleza majukumu yale na hili tutaliangalia ni kweli tumegundua kuna mgongano huo na tutalifanyiakazi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe pia walizungumzia suala la *Vocational Training* na wengine wakasema kwamba lirejeshwe huku na wengine wakasema likirejeshwa huku itakuja kujulikana hivi vituo vya Mwalimu Haroun Ali Suleiman. Kwa hiyo, alipokuwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, hivi vilikuwa Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wawanake na Watoto akavirejesha huku na sasa kenda kule anataka kuvichukua kule.

Suala hilo sijasema na wala kwenye hotuba yangu halimo, isipokuwa Waheshimiwa Wajumbwa walipendekeza kwamba kwa sababu Vituo vya Kazi za Amali vinazalisha ajira, basi ni vizuri viwemo katika wizara inayohusika na ajira na nchi nyingi duniani zimefanya hivyo, lakini ni mgawanyo wa kazi.

Kwa mfano, *ZSSF* ile ni michango inayotolewa na wafanyakazi ni haki yao, kwa hivyo baadhi ya nchi duniani hata katika Mkutano wa *Geneva* tuliokwenda tumegundua kwamba nchi nyingi mifuko ile iko kwenye wizara inayohusiana na masuala ya ajira. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Tanzania Bara *NSSF* inashughulikiwa na Wizara ya Kazi, lakini kwa utaratibu wetu tunaelewana na wala hakuna tatizo hilo na sisi tuko tayari kushirikiana na wenzetu wa *ZSSF* kupitia Wizara ya Fedha, Wizara ya Wanawake na Watoto kuhusu suala la vijana na watoto wadogo. Vile vile pamoja na wizara nyengine kama vile ya Elimu na Mafunzo ya Amali katika masuala ya *Vocational Training* hakuna matatizo kubakia huko ziliko na sisi tutaendelea kushirikiana nao kwa kujenga umoja wetu. *(Makofi)*

Nataka nitoe ufafanuzi kidogo Mhe. Spika, kuna Mhe. Mjumbe mmoja alisema sasa Mfuko mmoja upo wa JK, lakini wa AK haupo, yaani kama kueleza kwamba ule mfuko haupo. Mhe. Spika, AK alitupa *capital* sisi ya shilingi milioni 600, fedha zile zinaendelea kuwepo kwa sababu zilitakuwa zikopeshwe wananchi na baadaye zirejeshwe ili wakopeshwe wengine. *(Makofi)*

Kwa hivyo, AK bado yupo na kinachofanyika hivi sasa Dkt. Ali Mohammed Shein ameshatanga kwamba ataanzisha Mfuko wake wa AS. Kwa maana hiyo, kutakuwa na mifuko mitatu, yaani JK, AK na AS na wala tusiwe na mashaka mifuko yote hiyo itafanyakazi vizuri na tutafaidika sote Waheshimiwa pamoja na wananchi wetu katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, suala la *ZANTEL* na Mhe. Ismail Jussa Ladhu alilizungumza sana. Kwa kweli suala hili ni zito na linahitaji busara na ninamuomba sana Mhe. Mjumbe bado aipe nafasi wizara yangu hii mpya tuendelee kuyafuatilia, kwa sababu tumeshaona mwanga wa kuona wapi tutafika.

Tatizo lililojitokeza kwamba walibadilisha taratibu zao *ZANTEL* na kuweka mfumo wao, sasa kuna kada hizi nyengine kama vile za walinzi na wengineo hawakubahatika kufaidika na utaratibu ule, ingawa wengine wafanyakazi wenzetu walifaidika na kupata *promotion*.

Lakini kuna haki zao kwa sababu hawa wengine kwa mujibu wa mfumo mpya wanapata fursa pamoja na *privileges* zote wanazipata, sasa hawa ambao huko nyuma hawakuzipata na katika mfumo huu mpya hawafaidiki nazo.

Suala hilo tunalifanyikazi Mhe. Spika namhakikishia Mhe. Mjumbe kwamba tutahakikisha kuwa tunazungumza na *ZANTEL*. Kwa hivyo, leo hii nimetoa agizo kwamba huyu mkubwa wa *ZANTEL* niitiwe kwa ajili ya kuzungumza naye ili nimpe kadhia hii kuwa aitekeleze na achukulie hatua haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hatuwezi sisi kama Wizara yetu ya Kazi basi hatuwezi hata mara moja kuona kwamba mwananchi wa Zanzibar ananyimwa haki na fursa yake. Kwa kweli mimi ni mtu ambaye ninatoka kijijini tena naona fahari mukiniita Mshamba, kwa hiyo ninajua tabu wanazopata wananchi kijijini, kwa sababu nimezaliwa huko pamoja na Mhe. Ismail Jussa Ladhu na yeye anakujua. *(Makofi)*

Kwa hivyo, wale Waheshimiwa Wajumbe waliosema kwamba tufikie sana vijijini, basi mimi nitakuwa wa mwanzo kuwafikia watu wa vijijini. Lakini katika utendaji wa kazi tunaangalia kwa upeo wa taifa, kwa maana hiyo tunaiangalia Zanzibar kama Zanzibar popote pale walipo wanapostahiki kupata haki yao basi watapata. Mhe. Spika, wafanyakazi hawa wa *ZANTEL* tunawahakikishia kwamba tutafanya kila tunaloweza kwa ajili ya kuwapatia haki zao. *(Makofi)*

Sasa wale ambao wanaadhibiwa wanapata matatizo hotelini. Mhe. Spika, tatizo lililokuwepo hawaji kuripoti pale wizarani, kwa sababu hawa wote wanalalamika ama nje au kupitia kwa Waheshimiwa. Kwa hivyo, nadhani ni vizuri malalamiko yao wasiogope, kwa sababu pale wizarani kuna Kitengo Maalum ambacho kazi yake ni kusikiliza matatizo ya wafanyakazi kama hao na wala wasiwe na mashaka tutawafuatilia na tumeshafuatilia kesi nyingi sana.

Kwa mfano, hivi karibuni kulikuwa na tatizo la Amani pale kwenye maeneo yaliyokuwa Viwanda Vidogo Vidogo, kuna mwekezaji alikuwa hawalipi haki zao wafanyakazi kutoka Ethiopia na wengine kutoka hapa nchini. Kutokana na hali hiyo, tumemwita na amechukua hatua ya kuwalipa haki zao zote na hivi sasa wanaendelea na kazi bila ya usumbufu wowote.

Mhe. Spika, natoa wito kwa Waheshimiwa kwamba waje watueleze na sisi tutajitahidi kutekeleza na kuwapatia kila ambacho wanastahiki kupata. *(Makofi)*

Nikiendelea na majumuisho sasa nizungumzie kuhusu Vyama vya Ushirika. Mhe. Spika, suala hili kuna Waheshimiwa Wajumbe waliosema kwamba vimekufa na vyengine vigonjwa na vyengine havijui vinakwenda vipi. Kwa kweli vilivyokufa tutavifufua, vilivyokuwa vigonjwa tutavipatia dawa na vipya tutavianzisha. *(Makofi)*

Suala la msingi tukubali kwamba watu walianzisha Vyama vya ushirika wakati ule, wengine walianzisha *just* kwa sababu wanataka kuanzisha Vyama vya Ushirika na wala hawakuwa na maandalizi ya kutosha. Mhe. Spika, hivi sasa utaratibu ambao tumejipangia kwa bahati nzuri Waheshimiwa Wajumbe Sera ya Vyama ya Ushirika tayari, Sheria ya Vyama vya Ushirika pia nayo tayari na karibu tutaipeleka kwenye vyombo vinavyohusika kwa ajili ya kupitishwa na hivi sasa tunaandaa Kanuni. *(Makofi)*

Kwa hivyo, katika kipindi cha miezi mitatu ijayo na tunatarajia katika kikao cha Baraza, basi Inshaallah tunaweza kuileta hapa sheria hiyo baada ya kuipeleka serikani, kwa ajili ya kuipitisha na kuweka taratibu za kuvijengea uwezo Vyama vya Ushirika.

Kwa kweli tunashukuru sana Wizara ya Kilimo na Mifugo kupitia Shirika la *IFAD*, hivi karibuni wamekuja wizarani pale na tumefanyanao kazi na wako tayari kujenga uwezo kwa Vyama vya Ushirika kwa kutoa mafunzo mbali mbali pamoja na kuwawezesha wananchi wetu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, wengi walizungumzia suala la maana hii ya uwezeshaji. Kwa mfano, kuna Mheshimiwa Mjumbe mmoja alisema anataka kufahamu hasa maana ya uwezeshaji, kwa bahati kwenye Kiambatisho Nam. 1 kwenye *budget speech* yetu tumeweka maana ile. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Mjumbe atumie muda kidogo kuangalia yale ambayo yameelezwa kule.

Suala jengine walieleza *concern* kwamba kuna tatizo la kupata *Passport* kwa wale wanaotaka kwenda nje inachukuwa muda mrefu. Kwa hivyo, masuala ya *Passport* yana utaratibu wake pamoja na njia zake. Kwa mfano, hata mimi ninapotaka *Passport* kama Waziri basi lazima taratibu zile nizifuate, yaani niende kule nikaweke *finger print* zangu, vielelezo vyangu kwa ajili ya kuangaliwa, yaani inaweza kuchukua wiki moja au pengine siku 10, ingawa nashukuru sijachukua muda huo lakini inawezekana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, inawezekana pengine taratibu hizi za kupata *Passport* hazikufuatwa na watu wa Uhamiaji nashukuru sana ni watu wenye

mashirikiano makubwa, kwa sababu *Passport* kwa mwananchi yeyote ni haki yake almuradi uwe umetimia ule umri wa kupata *Passport* hiyo. Kwa hivyo, nadhani hivi sasa hata watoto wadogo wanazo *Passport* zao. Kwa hiyo, halina matatizo isipokuwa ni taratibu.

Vile vile wengine wamezungumzia suala la kuchukua muda katika usajili wa Vyama vya Ushirika. Mhe. Spika, ni kweli lakini lazima tuvihakiki, kwa sababu huwezi kuja pale ofisini na kusema tukisajili Vyama chake cha Ushirika kama sisi hatujenda kule tukakiona hicho chama chenyewe kama kipo. Kwa hivyo, hilo tukubaliane kwamba tutakwenda pamoja tutashirikiana, ili kuhakikisha tunafanya vizuri.

Mhe. Spika, pia kuna Mhe. Mjumbe mmoja aliuliza mbona *capital*, yaani fedha za maendeleo ni shilingi milioni 90/=, lakini kwenye *other charges* pamoja na matumizi mengine kuna fedha nyingi, kwa sababu huku imejumuisha mishahara pamoja na mambo mengine lazima kuwe na fedha nyingi.

Kwa kweli hizi shilingi milioni 90/= utaziona kidogo lakini si kidogo kwa sababu tumegawana keki ambayo tuliyonayo serikalini na mimi nimepata hizi na *Inshaallah* mwakani tutajiandaa kupata keki kubwa zaidi, ili tuweze kuwawezesha wananchi wetu kwa nguvu zaidi. *(Makofi)*

Pamoja na hilo Mhe. Ismail Jussa Ladhu aliuliza suala la Idara ya Mikopo kuwa imepatiwa ruzuku. Mhe. Spika, ni kweli imepatiwa ruzuku na ni ombi maalum ambalo tulipeleka Wizara ya Fedha kuwa wapatiwe ruzuku kwa sababu maalum, kwani hii ni idara inahitaji kufuatilia mambo mengine na wala hawana fedha kama ni idara moja kwa moja. Hivyo, wamepewa ruzuku hii kwa kukubaliwa serikalini pamoja na kukidhi mahitaji ya mishahara pamoja na mambo mengine kama hayo.

Kwa hivyo, naomba tukubaliane kwamba ruzuku ile ilikuwa ni maalum na wala si kawaida kweli kwa idara kupewa ruzuku. Lakini tuliomba na serikali ilidhinisha kwamba tupatiwe ruzuku hiyo.

Mhe. Spika, watu wameeleza kuna *SACCOS* na Vyama vya Ushirika tofauti yake nini. Kwa kweli ni kubadilisha majina tu, lakini mambo ni yale yale. Kwa mfano, tunabadilisha majina kama vile mama kumwita bimkubwa na baba kumwita bwana mkubwa ndio yule yule.

Sasa pengine kuna njia una-*justify* wewe labda tukiita *SACCOS* inakuwa na nguvu ya mvuto unaweza kufaidika na kupata mambo mengine zaidi, lakini ni kile kile ambacho kimekusudiwa. Kwa hiyo, hakuna tofauti kubwa sana juu ya jambo hilo.

Kwa mfano, kuna WEZA, JEKA, wengine wanaita VIKOBA. Kwa hivyo, hizi *SACCOS* au Vyama vya Ushirika vyote lazima vimekuwa-*registered* na WEZA, JEKA na VIKOBA havina ulazima wa kuwa *registered*, lakini kama watapenda kuwa *registered* basi wanaweza kupata fursa hiyo. Sasa kwa upande wa Vyama vya Ushirika na *SACCOS* lazima viwe na *registration* ya kutosha.

Mhe. Spika, kuna Mhe. Mjumbe mmoja alizungumzia suala la kwamba wafanyakazi wapimwe afya zao. Kwa mfano, zamani kulikuwa na utaratibu kabla ya kupata ajira serikali unakwenda kufanya *Medical Examination*, lakini kama vile mimi nilikwenda *Medical Examination* mwaka 1973 mpaka leo sijenda na hii ni hatari, kwa sababu naona napata pumzi naishi vizuri, lakini kuna hatari ndani yake.

Kwa hivyo, ni vizuri kuwe na utaratibu kwa waajiri wote wa Sekta za Umma na Sekta Binafsi tuhakikishe wafanyakazi wetu wanapatiwa huduma zile. Kwa kweli ni vizuri, kwa sababu pengine umemuweka mahala kuna mavumbi.

Kwa mfano, Mhe. Mjumbe mmoja amezungumza kama vile walimu wapatiwe vifaa vya hifadhi ya afya zao. Lakini mwalimu ukimvalisha kitu mdomoni kwamba asipate unga wa chaki na yule mwanafunzi hamuoni vile anavyotamka yale maneno mdomoni, kwa sababu ukisema *blackboard* mwanafunzi akuone jinsi gani unavyoitamka, yaani auone ule mdomo wako, sasa uko ndani unasema kwa ndani hakuoni, basi na yeye atatamka hivyo hivyo, ukisema *pen* aone vile unavyotamka, ukisema *table* aone.

Sasa tunamfikiri mwalimu kwamba anaathirika, lakini mule ndani kuna wanafunzi 40 au 50 na wao pia wanaathirika. Kwa kweli chaki ndio chaki na wengine ndizo zilizotufikisha hapa wengine. Kwa hiyo, tutaliangalia kwa njia gani tushirikiane, ili kuona kwamba chaki zinazoletwa zina *quality* ambazo hazina mavumbi, kwa sababu na hilo ni jambo jengine vile vile.

Kuhusu suala la kupima afya za wafanyakazi na ninamuomba sana Mhe. Waziri anayehusika na Mambo ya Utumishi wa Umma na Waziri wa Afya tushirikiane kwa pamoja, ili wafanyakazi wetu wote waliomo maofisini tuhakikishe tunapima afya zao kwa ajili ya kuona kwamba pale wanapofanyakazi, kwa sababu unaweza kumpeleka mtu pahala kumbe vile ile *Air Condition* inamdhuru na yeye anakaa kwenye *Air Condition*. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kuhusu ziara za nje waziri tuambie umekwenda nje umetuletea faida gani. Ziara ya kwanza niliyokwenda nje Mhe. Spika, nilikwenda Burundi kwenye Kikao cha Afrika ya Mashariki na kulizungumzwa suala zima la masuala ya ajira au Soko la Ajira la Afrika ya Mashariki. Kwa hiyo, tumerudi na tumelieleza na tumefahamisha na wafanyakazi wetu wanalielewa na

wananchi wote wanatakiwa kuelewa haki na fursa za kazi katika Soko la Afrika ya Mashariki.

Mhe Spika, Mkurugenzi wangu hivi sasa anafanya utaratibu maalum wa kuandaa *programs* za kuweza kutoa taaluma je wananchi wa Zanzibar watafaidika vipi katika Soko la hili la Ajira katika Afrika Mashariki. Hivyo, ni vyema na sisi tukajiandaa vizuri hivi sasa kwa sababu soko lipo, lakini kwanza tujitosheleze na soko letu wenyewe humu ndani, kwani tunalalamika kwamba maeneo ya hoteli wameajiriwa watu ambao si Wazanzibari.

Kwa hivyo, tujitahidi na wasomi walio-*graduate* kwenye Vyuo Vikuu wapo. Kwa mfano, waliosomea Sheria, *Business Administration* pamoja na wengine wapo, kwa maana hiyo tuhakikishe tunawa-*observe* vizuri. Lakini pia tusione tabu kuomba nafasi hizi katika Soko hili la Afrika ya Mashariki fursa zipo.

Mhe. Spika, nilipotoka Burundi safari iliyofuata nilikwenda Geneva na tayari nimeshaeleza faida ambazo tumezipata.

Vile vile nilipata nafasi ya kuvuatana na Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais na kwenda Oman. Mhe. Spika, nashukuru matunda ya ziara ya Oman yanaonekana. Kwa mfano, kuna Kikundi cha Utamaduni kipo hapa Zanzibar kinaendelea na shughuli zake mbali mbali. *(Makofi)*

Wakati nilipokuwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali ambaye nilikuwa nikihusika na mambo ya kale nilisaini makubaliano hayo kati ya Oman na Zanzibar, ambapo leo nafarajika kwamba watunda yake tunayaona. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ziara ile ya Makamu wa Kwanza wa Rais imejenga mahusiano mazuri zaidi kati ya Oman na Zanzibar na *Inshaallah* tunamuomba Mwenyezi Mungu ingawa leo na kesho hatuwezi kuona *product* ile, lakini matokeo ya maendeleo ya ziara zile yataonekana baadaye. Kwa kweli *achievement* ya mwanadamu siku zote huwezi kuiona kwenye kioo, yaani kwenda kujitizama na kujiona, kwa sababu zinakuja *on process*. Kwa hiyo, kidogo kidogo mpaka tutafika mahala ambapo tunaona.

Vile vile nilibahati kwenda Equatorial Guinea na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wa *AU*, kule yalizungumzwa masuala ya *empowerment* ya vijana na ndio hayo ambayo tuyaratibu hivi sasa.

Kwa mfano, tumeanzisha kile Kituo cha Kutoa Taarifa mbali mbali za Kupata Kazi, pia tunaanda utaratibu hivi sasa wa kufanyakazi na Masheha katika shehia tofauti, ili tuweze kushirikiana nao kujua vijana gani wapo waliomaliza skuli ambao wanahitaji kuingizwa kwenye Soko hili la Ajira, ili tuweze

kufanyakazi kwa kushirikiana na pale zinapopatikana fursa za ajira basi tutumie huduma hizo.

Mhe. Spika, ziara niliyokwenda ya mwisho ilikuwa ni binafsi nilikwenda Uingereza mtoto alikuwa ana-*graduate* na kijana huyo atakuja kufanyakazi Zanzibar, kwa hivyo hii ni faida nyengine pia. *(Makofi)*

Kwa hivyo, tumejitahidi na wale waliokuja kuonana na sisi Mhe. Spika, tumefanyakazi nao kwa mashirikiano na tunakwenda vizuri. Kwa mfano, *ILO* nimekuwa nikisema kila wakati wametusaidia sana, Marekani wanaendelea kushirikiana na sisi vizuri pamoja na taasisi nyengine pia kama vile India, China, Oman tumeanza kushirikiana nao vizuri na tutaendelea kushirikiana nao. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, nawaahidi kwamba safari zote ambazo zitafanywa na bahati nzuri sikufanya ziara hiyo peke yangu waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Kamishna wangu pamoja na Wakurugenzi wamesafiri nje ya nchi. Sasa leo nimewahakikishia kuwa kila pale ambapo kuna fursa ya kwenda kujifunza na kuona basi serikali itajitahidi na tutashirikiana, ili kuhakikisha wanapata fursa hizo kwa ajili ya kwenda kuona mengi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nilipokuwa Waziri wa Elimu namshukuru Mwenyezi Mungu karibu Wakurugenzi wote walipata nafasi na fursa za kwenda kujifunza Marekani na nchi nyengine na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi wakaa mkao wa kwenda kusoma na wala hakuna wasi wasi wowote. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nimekubali wazo hili la kwamba Vikundi hivi vya *SACCOS* na Ushirika viwe na utaratibu wa kubadilishana. Kwa mfano, kikundi ambacho kimefanya vizuri basi kiende sehemu nyengine, yaani kufanya ziara na kuweza kuwafundisha wenzao na wale ambao hawajafanya vizuri basi waende wakajifunze kwengine.

Kwa kweli hilo ni jambo zuri na ninaomba liendelee. Lakini hili ni mipango ya Mhe. Mwakilishi mwenyewe katika jimbo kwa kushirikiana na Mhe. Mwakilishi mwenzake na kuandaa utaratibu wa kutembeleana. Kwa hivyo, ni vyema kuanzisha urafiki sisi wenyewe na utaweza kudumu vizuri zaidi na tutafika mahala pazuri na ikifika siku za uchaguzi unasaidiana vizuri. *(Makofi)*

Mhe. Spika, wizara hii ni *crosscutting* kwa lugha ya hivi sasa ni mtambuka na wala huwa siyapendi maneno haya, lakini wakati mwengine inabidi niyatumie. Wizara ya Kilimo na Maliasili wakulima wale wanaolima kilimo wanataka

kuwezesha na Waziri wa Kilimo na Maliasili pake yake hawezi anahitaji na mimi niwa-*empower* watu wake, ili waweze kujitegemea. *(Makofi)*

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, kwa hiyo wavuvi wanataka vyavu, boti pamoja na vifaa vyengine mbali mbali na kuna Mhe. Mjumbe mmoja amependekeza tutoe meli kwa kila jimbo, sasa meli hizo tutatoa ngapi. Mhe. Spika, nadhani tutakachokifanya ni kukaa na wenzetu Wizara inayohusika na Mifugo na Uvuvi kwa ajili ya kushirikiana nao. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Wizara ya Afya tunahitaji kuwa na wafanyakazi wenye afya nzuri, pia Wizara ya Elimu kwa ajili ya kutoa elimu. Kwa kweli wizara hii imegusa karibu wizara zote tulizonazo katika Serikali yetu hii ya Mapinduzi. Kwa hivyo, ninachowahakikishia ni kwamba tutashirikiana na ninaomba watupe mashirikiano, kama nilivyosema wakati nilipokuwa nikijibu maswali kuwa kuna mambo ambayo yatahitaji tufanyekazi kwa pamoja na tushirikiane kama tutahitaji msaada wao basi tutapata msaada huo.

Mhe. Spika, nachukua nafasi hii kumshukuru sana Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili pamoja na Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi tumekuwa tukishirikiana vizuri hasa kupitia mashirika yale ambayo yanasaidia kilimo kupitia *IFAD*.

Mhe. Spika, napenda niwahakikishi Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu wote kwamba nimejipanga vizuri na watendaji wangu. Mhe. Spika, namahani natumia Lugha ya Kiingereza ndipo tutakapopata *taste* yenyewe *It is not a proper to down early conclusion, let us wait and we will see*, ndio kwanza miezi minane nimepewa. *(Makofi)*

Kwa hivyo, kama leo umevaa viatu vya raba, basi naomba baada ya mwaka mmoja watafute vyenye njumu waje wanigongee, lakini leo wawe *soft* kidogo kwa sababu sina nia ya kuyadharau yote ambayo walinieleza. Mhe. Spika, nia yangu ni kuwatumikia wananchi wa Zanzibar wakiwemo wao Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nadhani kwa ujumla nimezungumza hayo na wala sitaki nichukue muda wako, kwa sababu kila nitakapozungumza sana itakuwa nina-*create* mambo mengine.

Lakini napenda nimhakishie Mhe. Rashid Seif Suleiman ambaye amenieleze mambo manne. Kwanza kuwe na uwazi, miradi ile ambayo inayotayarisha inakamilika na iwe inagaiwa kwa uwiano ya Unguja na Pemba na nne kuangalia maeneo yenye *hardship areas*, yaani maeneo magumu. Kwa kweli Mhe. Mjumbe nimeyakubali yote haya. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nimempa nafasi hii maalum Mhe. Rashid Seif Suleiman kwamba *pillars* zake nne, kwa sababu alisema mwaka huu sina maneno namuachia kama hakutekeleza haya baada ya mwaka mmoja kama alivyokuwa ananifanyia Wizara ya Elimu basi na huku ataendelea kunifanyia hivyo hivyo. *(Makofi)*

Kwa kweli napenda niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe kwamba halitotokezea hilo na tutafanya kila tunaloliweza kuhakikisha kuwa tunashirikiana na Waheshimiwa Wajumbe wetu wote. *(Makofi)*

Kwa hivyo, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wote kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba waipitishe na kuikubali bajeti hii na Inshaallah tutafika pazuri. Ahsanteni sana.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwahoji wale wanaokubalia na hoja hii ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza limejadili na kuikubali Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika. Sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi, ili kuvipitisha vifungu vya matumizi vya wizara yangu.

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU – 27 WIZARA YA KAZI, UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI NA USHIRIKA

Kifungu 0801	Kamisheni ya Kazi	60,000,000/=
Kifungu 1001	Idara ya Ushirika	8,500,000/=
Jumla ya Fungu		**68,500,000/=**

Kifungu 0301	Afisi Kuu Pemba	117,126,000/=
Kifungu 0401	Idara ya Mipango, Sera na Utafiti	

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri na fasaha katika nukta nyingi tulizozieleza. Lakini katika mchango wangu kuna suala moja nililizungumza kwa urefu kidogo na kwenye majumuisho yake sikulisikia, sasa naomba anipatie maelezo ili tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti, suala lenyewe linahusu Ajira *Quota* ya Zanzibar katika Taasisi za Muungano, nilitaja kwamba tuna *quota* nyingi ambazo tulikuwa tuzipate lakini hatuzipati mfano wa Jeshi, Polisi katika mambo ya nje nikataka kujua nini *roll* ya Wizara ya Kazi Uwezeshaji wananchi Kiuchumi na Ushirika katika kusimamia kuona kwamba nafasi hizi za ajira kwa upande wa Zanzibar zinapatikana, naomba maelezo kuhusu hilo.

La pili naomba nimalize kabisa katika fungu la sera nilihoji kuhusu ziara ya Kaka na nashukuru maelezo mazuri aliyotoa Mhe. Waziri nafasi za ajira, lakini kataja mfuko wa Qatar *Foundation* akasema ni moja inayoshughulikia masuala haya ni Mke wa Mfalme Bi Moza, nataka niwaambie tu kwamba Bi Moza alikutana nae Mhe. Haroun katika ziara yake ?

Mhe. Waziri wa Kazi Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Suala la kwanza namuomba nimjibu masuala yale hayako kwenye wizara yangu ni masuala ya muungano, ndio maana sikuyagusa hata kwenye bajeti yangu sikuyazungumza, ni masuala ambayo yanashughulikiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ajira zile haziko kwangu kwa hivyo halihusiani jambo lolote katika wizara yangu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba bora tuendelee kwa sababu yule ni Mke wa Mfalme na kwa kweli nilikutana nae hapa Zanzibar pamoja na Mumewe walipokuja kwenye mapumziko yao, lakini pia yeye ndio Mwenyekiti na nilipokwenda kwenye Mkutano wa *World International Education. Coram* uliofanyika kule nilikutana nae kama Mwenyekiti, kwa sababu mwaliko ule niliotoka nao walinialika wao kwa hivyo nimekwenda, lakini masuala hayo yote yanayohusiana na *project* ya Zanzibar yeye mwenyewe alitaka kutusaidia katika maeneo fulani ya *project* na alikwenda kumuona Mhe. Rais Karume alipokuwa Ikulu pale na baadae akamwambia basi maelezo haya nitayaelekeza kwa Waziri anayehusika na elimu kwa wakati ule na wakati ule ndo nilikuwa mimi.

Sasa nimekutana nae na ndio miongoni mwa hayo sasa hivi mnaona yanafanyika ya masuala ya Wizara ya Elimu na Wizara ya Afya ambayo wanatarajia wataleta matunda mazuri sana tukijaaliwa.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti tuendelee ahsante sana.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti nakushukuru sana mimi nilipochangia nilimweleza Mheshimiwa kwamba kutokana na kuwakuza wajasiria mali wetu na kuna baadhi ya vikundi na wafanya biashara wadogo wadogo na wengine, nilimtaka Mheshimiwa kwamba huwezi kufanya kitu chochote bila ya kuwa na elimu nacho. Kwa hivyo nilimtaka waziri kuwapatia elimu wale watu wetu ili wajue wanachokifanya ni kitu gani na itakuwa ni kukuza zaidi katika kuleta mabadiliko ya kiuchumi katika nchi yetu na kuwakomboa wananchi katika kupunguza huo umasikini.

Kwa hivyo Mhe. Waziri alipojibu hiyo hoja hakunambia kama hilo suala aidha watalifanya, au hilo suala kalikubali au kalikataa alisahau kunijibu sijui kwa bahati mbaya au vipi, sasa nataka kujue kwamba nilimtaka awape elimu watu wetu ili wapate kukuza.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Subeit jana nilipokuwa na *wind up* Mhe. Ramadhani Abdalla Shaaban alisahau hata jina langu kunita ilibidi aulize ni Waziri gani aliyekuwa wa elimu, sasa na leo nilipokuwa natoa maelezo nimesema kitu cha msingi katika bajeti yangu nimekieleza tutatoa mafunzo na tutaelimisha wajasiria mali wote, nilieleza bayana kwa hivyo kwa sababu kalikumbuka jina langu na mimi namthibitishia kwamba namkumbuka na masuala hayo tutayafanyia kazi kama nilivyotoa maelezo kwenye maelezo yangu.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti nakubali lakini nilikuwa na jengine nataka nilichomeke kabisa hapa hapa kabla ya kumaliza zamu yangu, nilimtaka Mheshimiwa kwamba Wilaya yangu ya Micheweni ni Wilaya moja ambayo kuwa ina umasikini mkubwa na hata kwenye vitabu vyetu na historia yetu inakubali hivyo, kwa hivyo nilimtaka katika mfuko ule wa AK na JK iwe anatoa kipaumbele kwa Wilaya yetu ya Micheweni, nikamuuliza je katika jimbo langu kuna watu wangapi ambaokuwa walifaidika na huo mfuko.

Pia nikamwambia mfuko huo wakati wa kutolewa urasimu wake kidogo ulikuwa na matatizo na walikuwa wakifaidika wale wakubwa tu, kwa hivyo Mheshimiwa alinijibu akasema kama Micheweni na wao walifaidika, lakini sasa nataka anijibu kwamba atatoa uthibitisho gani kwa Wilaya yangu ya Micheweni hasa ukizingatia kama ni watu waliokuwa wana unyonge unyonge.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Mwenyekiti Mhe. Subeit Khamis Faki nilitoa maelezo na nikakutaja wewe mwanzo kwamba Mhe. Subeit Wilaya ya Micheweni tumeipa *priority* hata kabla hujaniomba, sasa ninachokuomba tembelea kwenye jimbo lako wakulize wananchi nina hakika watakwambia kwamba tumewapa *priority*. Lakini nakuahidi vile vile kwamba nimesema hapa nitayatembelea majimbo yote

Hamsini nilitoa kauli hii mbele ya wajumbe wote ili tuweze kuwashirikisha na ulipiga makofi sana niliposema tutashirikiana na wewe nitakapokuja huko jimboni ili kuwahamasisha wananchi.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti kwa sababu Waziri amesema kwamba amenipa kipaumbele na kuna watu wengi waliofaidika basi namuomba aendelee kuwafaidisha watu wangu.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti nilipokuwa nikichangia hotuba yangu nilizungumzia juu ya wasi wasi wangu kuhusu mikopo hii ya AK na JK ambayo ilikuwa ikitolewa, nikasema kwamba huenda mikopo hii inatolewa visivyo inaanalia maeneo zaidi kuliko maeneo mengine na nikatoa mfano kwa jimbo langu ambalo hata Mhe. Waziri amekubali kwamba halikubahatika na mkopo.

Lakini Mhe. Waziri alipokuwa akijibu anasema kwamba fedha hizo hazikutolewa kwa ubaguzi, yaani zilikuwa zimetolewa na ameahidi kwamba atazisimamia na hata kwangu Magomeni ziatafika, lakini sasa nimueleze Mhe. Waziri kwamba katika shehia 45 za Wilaya ya Mjini shehia zilizopata mikopo hiyo ni shehia sita tu na shehia 39 zote hazijabahatika hata mtu mmoja kupata mkopo. Sasa nilichotaka kumwambia Mhe. Waziri kwamba huo ni ushahidi fedha zile hazikutolewa kwa watu wote ni shehia sita peke yake zilizotolewa.

Sasa nataka nifahamishe tu kwamba katika kipindi chake hichi Wizara yake itafanya vipi na ukitilia maanani kwamba maombi yale yanakuwa yanapelekwa katika shehia, Wilayani zinakwenda benki sasa nini *roll* yake katika kuhakikisha kwamba watu wote wanafaidika katika maeneo yote.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Mwenyekiti, nilikiri hapa nikasema kweli kulikuwa na matatizo nikasema waheshimiwa wa majimbo mawili hawakufaidika na Mkopo wa AK na JK Jimbo la Magomeni Mhe. Salmin Awadh Salmin hakufaidika na Mhe. Haroun Ali Suleiman hakufaidika wa jimbo la Makunduchi, kwa sababu Makunduchi hawakufaidika kwa sababu tayari tulishakuwa tumeshahamasisha sisi wenyewe viongozi wawakilishi pamoja na wabunge tulikaa tukawahamasisha wananchi wetu mapema. Kwa hivyo wakaona kwamba labda hakuna haja ya kuomba mikopo ile, lakini haki ile wanahitajia kupata kama wananchi wote wanaoishi Zanzibar na Magomeni hivyo hivyo.

Sasa nilichosema kwamba sasa hivi tumebadilisha utaratibu na nilisema hapa Mheshimiwa kwamba sasa hivi mikopo itaanzia kwa masheha, lakini tutahakikisha kwamba waheshimiwa wabunge na wawakilishi wanashirikishwa, halafu zinakwenda Wilayani halafu Wilayani zinakuja

Wizarani kwangu pale kuna kitengo maalum kitashughulika na masuala yale, kama kuna watu wote ambao wameomba na wana matatizo katika kuomba, tutawafahamisha na nitawapa fomu nyengine ili wengi baadae wapate mikopo hiyo, lengo ni kuhakikisha kwamba katika miaka mitano ijayo wananchi wote wa Zanzibar hatuwezi kuwapa wote lakini wale ambao watabahatika kaatika maeneo mengi au sehemu zote za Unguja na Pemba wafaidike na mikopo hiyo Mhe. Spika,

Kwa hivyo tutajitahidi kuhakikisha kwamba fursa hizo wanazipata na wale ambao wamezikosa tutawapa *priority* ili waweze kufaidika na mikopo hiyo.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahasante kwa mujibu wa maelezo ya Mheshimiwa lakini naaka akubali kwamba fedha hizi zilipotolewa hazikutolewa kwa ajili ya wananchi wote, nimetoa mfano kwamba fedha katika shehia 45 mimi nazungumzia Wilaya ya Mjini katika shehia 45 ni shehia sita tu zilizofaidika, kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri akubaliane na hoja yangu kweli fedha hizi zilikuwa hazitolewi kwa utaratibu ule na yeye sasa hivi atasimamia ili kuhakikisha kwamba sheria zote zinafaidika japo sio kwa watu wote, lakini kila shehia hiyo keki iliyokuwepo kila mmoja anafaidika nayo kuliko vile fedha ambavyo zimetolewa.

Haiwezekani kwamba shehia 45 zipate shehia sita kwa hivyo namuomba akubaliane na hoja yangu kwamba utaratibu uliokuwa ukitumika wakati ule hakukuwa sahihi na sasa hivi anataka kurekebisha ili kila mmoja afaidike.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mimi siwezi kukubali moja kwa moja kwamba utaratibu ulikuwa haufai kwa sababu Waziri aliyekuwa anahusika na dhamana ile alikuwa na utaratibu wake, sasa kama alipanga yeye akaona ni sahihi. Mimi nimekiri hapa kwamba sasa hivi tumegundua kuna kasoro za hapa na pale sidhani kama utaratibu ulikuwa mbaya, lakini kinachohitajika sasa hivi nilichosema ni kwamba tumerejesha *system* ile AK na JK tuhakikishe sisi Wizarani wenyewe tunairatibu na kuipitisha halafu tena ndio tunaipeleka Benki. Hili la shehia sita kwamba ndio waliopata sijui kama hizi nyengine zimeomba na kama wameomba hawakupata labda kulikuwa na sababu wakati huo, sisi tunasema sababu zilizokuwa za msingi hawakukidhi pengine kupata mikopo hiyo, tunachofanya sasa hivi kama hawakukidhi yale ambayo yanahitajika basi ni kuwahamisha ili warudi na walete maombi yao tena ili tuwape mikopo hiyo.

Mhe. Salmin Awadh Salmin asiwe na wasi wasi hilo tutalifanyia kazi na mimi nilisema tumelirekebisha hilo baada ya kuona kulikuwa na matatizo ya hapa na pale, siwezi kutoa *statement* ya kusema kwamba Waziri mwenzangu aliyekuwa katangulia kafanya makosa hiyo siwezi kusema kwa sababu alifanya hivyo kwa

maamuzi ambayo wakati ule yalikubalika, ndio maana yake pesa zile tukazipeleka bank.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti naomba tuendelee.

Kifungu 0401	Idara ya Mipango sera na Utafiti	109,000,000
Kifungu 0501	Idara ya Uendeshaji na Utumishi	

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti nilipokuwa nikichangia Idara hii nilimpongeza Mhe. Waziri kwamba mwaka jana alitoa mafunzo ya watendaji ishirini ndani na nje ya nchi, nikaona mwaka huu pia ametenga milioni 47,500,000 lakini ni kuwafunza ndani ya nchi tu. Sasa nikaomba kujua tu kwenye fedha hizi kwa nini mara hii hakumalizia wale watendaji wake kwa mafunzo ya nje na sera hizi labda itawasilisha wafanyakazi wangapi, naomba kujua kidogo unielimishe kidogo.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Ni kweli safari hii hatukuweka bajeti ya kuwapeleka nje, lakini hata hivyo haijazuia pale ambapo zitatangazwa *scholar ship* na taasisi mbali mbali kuomba Wizara ya Elimu wana utaratibu wa kupokea *scholar ship* mbali mbali na wanazitangazia. Kwa hivyo itawapa fursa wananchi wote wa Zanzibar popote pale walipo sio lazima wafanyakazi wangu sarafi hii kwa sababu kuna vijana wengi wako nje sasa hivi wanaendelea kusoma, kwa hivyo tuendelee tena na tulizokuwa nazo chache nakusudia kuzitumia kwa ajili ya wale kuliko kuwapeleka wengine tukashindwa kuwalipia.

Kwa hivyo safari hii tumekusudia kusomesha hapa hapa nchini ili kuweza kukidhi mahitaji hayo.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu 0501	Idara ya Uendeshaji na Utumishi	490,874,000
Kifungu 0502	Idara ya Mikopo	

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi hii pamoja na majibu mazuri aliyonipatia Mhe. Waziri kuhusu masuala ya mikopo, lakini pia ningeliomba nipate ufafanuzi kutokana na mikopo inavyotoka. Mhe. Mwenyekiti mikopo inavyotoka ni mashirikiano makubwa baina ya wakuu wa Wilaya, Masheha na Kamati zao za masheha na kwa bahati mbaya Sheha anateuliwa nay eye binafsi anateua kamati yake na ndivyo anavyoshirikiana na kamati yake kutoa hii mikopo, vile vile hivi ndivyo inavyotokea hata panapoundwa vikundi vya ushirika.

Mhe. Mwenyekiti mimi binafsi na kamati yangu ilibidi wakati mwengine hata hizo kamati ziliopo za ushirika tuzivunje na zifanye uchaguzi mpya kwa kushirikiana na Wizara husika, kutokana na mambo yalivyokwenda kinyume na utaratibu.

Mhe. Waziri anaweka mpango gani hasa uliokuwa madhubuti wa kuona kuwa mikopo hii inatolewa kwa mujibu inavyokusudiwa. Yaani isiende upande mmoja wa kisiasa au sheha asitumiwe kwa sababu ya kamati yake na watu maalum wengine wakawa wanakosa kwa sababu ya sheha, maana ule mpango hasa ulio wazi utakaotumika utakaonekana kuwa mikopo hii inawafika watu waliokusudiwa.

Mhe. Waziri wa Kazi Uwezeshaji Kiuchumi Wananchi na Ushirika: Mhe. Mwenyekiti, naomba nirejee hayo ambayo nimeyazungumza hapo nimeeleza wazi wazi kwamba tumegundua kwamba utaratibu uliokuwa unatumika wakati ule unaanzia kwa Sheha, Mkuu wa Wilaya unakwenda Benki. Nimesema Wizara hii sasa hivi Mhe. Salum tutafanya utaratibu kuwaambia masheha kwamba wakati wanapopeleka maombi yao nimesema Wabunge na Wawakilishi watashirikishwa, kwa makusudi lakini nimesema tunashirikisha wabunge na wawakilishi sio kwa lengo la kisiasa ili wajue tu kuna mambo haya yanatendeka katika majimbo yao.

Kwa sababu hatutaki tuje kutoa mikopo kwa njia moja au nyengine ikaonekana kuna hisia za kisiasa wananchi wote wa Zanzibar wana haki ya kupata waliokuwa na vyama na wasiokuwa na vyama wote wana haki ya kupata mikopo hiyo, lakini pia haitomalizika benki moja kwa moja itapitia kwanza wizarani kwangu, kuna kitengo nimeeleza Mhe. Mwenyekiti, mara nyingi sisi ndio tutahakiki yale masuala na kama tukigundua kuna kasoro Mhe. Salim watu wa Mtambwe wameomba wengine hawakupata tutawafahamisha kwamba nendeni kajazeni fomu hii upya halafu tuleteeni sisi tutakufahamisheni na baadae wapate haki yao.

Kwa wale ambao wanastahiki watapata lakini kuna vigezo vya kupata mkopo sio kila anayeomba anapata mkopo, lazima kuna masharti yake uyatimize haiwezekani kwamba kwa sababu tunataka apate mkopo fulani nae lazima hiyo haiwezekani, kuna taratibu zitawekwa wakikidhi mahitaji hayo basi wakae mkao wa kupata mkopo.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana kwa jibu la Mhe. Waziri na hii ndio sababu ya mikopo hii inapoletwa ikawa sisi hatuna habari yoyote wanaifanya kisiri siri kwa sababu ya kufanikisha mipango yao, ushauri wangu tusiarifiwe tu lakini tushirikishe kikamilifu pamoja na madiwani wetu pia ili tuone kuwa haki inatendeka.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi naomba nianze kwanza kwa kumshukuru sana na nimpongeze Mhe. waziri kwa jinsi alivyojibu kwa umakini wa hali ya juu kabisa.

Mhe. Mwenyekiti wakati nachangia nilimuomba Mhe. Waziri kwamba ili kuondosha matatizo na shutuma zilizoko huko mitaani lazima afike pahala atueleze kama Baraza la wawakilishi na kama wawakilishi na atupe ushahidi wa jinsi mikopo hii ilivyotolewa katika majimbo yetu. Nashukuru Mhe. Waziri kalitekeleza hilo na mara tu alipoingia hapa katugawiya zile karatasi, haraka haraka niliangalia nikaona Chake Chake wamo nilifurahi sana. Lakini nilichukizwa kidogo na kile kitendo alichosema kwamba tuzikusanye kwamba ni siri kati ya benki na wateja.

Mhe. Mwenyekiti hili ni Baraza la Wawakilishi na lina nguvu zake tukirejea sheria Namba 4 ya mwaka 2007 inayohusiana na kinga fursa na uwezo wa Baraza kifungu cha 19 (2) kinasema hivi. Naomba kwa ruhusa yako Mhe. Mwenyekiti nikisome.

"Sheria unless the president otherwise direct in writing no public officer shall refeuse (a) to give before the house or a committee there any evidance or (b) the produice before a house a committee an document".

Mhe. Mwenyekiti sasa hii ni sheria inayoeleza kwamba ofisa yoyote hatokataa labda rais aeleze vyenginevyo kulikabidhi baraza hili *document* ambazo tunazihitaji, benki ni *public sector* sasa kama baraza hatuna maana yake kuna siri gani ambayo yale ni mahisabu yetu, sasa mimi nadhani mwenyekiti nipate muongozo wako, hivi baraza hili halina uwezo wa kutaka mambo kama haya kwa sababu kile kinachoendelea pale ni zile *public money* ambazo baraza inataka kujue nini kinachoendelea. Kwa hivyo naomba muongozo wako Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. waziri alisema mapema kwamba yeye hakatai na ndio maana akazileta zile kwa ajili ya kutoa hizo taarifa ambazo waheshimiwa wajumbe mmeziomba, lakini akakuta kwamba kuna kikwazo kinachohusu mteja na benki akaomba basi Mhe. Spika, naomba utoe muongozo wako juu ya hili ambao na wewe sasa unaomba hivyo hivyo.

Mimi nadhani kwa jambo hili ni jambo la nchi ni jambo la serikali na hivi fedha ni za serikali na tayari waheshimiwa wajumbe mmeomba mshirikishwe katika suala hili hili, hakuna sababu kwamba tusijue taarifa hizi. Kwa hivyo muongozi ninaotoa kwamba taarifa zile tutazitoa na kama alivyokiri Mhe. waziri kwamba wajumbe washirikishwe katika safari zinazokuja huko mbele na sote tukakubaliana kwamba iwe hivyo basi kushirikishwa kiasi hicho huko

maana yake hata hiyo siti itakuwa haipo, kwa hivyo kwa hii pia hakuna sababu ya kuzuia.

Kwa sababu hatimae wananchi wanapokosa wanawatuma nyinyi wawakilishi wao, kwa hivyo taarifa hizi zitagawiwa ili waheshimiwa wajumbe tuzielewe na kama alivyoahidi Mhe. Waziri ushirikishwaji utakuwepo ndani ya majimbo yetu wawakilishi wa wananchi.

Kwanza sijui kama mmeridhika Mhe. Omar Ali Shehe.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti hii ndio maana ukachaguliwa kuwa Spika, katika baraza hili kwamba hizo document tuzipate ili tumsaidie Mhe. Waziri kupata madeni yanayodaiwa. Naomba tuendelee.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti nilipokuwa nikichangia katika sehemu hii ya Idara ya Mikopo kulikuwa na mambo mawili niliyauliza, moja nashukuru kanipatia maelezo Mhe. Waziri la kwanini hutolewa ruzuku kwa Idara lakini nasikitika maelezo yake mimi hayakunitosheleza, kwa sababu nilisema Idara hii pamoja na Idara nyengine sasa ningeomba kuelewa kwamba ruzuku pale uendeshaji kwa maana ile mikopo, lakini ninapoona kuna ruzuku kwa ajili ya mishahara halafu kuna fungu la jumla tu Mhe. Mwenyekiti ninapata matatizo. Kwa sababu nimezoea kuona katika Idara nyengine zote kuna mchanganuo wa yale matumizi ambayo yanakwenda pale kwa kazi za kawaida, lakiini idara hii inaonekana ya aina yake na peke yake na katwambia kwamba kaiombea iwe hivi.

Sasa naomba nipate maelezo kwa nini iombewe hivyo kwa sababu hii ni idara sio shirika linalojitegemea, sio kama taasisi nyengine zinazojitegemea na kupewa ruzuku, sasa nilikuwa nataka maelezo kwa sababu hapa Mhe. Mwenyekiti, tunapitisha matumizi ya fedha za walipa kodi zikijumuishwa namna kama hii utaratibu wake wa kuzifuatilia kwa kamati za Baraza lako Mhe. Mwenyekiti, kwa vyombo vyengine inakuwa ni tofauti na vyombo vyengine inakuwa ni tofauti na iinapokuwa zimewekwa na zimechanganuliwa kwa kila kimoja kwa matumzi yake.

Kwa hivyo hili naomba maelezo hasa kwa kifungu kinachohusu mishahara ile uendeshaji nasema inahusu mambo mengine sijui, lakini nataka maelezo.
Lakini la pili Mhe. Mwenyekiti, hapo hapo niliuliza kwamba katika ule mchanganuo wa mikopo na marejesho wa mfuko wa kujitegemea ambao ulikuwa ukisimamiwa hapa ni kwamba kwa upande wa Unguja yaonekana zilitolewa milioni 48 lakini zimerejeshwa milioni 55 nikaomba maelezo kwa sababu Pemba ni tofauti hapa zilizorejeshwa zinaonekana ni nyingi zaidi sasa

ni upungufu wa mahisabu, wamarejesha na faida, naomba maelezo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Kazi Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Mwenyekiti nilieleza mwanzo kwamba pesa za ruzuku ni maalum tuliziomba Wizara ya Fedha, suala la ulipaji wa wananchi mikopo imekuwa ni tatizo kubwa sana hapa katika nchi yetu, tukasema ili idara hii iweze kufanya kazi vizuri tunaomba tupatiwe ruzuku ya kuweza kuwafuatia wananchi huko vijijini walipo, ili waweze kuhamasishwa na waweze kulipa mikopo ile. Kwa hivyo tukaomba wenzetu Wizara ya Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo wametukubalia, naomba Mheshimi pamoja na waheshimiwa wote wa baraza hili wakubali kwamba suala la kulipa mikopo limekuwa tatizo kubwa sana.

Kama hatujaweka kifungu hiki kuwasaidia wenzetu hawa wa Idara hii kwa kufuatilia Mheshimiwa tutaendelea kukwama na sisi hatutaki tukwame, kwa hivyo naomba atuelewe kwamba ilikuwa ni ruzuku maalum, ombi maalum Wizara ya Fedha wakalikuabli hilo kwamba tutumie kufungu hicho kwa ajili ya kuisaidia Idara hii, inawezekana kwa mwaka huu tu pengine mwakani kisiwepo kabisa kwa sababu tayari taaluma itakuwa imeshawafika wananchi hakutokuwa na haja tena ya kufanya hivyo.

Suala lake la pili naomba anikumbushe kidogo.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti suala langu la pili lilikuwa katika ukurasa wa 30 na 31 wa kitabu chake baada ya mikopo ile AK na JK amezungumzia mikopo inayotoka katika mfuko wa kujitegemea, nilisema kwa ufupi tu kwa kuwa ilikuwa nimeshalizungumza lakini bora nieleze kwa ufasaha nielewe, nasema ametwambia hapa kwamba katika sehemu hii kulitolewa milioni 83 kwa mikopo halafu katutolea *break down* ya Unguja na Pemba, sasa katika kurejesha nasema Pemba ilipatiwa milioni 35,100,000 kilichorejeshwa ni milioni 37.900,000.

Lakini Unguja kulitolewa milioni 48,700,000 zilizorejeshwa milioni 55,128,250 sasa ndio maana nikataka maelezo kwamba, huku zimezidi fedha zilizorejeshwa ni zaidi ya zile ambazo zilitolewa, ndio maana nikauliza kulitolewa na faida, kwa sababu tulivyozoea kuona sote ni kwamba wananchi wetu wana matatizo ya kurejesha mikopo, sasa hapa imezidi asilimia mia moja tofauti na kwengine kote ndio maana nikataka maelezo kumepita nini katika mahisabu hapa, naomba maelezo.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Jussa alikuwa mwanafunzi wangu Haile Selassie nilipokuwa nafundisha hesabu mwaka thamanini na hizo, nilimfundisha hisabu sasa hizi zimekuwa

zimerejeshwa nyingizaidi kutokana na zile za nyuma ambazo hatukuzitia kwenye bajeti imeweza kurejeshwa, sasa hizi kimeongezeka hapo.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti nashukuru ndio maana nilimwambia Mhe. Waziri wakati anachangia kama mimi ananikumbuka nilikuwa pochwe wa hisabu na nilikuwa mgumu wa kufahamu, lakini sasa nashukuru kwamba kanieleweshа na yeye mwenyewe shahidi kwamba nilikuwa posho sana alipokuwa akinisomesha kwa somo lake.

Lakini hili la mwanzo hili la ruzuku naomba kidogo maelezo ya ziada, kwatwambia kwamba hii ni kutokana na kufuatilia mikopo kwa urahisi kwa mikopo ambayo hairejeshwi, sasa mimi kidogo ananipa mashaka Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu anasema hata ingechanganuliwa katika fungu la kawaida la Idara kunakuwa na fungu la usafirishaji kama magari, kama ni fungu la safari kunakuwa na fungu la safari za ndani na nje. Sasa kama ni suala la kufuatilia kama hizo safari za ndani ya nchi itakuwa na fungu lake, sijapata majibu ya kuniridhisha Mhe. Mwenyekiti, kwa nini kuwe na fungu la jumla jumla katika idara hii la ruzuku tofauti na wizara nyengine. Kama hoja ni kwenda kufuatilia mikopo tu maelezo ya Mhe. Waziri hayakidhi haja, lakini kwa kuwa katwambia kwamba hii ni mara yake ya mwanzo tumuachie nakubali tumuachie lakini mwakani Mhe. Mwenyekiti, suala kama hili lisije katika namna kama hii. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu 0502	Idara ya Mikopo	110,000,000
Kifungu 0601	Idara ya Ajira	94,000,000
Kifungu 0701	Idara ya Usalama na Afya Kazini	104,000,000
Kifungu 0801	Kamisheni ya Kazi	

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kwenye mchango wangu katika Kamisheni ya Kazi katika mambo mengi niliyoyazungumza nilizungumzia suala la kazi ambazo kimsingi hazipaswi kufanywa na wageni. Nashukuru yale maelezo ya ajira katika mahoteli Mhe. Waziri ametupa maelezo mazuri kwamba atafuatilia, lakini kulikuwa na suala zima nililolizungumza la baadhi ya kazi ambazo sheria za Zanzibar za kazi haziruhusu kufanywa na wageni na nikatoa mfano wa kazi za *tours* ambazo sheria zetu zinakataa *specifically* kwamba hizi zinapaswa zifanywe na wenyeji ili ziwafaidishe. Sasa ametwambia atafuatilia lakini nilikuwa nataka Mhe. Waziri anambie kwamba anahitaji tumpe muda gani ili tuone suala hili Kamisheni ya Kazi inalisimamia na kulimaliza ili lisiendelee kuwa tatizo katika Zanzibar yetu.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Mwenyekiti, narejea tena katika maelezo yangu kuweka bayana kwamba, tutaanza kufuatilia wawekezaji wote ambao wameajiri wafanyakazi ambao

kisheria hawawajibiki kuajiriwa katika sekta hizo. Lakini hatuwezi kusema leo wawaondoe mara moja hoteli zetu zika-*collapse* na uchumi tunahitajia na mapato tunayataka. Kwa hivyo, nimesema kwa mwaka huu wa fedha 2011/2012 tutafuatilia na kuona wale wote ambao wameajiriwa katika maeneo ambayo kwa mujibu wa sheria hawawajibiki basi wanatafutiwa mbadala na tunaweka wazalendo katika maeneo hayo.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, hakunipa maelezo ninayoyahitaji, nilikuwa nahitaji atwambie ni muda gani kama mwaka mmoja, miwili au mitatu kwa sababu hii sheria kama tunazipitisha hatimaye nguvu ya sheria na thamani yake ni kuona kwamba zinatekelezwa na kufanya kazi. Sasa kweli serikali tunataka mapato lakini pia upande mwengine tunaathirika kwamba watu wetu wanakosa ajira na nimesema Jimbo la Mji Mkongwe ni moja katika majimbo ambayo yanaathirika sana kwa sababu ziko hizi *tours operators* kuna watu wanaopeleka watu visiwani kule, hizi zote kwa mujibu wa sheria zetu zinapaswa zifanywe na Wazanzibari na zisifanywe na wageni. Sasa akinamba tu kwamba tutafuatilia lakini tunahitaji mapato naona kama ni majibu ya kisiasa zaidi Mhe. Mwenyekiti. Naomba anambie *specifically* mwalimu wangu suala hili atalisimamia na anahitaji muda gani kama mwaka mmoja au miwili lakini tuwe na kipimo na ndio faida ya kuona Baraza ambalo linafanya kazi yake sawa sawa.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Ismail Jussa alikuwa anasema hafahamu hesabu sasa sijui nimwambie afahamu na nini. Kwa sababu nilisema katika bajeti hii ya 2011/2012 tutahakikisha masuala hayo tunayafuatilia. Kwa hivyo, nikisema *financial year* basi maana yake ni kipindi cha.….*period of one year*. Kwa hivyo, Mhe. Jussa nadhani ni *one year*, tutafanya hilo kwa sababu hatuwezi sasa hivi ghafla tukawaambia wawekezaji wale ambao tumewakubali wenyewe, wamekuja hapa wakawaajiri, kama sheria zimepingwa ni wajibu sasa kwenda nao tukatumia busara na hekima ili kuwaambia bwana wee kwa mujibu wa sheria pengine wamewaajiri wale bila ya kujua sheria zile. Nafasi hii haiwajibiki kupata mgeni inahitaji kupata mzalendo na Mheshimiwa tumeanza kufanya hivyo na tumefanikiwa kwa kiasi kikubwa sana.

Kwa hivyo, tunaomba muda huu wa bajeti ya 2011/2012 tulirekebishe hilo ili vijana wetu wenye sifa, kwa sababu wakati mwengine inaweza kutokezea nafasi ile tunamtaka mtu pengine hana sifa hatuwezi kumsisitiza tu yule bwana kwamba amuondoshe mtu yule, tunaweza tukampa kibali cha muda akafanya kazi kwa kujua kwamba siku yoyote atapopatikana mzalendo ambaye ana sifa zile akaweza ku-*accommodate* na akaziba nafasi ile. Kwa hivyo, ni kipindi cha mwaka mmoja Mhe. Ismail Jussa tutafanya hiyo kazi.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nafurahi kwamba sasa amenitamkia mwaka mmoja lakini naomba tu, nimalizie kwa kusema kwamba inanipa wasi wasi hii kauli yake ya mwisho. Naomba hili Mhe. Waziri alirekebishe, anaposema kwamba kwa nafasi ambazo hatuna watu. Nimetoa mifano hapa Mhe. Mwenyekiti, *specifically* hatuna upungufu wa watu wanaoweza kufanya kazi za *tours* Zanzibar na wenyewe wanaofanya kazi hizi *locally* wanapiga kelele kwamba wanakosa kazi kwa sababu wanafanya watu wengine ambao hawapaswi kuzifanya, ni tofauti na zile kazi nyengine ambazo labda zinakosa Wazanzibari.

Sasa kwa sababu kasema atafuatilia nakubali tuendelee ndani ya mwaka mmoja tukijaaliwa tutakuja kumuuliza Mhe. Waziri kafikia wapi. Lakini katika kufuatilia nataka alikumbuke hilo tu kwamba sizungumzi zile nafasi za mameneja au watu wengine ambao hatuna, lakini pia kuna kazi kama hizi ambazo sheria zetu *specifically* zinakataza kufanywa na tunao Wazanzibari lakini *competition* inakuwa mbaya zidi yao kwa sababu kuna watu ambao wanajiingiza katika kazi ambazo haziwahusu. Kwa hivyo naomba alifuatilie hilo na baadae naomba tuendelee.

Kifungu 0802	Kamisheni ya Kazi	222,000,000
Kifungu 0901	Idara ya Uendeshaji na Uratibu wa Mpango na Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi	123,000,000
Kifungu 1001	Idara ya Ushirika	175,000,000
	Jumla ya Fungu	**1,545,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu 0401	Idara ya Mipango Sera na Utafiti	90,000,000
	Jumla ya Fungu	**90,000,000**

(Baraza lilirudia)

Mhe. Spika: Ahsante sana Waheshimiwa Wajumbe, makofi yamekuwa mengi mpaka askari wangu wameshtuka.

Mhe. Waziri wa Kazi Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, ilivyokuwa kamati ya matumizi imejadili na kupitisha makadirio ya fedha ya wizara yangu bila ya mabadiliko. Sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza liyakubali makisio hayo. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: niwahoji basi Waheshimiwa Wajumbe, wale wanaokubaliana na makadirio hayo wanyooshe mikono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, UTALII NA MICHEZO KWA MWAKA WA FEDHA 2011/2012

UTANGULIZI

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, kwa niaba ya Wizara yangu na kwa idhini yako naomba kusoma bajeti yangu hii.

Kabla sijasoma bajeti ningependa nichukue fursa hii kutangaza na kujulisha rasmi kwamba nimefanya uteuzi wa wafuatao kuwa wajumbe wa Baraza la Taifa la Michezo nao ni:-

	JINA	**ANAPOTOKA**
1.	Mussa Abdulrabi Fadhil	Wizara ya Elimu
2.	Amran Masoud Abdallah	Pemba
3.	Hassan Haji Silima	Walemavu

Vile vile ningependa nitoe taarifa ya furaha, kwamba leo tumepokea kikundi chetu cha wanajudo ambao wamekuja na medali ya dhahabu. Vijana hawa walishiriki katika mashinda ya judo ya Afrika Mashariki na Kati na leo tumewapokea saa 9 na medali ya dhahabu. Hiyo ni taarifa tu.(*Makofi*).

Mhe. Spika, baada ya hapo napenda kuchukua fursa hii nitoe taarifa ya bajeti yangu.
Mhe. Spika, kwa ruhusa yako, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ili lipokee, lijadili na hatimaye lipitishe Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Mhe. Spika, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu mwenye wingi wa Rehema kwa kutujaalia kukutana tena tukiwa na afya njema; pia nchi yetu ikiendelea kuwa na amani na utulivu baada ya kumalizika Kura ya Maoni pamoja na Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2010 uliowezesha kupatikana kwa Serikali yenye muundo wa Umoja wa Kitaifa inayoongozwa na Mhe. Rais wa Zanzibar Dk. Ali Mohamed Shein. Aidha, nichukue fursa hii kukishukuru chama changu cha *CUF* kwa kunipendekeza kuwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo na vile vile nimshukuru Mheshimiwa Rais wa

Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein kwa kuniteua kuwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo.

Mhe. Spika, kwa niaba ya viongozi na wafanyakazi wa Wizara yangu, naomba kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mhe. Dk. Ali Mohamed Shein, kwa kuchaguliwa katika uchaguzi Mkuu uliopita kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi; Mhe. Seif Sharif Hamad, kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais na Mheshimiwa Balozi Seif Ali Idd, kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Spika, kwa kuzingatia kwamba hiki ni kikao chetu cha kwanza cha Bajeti ya Serikali tokea kumalizika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2010, naomba pia kukupongeza Mhe. Spika, wewe binafsi, kwa kuchaguliwa tena kuliongoza Baraza hili tukufu likiwa katika mfumo mpya na sura nyingi mpya. Pia nampongeza Mhe. Naibu Spika, pamoja na watendaji wote wa Baraza hili ambao tutakuwa nao pamoja katika kazi zetu za kila siku za kupitisha maamuzi mbali mbali ya Serikali.

Mhe. Spika, wakati nikijitayarisha kuwasilisha hotuba yangu ya Bajeti ya mwaka 2011/2012, naomba niungane na waheshimiwa wenzangu wa Baraza hili kutoa mkono wa rambi rambi kwa familia ya aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana na Watoto Marehemu Rahma Moh'd Mshangama. Rambi rambi hizi pia ni kwa Waheshimiwa viongozi, wafanyakazi wote kwa ujumla, kwa kuondokewa na kiongozi mwenzetu wa Serikali, Mola ailaze roho ya Marehemu mahala pema Peponi - Amin.

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo, sasa niruhusu kutoa maelezo kuhusu muelekeo wa bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Katika maelezo hayo nitatoa uchambuzi wa malengo tuliyoahidi kutekeleza katika mwaka wa fedha 2010/2011 na utekelezaji wake. Kisha nitaeleza malengo ya mwaka wa fedha 2011/2012 ambayo Wizara imekusudia kuyatekeleza baada ya kupatiwa fedha tunazoziomba.

Mhe. Spika, kabla ya mabadiliko ya Serikali na Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2010, Wizara yangu ilikuwa ikisomeka Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo na sasa inajulikana Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo. Haya ni mabadiliko ya msingi ndani ya Serikali ya Awamu ya saba kutokana na kuengezeka sekta ya Utalii na Idara ya makumbusho na Mambo ya Kale. Kutokana na hali hiyo Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo imeundwa na taasisi (18) zifuatazo:-

i. Idara ya Uendeshaji na Utumishi,
ii. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti,
iii. Shirika la Utangazaji Zanzibar
iv. Idara ya Habari Maelezo,
v. Shirika la Magazeti ya Serikali,
vi. Chuo cha Uandishi wa Habari,
vii. Tume ya Utangazaji,
viii. Kamisheni ya Utalii,
ix. Shirika la Utalii,
x. Chuo cha Maendeleo ya Utalii,
xi. Hoteli ya Bwawani.
xii. Kamisheni ya Utamaduni na Michezo,
xiii. Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale,
xiv. Baraza la Kiswahili
xv. Baraza la Sanaa,
xvi. Bodi ya Sensa ya Filamu na Sanaa za Maonesho,
xvii. Baraza la Taifa la Michezo na
xviii. Kituo cha *EACROTANAL*,

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, Wizara yangu ilipangiwa kupata shilingi 4,802,334,446 kwa kazi za kawaida na shilingi 875,000,000/= kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia mwezi wa April 2011, Wizara ilikwishapatiwa jumla ya shilingi 3,622,725,608/= kwa kazi za kawaida, sawa na asilimia 75 na shilingi 625,000,000/= kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 71 (Tafadhali angalia Viambatisho Nam. 1a na 1b).

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2010/2011,Wizara ilipanga kukusanya mapato ya shilingi 1,126,800,000/=. Hadi kufikia April 2011, Wizara imeweza kukusanya jumla ya shilingi 1,007,235,117/= sawa na asilimia 89 (Tafadhali angalia Kiambatanisho namba. 2).

MAPITIO YA UTEKELEZAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2010/2011

Mhe. Spika, malengo tuliyojipangia kuyatekeleza na utekelezaji wake kwa mwaka wa fedha 2010/2011 kiidara na taasisi zilizo chini ya Wizara ni kama ifuatavyo:-

IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

Mhe. Spika, Idara hii iliundwa baada ya bajeti ya mwaka 2010/2011 na ilibeba baadhi ya shughuli za Idara ya Mipango zilizoidhinishwa na Baraza lako tukufu. Katika kutekeleza majukumu hayo, Idara imeweza kulifanyia ukarabati jengo tulilokabidhiwa na Serikali kuwa Makao Makuu ya Wizara kwa

kulifanyia ukarabati, kulitia rangi nje na ndani, kuliezeka upya, kuliwekea miundombinu mipya ya maji na umeme, kununua samani, kununua vitendea kazi, kama vile Kompyuta na printa zake pamoja na kuweka huduma za mawasiliano ya simu, nukushi (*fax*) na Intaneti.

Mhe. Spika, idara hii pia imefanikiwa kuwapatia ajira za kudumu wafanyakazi wa STZ, TVZ, Habari Maelezo na Hoteli ya Bwawani ambao walikuwa wakifanyakazi kwa mikataba ya muda mfupi na kujitolea. Jumla ya wafanyakazi 147 wanawake 90 na wanaume 57 wamepatiwa ajira hiyo. Ufafanuzi wa ajira hizo unaonekana katika kiambatanisho namba 3.

Mhe. Spika, wizara imeweza kuitisha vikao 6 vya Zabuni kwa ajili ya kutafuta wazabuni wa kusimamia na kuendesha taasisi zinazohitaji wawekezaji na ujenzi. Kazi zilizopatiwa wazabuni ni ukarabati wa jengo la Makao Makuu ya Wizara, Uchoraji wa ramani wa Jengo la Chuo cha Habari litakalojengwa Tunguu, kukodishwa kwa Ukumbi wa Komba Disco Bwawani Hoteli, Ujenzi wa Chuo cha Maendeleo ya Utalii Maruhubi na upatikanaji wa vifaa vya Chuo hicho pamoja na kupatikana msimamizi Ujenzi wa Jengo jipya la Chuo cha Maendeleo ya Utalii Maruhubi. (Maelezo ya ndani ya zabuni yanaonekena katika kiambatanisho namba.4)

Mhe. Spika, idara hii imeweza kuwapatia nafasi za mafunzo wafanyakazi 71, kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo na Wizara inayohusika na Elimu ya Juu. Kati ya hao, wafanyakazi 40 ni wanawake na 31 wanaume. (Angali kiambatanisho namba.5)

Mhe. Spika, majukumu ya msingi ya Idara ya Uendeshaji na Utumishi ni kusimamia shughuli zote za Utawala, Utumishi (Rasilimali watu), Maendeleo, wajibu na maslahi ya wafanyakazi wote na kusimamia udhibiti wa bajeti katika Wizara. Katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Idara imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kuongeza ufanisi wa uongozi na Utawala katika taasisi zote zilizo chini ya Wizara kwa kusimamia na kutathmini utendaji wa kazi kwa watendaji wa Wizara.

2. Kusimamia upatikanaji wa nafasi za masomo na mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu kwa watumishi wa wizara ili kuwa na wafanyakazi watakaokuwa na ujuzi na uwezo katika utekelezaji wa majukumu ya wizara.

3. Kusimamia na kuimarisha upatikanaji wa miundombinu mbali mbali pamoja na vitendea kazi katika maidara yaliyomo ndani ya wizara ili kuimarisha ufanisi wa kazi.

Mhe. Spika, ili Idara ya Uendeshaji na Utumishi iweze kutekeleza malengo yake katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, naomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 637, 340,000 kwa kazi za kawaida.

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

Mhe. Spika, majukumu ya msingi ya Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ni kupanga, kutayarisha, kukagua na kutathmini mipango ya maendeleo ya wizara, kupitia Sera, kufanya tafiti mbali mbali na kusimamia utekelezaji wake. Katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, idara hii ilipanga kutekeleza malengo makuu yafuatayo:-

i. Kusimamia na kuratibu shughuli za Sera na Mipango ya Wizara.

ii. Kuendelea kuwasiliana na washirika wa maendeleo na taasisi za kimataifa katika kushirikiana ili kufanikisha utekelezaji wa malengo na mipango ya Wizara.

iii. Kuendelea kuratibu na kutoa mafunzo ya kupambana na maambukizo mapya ya Virusi vya Ukimwi kwa wafanyakazi wa Wizara.

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Spika, napenda kuliarifu Baraza lako Tukufu kuwa katika hatua ya awali Idara imezipitia sera zake zikiwemo Sera ya Habari na Sera ya Utalii na kubaini kwamba Sera hizi zinahitaji kufanyiwa marekebisho ili ziende na wakati. Kwa upande wa Sera ya Utalii mchakato umeanza wa kuifanyia marekebisho sera hiyo. Aidha Idara imeweza kuzitafsiri Sera ya Michezo na Sera ya Utamaduni kwa lugha ya kingereza ili kukidhi haja ya watumiaji.

Mhe. Spika, pamoja na utekelezaji huo katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, Idara hii pia imefanikiwa kutekeleza malengo yake kama ifuatavyo:-

i. Kupitia Programu ya Kujengea Uwezo (JP5) Idara imeweza kuandaa Semina ya siku nne (4) ambapo wafanyakazi 107 wamefaidika na mafunzo hayo.

ii. Idara kupitia Kamati ya kutoa mafunzo ya kupambana na Ukimwi katika sehemu za ndani na nje ya kazi imefanikiwa kutoa makala za Ukimwi zipatazo 14 na matangazo yanayohusu maambukizo ya virusi vya Ukimwi na ushajiishaji wa kupima VVU kupitia gazeti la Zanzibar leo, TVZ na STZ.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2011/2012

Mhe. Spika**,** katika mwaka wa fedha 2011/2012 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuimarisha shughuli za mipango, sera na utafiti kwa maendeleo ya Wizara.

ii. Kusimamia na kuratibu utekelezaji wa sera na matokeo ya tafiti kwa shughuli za Wizara.

iii. Kuandaa mipango ya kupunguza maambukizi mapya ya virusi vinavyosababisha Ukimwi (VVU) na kuhakikisha masuala mtambuka yanaingizwa na kutekelezwa katika mipango ya Wizara.

iv. Kuimarisha vitengo vya utafiti na takwimu ili kuweka utaratibu mzuri wa ukusanyaji na utunzaji wa takwimu kwa maendeleo ya Wizara.

Mhe. Spika, ili Idara ya Mipango, Sera na Utafiti iweze kufanikisha malengo yake katika mwaka wa fedha wa 2011/2012 kwa ufanisi, naomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 76,000,000/= kwa kazi za kawaida.

OFISI KUU PEMBA:

Mhe. Spika, majukumu ya msingi ya Ofisi Kuu ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo Pemba ni kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Wizara Kisiwani Pemba. Afisi hii ni kiunganishi katika kuhakikisha kwamba majukumu, malengo na shughuli za Wizara kwa upande wa Pemba zinatekelezwa kama zilivyokusudiwa. Katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, Ofisi hii ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuvijengea uwezo vyombo vya habari ili vitekeleze majukumu yake kwa ufanisi na kwa kuzingatia Ilani ya Uchaguzi.

ii. Kulifanyia matengenezo jengo la Ofisi Kuu ya Wizara Pemba.

iii. Kuendelea kukilea Kituo cha redio jamii Micheweni.

iv. Kuendelea kuwazindua wafanyakazi juu ya kujikinga na maambukizo mapya ya Ukimwi.

v. Kuwajengea uwezo wafanyakazi ili kila mmoja afanye kazi kwa mujibu wa kada yake.

UTEKELEZAJI HALISI:

Mhe. Spika, Ofisi Kuu ya Wizara ya Habari Utamaduni, Utalii na Michezo Pemba imeviwezesha vyombo vya Habari Pemba kufanya kazi zake kwa ufanisi mkubwa kama ifuatavyo.

i. Ofisi imefanikiwa kufunga mtambo mpya wa FM wenye uwezo wa 2KW. Mtambo huo unatangaza katika mawimbi 94.1FM na unatoa matangazo ya Sauti ya Tanzania Zanzibar moja kwa moja. Kabla ya Mtambo huu kufungwa tulikuwa tukitumia *Spice FM* kusaidia matangazo ya MW na kwa sasa *Spice FM* inajitegemea kwa kuwa na vipindi vyake tofauti na vya MW na FM.

ii. Ofisi imeanza kujitegemea kwa kuwa na Afisi yake baada ya Afisi iliyokuwa ya Waziri Kiongozi kuhama katika jengo la pamoja. Hatua hiyo imetoa fursa ya kupanga idara katika makazi mazuri. Kazi ya Ukarabati wa Jengo umeanza kwa kutandaza waya za umeme (*fitting*) kwenye jengo lote na hatua ya kugawa vyumba vya ofisi inaendelea. Aidha, hatua za ununuzi wa samani zinatekelezwa kwa awamu.

iii. Ofisi imeendelea kukilea kituo cha Redio Jamii Micheweni na kwa kushirikiana na UNESCO imeweza kutoa msaada wa Redio 100 kwa wanajamii wa Jimbo la Micheweni. Jumla ya familia 100 zimefaidika na msaada huo.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2011/2012

Katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Ofisi hii imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuratibu mipango ya maendeleo ya Ofisi Kuu Pemba.

ii. Kusimamia na kuimarisha utekelezaji wa shughuli za Ofisi Kuu Pemba.

iii. Kuibua muamko wa kupunguza maambukizi mapya ya virusi vya ukimwi na kuratibu shughuli mtambuka za Ofisi Kuu Pemba.

iv. Kusimamia upatikanaji wa nafasi za masomo na mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu kwa watumishi wa Ofisi Kuu Pemba ili kuwa na wafanyakazi watakaokuwa na ujuzi na uwezo katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

v. Kufanya tathmini ya utendaji kazi kwa watendaji wa Ofisi kuu Pemba ili kuongeza ari ya kufanyakazi na kuhakikisha haki na mafao ya wafanyakazi yanapatikana kwa wakati.

vi. Kukamilisha ujenzi wa uzio wa kituo cha TVZ Pemba.

Mhe. Spika, ili Ofisi Kuu ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo Pemba iweze kutekeleza malengo yake kwa ufanisi, naomba Baraza lako tukufu liidhinishe shilingi 493,900,000 kwa kazi za kawaida, kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012.

SEKTA YA HABARI

Mhe. Spika, sekta ya Habari imeundwa na taasisi tano, Shirika la Utangazaji Zanzibar ambalo linaundwa na Sauti ya Tanzania Zanzibar na Televisheni Zanzibar, Idara ya Habari Maelezo, Shirika la Magazeti ya Serikali, Tume ya Utangazaji na Chuo cha Uandishi wa Habari. Majukumu ya Msingi ya taasisi hizi ni kuarifu, kuelimisha na kuburudisha jamii, kuratibu uchapishaji wa magazeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kusimamia vyombo vya utangazaji vya Serikali na vya binafsi na kutoa taaluma kwa waandishi wa habari. Malengo ya sekta ya habari ya mwaka 2011/2012 kwa kila taasisi ni kama ifuatavyo:-

SHIRIKA LA UTANGAZAJI

Mhe. Spika, Shirika hili limeundwa baada ya Serikali ya Awamu ya Saba kuamua kuziunganisha shughuli za matangazo ya Televisheni na Redio zinazosimamiwa na Serikali. Majukumu ya msingi ya Shirika ni kutoa habari, kuelimisha, kuburudisha na kuhamasisha jamii juu ya masuala ya kiuchumi,

kijamii na kisiasa. Kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011 Shirika hili (Sauti ya Tanzania Zanzibar na Televisheni Zanzibar) lilijipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuimarisha usambazaji wa habari kwa kufungua Ofisi Dar es Salaam.

ii. Kununua vifaa vya kisasa vinavyotumia Teknolojia ya Dijital katika kuimarisha shughuli za utangazaji Zanzibar.

iii. Kuendeleza kufanya vipindi mbali mbali vya kuelimisha, kupasha habari pamoja na kuburudisha jamii.

iv. Kuwapatia wafanyakazi wa sehemu ya ufundi elimu ya teknolojia ya "Digital" ili kwenda sambamba na vifaa vya teknolojia hiyo ya kisasa.

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Spika, Shirika la Utangazaji (Sauti ya Tanzania Zanzibar na Televisheni Zanzibar) limefanikiwa kutekeleza malengo hayo kama ifuatavyo:-

i. Shirika limeshafungua ofisi yake katika Jengo la Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo Zanzibar lililopo Magogoni Dar es Salaam. Ofisi hiyo imefanikiwa kupata ufadhili kutoka Shirika la Bima Zanzibar linalodhamini urushaji wa kipindi cha kutoka magazetini kila siku asubuhi.

ii. Shirika tayari limepata vifaa vya matangazo ya digital vitakavyofungwa Unguja na Pemba ambapo baada ya kufungwa vifaa hivyo, matagazo ya TVZ yataonekana Zanzibar nzima.

iii. Jumla ya vipindi vya taaluma visivyopungua 140, habari, vya kuburudisha jamii vimetayarishwa na kurushwa hewani kupitia shirika hili.

iv. Kwa hatua ya awali semina zilifanywa juu ya teknolojia ya "*Digital*" kwa wafanyakazi na wadau wa shughuli za habari katika Kituo cha *TVZ* na sehemu nyengine.

MALENGO KWA MWAKA FEDHA 2011/2012

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Shirika la Utangazaji limepanga kutekeleza malengo makuu yafuatayo:-

i. Kuimarisha ubora wa matangazo yake ili kuweza kuvutia wasikilizaji, watazamaji wengi na wafanyabiashara wa ndani na nje ya Zanzibar.

ii. Kuimarisha uwezo wa waandishi wa habari, mafundi mitambo na wafanyakazi kwa kukuza ubora wa habari na vipindi.

iii. Kukarabati Mnara wa mawimbi mafupi (*short waves*) kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China.

iv. Kuanza majaribio ya urushaji wa matangazo kwa kutumia teknolojia ya *digital*.

v. Kuanzisha utaratibu wa kupasha habari kwa njia ya ishara ili kuwapatia fursa ya kupata habari watu wenye mahitaji maalumu (Wasiosikia na wasioweza kusema)

Mhe. Spika, ili kuliwezesha shirika hili kutekeleza malengo liliyojipangia katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya shilingi 642,400,000/= kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida za kuendeshea matangazo ya televisheni na kukusanya jumla ya sh. 80,000,000/= kwa ajili ya kuchangia katika mfuko wa Serikali. Aidha, jumla ya shilingi 541,000,000/= kwa kazi za kawaida za kuendeshea matangazo ya redio na jumla ya sh. 2,440,000,000/= kwa kazi za maendeleo kati ya hizo Shs. 40,000,000/= ni mchango wa Serikali na Shs. 2,400,000,000/= msaada kutoka Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China. Sauti ya Tanzania Zanzibar imepanga kukusanya jumla ya Shs. 80,000,000/= kwa ajili ya kuchangia katika mfuko wa Serikali.

IDARA YA HABARI MAELEZO

Mhe. Spika, jukumu kuu la Idara ya Habari Maelezo ni kutoa elimu za maendeleo mjini na vijijini pamoja na kujenga uhusiano mzuri kati ya Serikali na taasisi mbali mbali za ndani na nje ya nchi. Idara pia ina wajibu wa kutayarisha na kutoa vielelezo katika mfumo wa picha, sinema, habari na majarida kuhusu shughuli za Serikali na kusimamia sheria ya habari Zanzibar. Katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, idara hii ilipanga kutekeleza malengo makuu yafuatayo:-

i. Kujenga mazingira mazuri ya kutoa Habari mjini na vijijini kupitia njia ya sinema
kwa kuelimisha jamii juu ya maambukizi ya *HIV* na ukimwi, jinsia, mazingira, kupinga ajira kwa watoto na kupambana na umasikini.

ii. Kuelimisha jamii juu ya uhuru wa Vyombo vya Habari kwa kutumia sheria iliyopo.

iii. Kuifanyia marekebisho sheria Nam. 5 ya mwaka 1988 ya usajili wa magazeti, vitabu na wakala wa habari na maandalizi ya kuanzisha sheria mpya ya uhuru wa vyombo vya habari Zanzibar.

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha uliopita idara ilisimamia, vyombo vya habari kushiriki katika shughuli za uchaguzi mkuu na kutoa habari, kutayarisha makala, kutoa mafunzo ya elimu ya upigaji kura, kutangaza sera za vyama na wagombea mbali mbali na kushajiisha jamii kushiriki katika uchaguzi mkuu kwa njia ya salama na amani.

Mhe. Spika, pamoja na utekelezaji huo idara hii pia ilifanikiwa kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Imeweza kuuza picha 180 za Rais wa Jamhuri ya Muungano, Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete na picha 980 za Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein katika taasisi za Serikali na za Binafsi.

ii. Imeweza kufanya ukarabati mkubwa wa jengo lake liliopo Rahaleo na kuweza kuipatia vitendea kazi vikiwemo kompyuta 5 pamoja na kuweka huduma ya intaneti.

iii. Imeweza kuonesha sinema vijijini kwa ajili ya kutoa elimu juu ya mwenendo na matumizi ya vyombo vya habari katika kutekeleza dhana ya utawala bora pamoja na elimu za maendeleo ya vijana na uhamasishaji wa kupunguza maambukizi mapya ya *VVU*. (Angalia kiambatanisho namba 6)

iv. Imetayarisha jumla ya vipindi 16 vinavyohusiana na sheria ya uhuru wa vyombo vya habari na kurushwa hewani kati ya hivyo 6 vimerushwa TV na 10 Redio pamoja na kufanya

semina kwa wadau wa vyombo vya habari. Aidha, imeweza kuendesha vikao 20 vya mikutano ya waandishi wa habari (*press conference*).

v. Imeweza kutoa na kusambaza taarifa 94 (makala) kupitia magazeti ya Nipashe, Jambo leo, Mwananchi, Habari Leo, Zanzibar Leo, *Daily News*, Mtanzania na Uhuru na kwa upande wa redio ni Redio Uhuru, Mlimani, Kheir, *Clouds*, Tumaini, Free Afrika, *Zenj FM*, *Alnoor* na *Hits FM*, STZ, pia redio za kiswahili za nchi za nje ikiwemo Redio China, Iran, *Deutch welle* na Redio Ufaransa. Aidha, kwa upande wa intaneti imeweza kutoa na kusambaza taarifa 50 kwa kupitia blog ya Shangwe, Issa Michuzi na Mzalendo.

MALENGO KWA MWAKA FEDHA 2011/2012

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, idara hii imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuratibu shughuli za vyombo vya habari nje na ndani vinavyofanya kazi Zanzibar.

ii. Kukuza usambazaji wa habari za maendeleo mjini na vijijini kwa kutumia gari la Sinema, zikiwemo kupunguza umaskini, maambukizi ya ukimwi, jinsia, mazingira na utumikishwaji wa watoto.

iii. Kuimarisha uwezo wa waandishi wa habari na wafanyakazi kwa kuimarisha Sekta ya Habari.

iv. Kuimarisha idara kwa kukamilisha ukarabati wa jengo na kulipatia vitendea kazi.

Mhe. Spika, ili Idara ya Habari Maelezo iweze kutekeleza malengo yake katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, naomba Baraza lako tukufu liidhinishe shilingi 200,000,000/= kwa kazi za kawaida na makusanyo ya Shilingi 7,800,000/= kwa ajili ya kuchangia katika mfuko wa Serikali.

SHIRIKA LA MAGAZETI YA SERIKALI

Mhe. Spika, majukumu ya msingi ya Shirika la Magazeti ya Serikali ni kusimamia uchapishaji wa magazeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kuelimisha wananchi ili kukuza uelewa wao wa mambo, na kutoa habari zenye

kuhamasisha kushiriki kwenye harakati za maendeleo ya nchi. Katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, Shirika la Magazeti ya Serikali lilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kukuza ubora na idadi ya magazeti yanayotolewa na Shirika la Magazeti ya Serikali na kupanua maeneo ya usambazaji Unguja, Pemba na Tanzania Bara ili kukabiliana na ushindani wa soko.

ii. Kuwaelimisha na kuwapatia wananchi taarifa mbalimbali zinazohusu maendeleo.

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Spika, napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kuwa Shirika limefanikiwa kutoa magazeti ya rangi ya Zanzibar Leo kuanzia tarehe 1 Septemba, 2010, lengo ni kuongeza idadi ya wasomaji na kuweza kuingia kwenye ushindani wa kibiashara. Aidha, Shirika la Magazeti ya Serikali limefanikiwa kutekeleza yafuatayo:-

i. Kuongezeka kwa sehemu za usambazaji wa magazeti yakiwemo maeneo mengi ya visiwa vya Unguja na Pemba na baadhi ya Mikoa huko Tanzania Bara. Aidha, Shirika limeamua kusambaza magazeti katika baadhi ya vijiji vya Unguja na Pemba kwa kupitia maskuli, ikiwa ni juhudi ya kulitangaza na kulijengea soko zaidi, pamoja na kuwajengea wananchi utamaduni wa kupenda kusoma magazeti. Miongoni mwa skuli hizo kwa upande wa Unguja ni Chwaka, Pongwe, Uroa na Matemwe na kwa upande wa Pemba ni Chambani, Uweleni, Mkanyageni, Michenzani, Dimbani, Pujini, Makombeni na Chokocho. Pia usambazaji wa taarifa za magazeti ya Shirika unafanywa kupitia vituo vya TV na Radio za Zanzibar na Tanzania Bara na kwenye mtandao.

ii. Shirika limeweza kuongeza kurasa za Magazeti ya Zanzibar Leo kutoka 12 hadi 16, idadi ya makala, habari na taarifa zinazochapishwa katika Gazeti hilo zimeongezeka kwa kiasi kikubwa, pamoja na kuwepo makala maalumu kulingana na siku.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2011/2012

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Shirika la Magazeti ya Serikali limepanga kutekeleza malengo makuu yafuatayo:-

i. Kuhakikisha gazeti linawafikia wasomaji Zanzibar nzima na maeneo zaidi ya Tanzania Bara.

ii. Kukuza uwezo wa waandishi wa habari wa magazeti na wafanyakazi kwa ajili ya kuongeza ubora wa makala, habari na matukio.

iii. Kuongeza ubora wa magazeti ili kuzidi kuingia katika ushindani wa masoko kwa kukuza mapato ya Serikali.

Mhe. Spika, ili Shirika la Magazeti ya Serikali liweze kutekeleza malengo hayo, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha shilingi 815, 000,000/= kwa kazi za kawaida kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

TUME YA UTANGAZAJI

Mhe. Spika, majukumu ya msingi ya Tume ya Utangazaji ni kusimamia vyombo vya utangazaji vya Serikali na vya binafsi vinavyoanzishwa nchini. Katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, Tume ya Utangazaji ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kusimamia majaribio ya urushaji wa matangazo kwa kutumia mfumo wa teknolojia ya *digital*.

iii. Kuendeleza, kuelimisha na kuratibu urushaji wa matangazo kwa kutumia mfumo wa teknolojia ya *digital* hadi kufikia kiwango kinachotakiwa.

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, Tume ya Utangazaji imefanikiwa kutekeleza malengo hayo kama yafuatayo:-

i. Katika kusimamia majaribio ya urushaji wa matangazo kwa kutumia mfumo wa teknolojia ya *digital*, Tume imetoa vibali vya kuanzisha vituo vya televisheni vya *digital* kwa wawekezaji wanne (4) wa ndani. (angalia kiambatanisho namba 7).

ii. Imeendesha vipindi vya redio, kutoa taaluma juu ya teknolojia ya utangazaji ya dijitali. Jumla ya vipindi nane (8) vimeendeshwa (kurushwa hewani) katika idhaa ya Sauti ya Tanzania Zanzibar. Aidha, kwa kushirikiana na *UNDP* imeandaa mafunzo juu ya njia bora za kutayarisha vipindi vyenye maudhui ya ndani vyenye kuamsha ari ya kupambana na umaskini na kuleta maendeleo, kwa watendaji wa vyombo vya habari na utangazaji vya Zanzibar. Vile vile Jumla ya semina nne (4) zimefanyika juu ya mada zenye mwelekeo wa utayarishaji wa vipindi bora vyenye maudhui mbali mbali.

Mhe. Spika, Tume ya Utangazaji Zanzibar pia imefanikiwa kupata uanachama wa Jumuiya ya Mawasilino ya Afrika Mashariki (*East African Communication Organization - EACO*) bila ya kupitia Tanzania Bara kuanzia mwezi Aprili, 2011. Miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana kwa kipindi hicho ni pamoja na kuwa na muongozo wa pamoja wa matumizi wa ving'amuzi vya *digital* kwa nchi zote za Afrika Mashariki.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2011/2012

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Tume ya Utangazaji imepanga kutekeleza malengo makuu yafuatayo:-

i. Kuandaa utaratibu wa kupunguza uingizaji nchini vifaa vya analogi na jinsi ya kudhibiti taka taka za vifaa hivyo.

ii. Kuratibu shughuli za Utangazaji nchini kwa kutoa huduma bora za utangazaji ili zisiingiliane baina ya watumiaji.

iii. Kujenga uelewa kwa vyombo vya utangazaji vya Serikali na watu binafsi juu ya maadili ya utangazaji.

Mhe. Spika, ili kukamilisha vyema malengo iliyojipangia katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha shilingi 160,000,000/= kwa kazi za kawaida na makusanyo ya shilingi 16,000,000/= kwa ajili ya kuchangia katika Mfuko wa Serikali.

CHUO CHA UANDISHI WA HABARI

Mhe. Spika, majukumu ya msingi ya Chuo cha Uandishi wa Habari ni kutoa mafunzo kwa wanafunzi wanaochukua taaluma ya uandishi wa habari kwa

ngazi ya Cheti na Stashahada. Katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, chuo kilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuendelea na usajili wa wanafunzi wapya wa ngazi ya Stashahada na Cheti pamoja na kuanzisha programu maalumu za mafunzo ya muda mfupi.

ii. Kuendelea kukuza uhusiano na kukitangaza chuo kwa taasisi mbali mbali za ndani na nje ya nchi.

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, Chuo cha Uandishi wa Habari kilifanikiwa kutekeleza malengo hayo kama ifuatavyo:-

i. Chuo kimeongeza usajili wa idadi ya wanafunzi wapya kutoka 75 mwaka 2009/2010 hadi kufikia 122 kwa mwaka wa masomo 2010/2011. Kati ya wanafunzi hao 80 ni wa Diploma wakiwemo wanaume 28 na wanawake 52. Wanafunzi wa Cheti ni 42 kati yao wanaume ni 12 na wanawake ni 30.

ii. Chuo kimeendelea kujitangaza kwa kusambaza maombi ya mashirikiano kwa Vyuo ndani na nje ya nchi. Aidha, ushirikiano kati ya China na Chuo umeimarishwa ambapo Somo la Lugha ya Kichina limeanza kufundishwa rasmi Chuoni humo.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2011/2012

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Chuo cha Uandishi wa Habari kimepanga kutekeleza malengo makuu yafuatayo:-

i. Kuwa na mtaala bora wa chuo ili kuimarisha ubora wa kiwango cha taaluma ya habari utakaoendana na mageuzi ya teknojia ya habari duniani.

ii. Kukiimarisha chuo kwa kukipatia vifaa vya kufundishia kwa njia ya vitendo na kukipatia walimu wenye sifa.

Mhe. Spika, ili kukamilisha vyema malengo ya Chuo cha Uandishi wa Habari katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya shilingi 290,000,000/=.

SEKTA YA UTALII

Mhe. Spika, Sekta ya Utalii inajumuisha Kamisheni ya Utalii, Chuo cha Maendeleo ya
Utalii, Shirika la Utalii na Hoteli ya Bwawani. Taasisi hizi zimepewa jukumu la kupanga, kusimamia, kuendeleza Utalii na kuitangaza Zanzibar ili Sekta hii iende sambamba na Sera na mikakati ya Serikali katika kufikia malengo makuu ya kuimarisha uchumi wa Taifa na kupunguza umasikini.

MALENGO YA SEKTA YA UTALII KWA MWAKA 2010/2011

KAMISHENI YA UTALII

Mhe. Spika, jukumu la msingi la Kamisheni ya Utalii Zanzibar ni kupanga, kusimamia na kuendeleza shughuli za Utalii ndani na nje ya nchi. Katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, Kamisheni imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuendelea kuitangaza Zanzibar ndani na nje ya nchi kwa kushiriki maonesho ya kitalii na mikutano ya kimataifa.

ii. Kushajiisha uandaaji wa michezo mbali mbali ya kitalii ikiwemo tamasha la Mzanzibari, Mwaka Kogwa, Marathon, Triathlon, Mountain Bike, Tamasha la Filamu la Nchi za Majahazi, Sauti za Busara na Siku ya Utalii Duniani.

ii. Kuchapisha kalenda (*scroll wall callenders*), kuendeleza jarida la Karibu Zanzibar na kuchapisha muongozo wa nchi na kutoa *DVD* zinazoonesha vivutio vya utalii.

iii. Kuendelea na utafiti wa utokaji wa wageni (*Tourism Sector Survey*) kwa kushirikiana na Idara ya Takwimu, Benki Kuu ya Tanzania, Wizara ya Maliasili na Utalii (Bara) ili kujua mapato halisi ya wageni wanoingia nchini.

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Spika, Kamisheni ya Utalii kwa mwaka wa fedha 2010/2011 imefanikiwa kutekeleza malengo yake kama ifuatavyo:

i. Kushiriki katika maonesho (9) ya Utalii yakiwemo *WTM* London ambayo ndio

maonesho makubwa duniani *ITB* Berlin, MAP Ufaransa, *BIT Milan, ATM-INDABA, ATM- Dubai, TUR*, Sweden, karibu - Arusha na maonesho ya biashara ya Saba Saba Dar-es-Salaam. Na kupata fursa ya kutoa taarifa kwa wageni juu ya vivutio vya Utalii wa Zanzibar.

ii. Kufanikisha sherehe ya siku ya Utalii duniani 2010 kisiwani Pemba, kwa nia ya kuifufua michezo ya asili kama vile mchezo wa ng'ombe na resi za ngalawa. Aidha, tamasha la Filamu la Nchi za Jahazi, Sauti za Busara na sherehe za Mwaka Kogwa zimefanyika kwa ajili ya kukuza utalii unaolinda mila na utamaduni wa Mzanzibari.

iii. Katika kufufua michezo ya marathon, kumefanyika mazungumzo ya awali baina ya Kamisheni na wanaotaka kufadhili mchezo huo kutoka kampuni ya *DISALVAMENTO* kutoka nchini Italy.

iv. Kufanikisha uchapishaji wa "*Scroll wall Calenders"* - (Kalenda za ukutani) 5000 kwa mwaka 2011, nakala 5000 za *DVD* inayoonesha vivutio vya utalii vya Zanzíbar, muungozo wa ndani na huduma za malazi *'Country directory* na *Accommodation Guide'* zimekamilika na hivi sasa zipo katika hatua ya uchapishaji.

v. Utafiti wa utokaji wa wageni kwa mwaka 2010 umekamilika na ripoti ya utafiti huo kwa mwaka 2008 tayari imeshatolewa kwa ajili ya kutumiwa na jamii.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2011/2012

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Kamisheni ya Utalii imepanga kutekeleza malengo makuu yafuatayo:-

i. Kukuza idadi na ubora wa huduma za watalii Zanzibar.

ii. Kuimarisha uhusiano wa Sekta ya Utalii na taasisi nyengine.

Iii Kukuza, kueneza na kutangaza Utalii wa Zanzibar Kitaifa na Kimataifa.

iv. Kukuza shughuli za utalii ili kuwa endelevu kwa maendeleo ya kiuchumi, kijamii na mazingira nchini.

v. Kuanzisha mfumo wa ukusanyaji wa takwimu utakaotumia *"t-start software"*.

Mhe. Spika, ili Kamisheni iweze kutekeleza malengo yake, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe matumizi ya shilingi 809,000,000 kwa kazi za kawaida kwa mwaka wa fedha 2011/2012 na kukusanya Tsh 842,000,000/= kwa ajili ya kuchangia katika mfuko mkuu wa Serekali.

CHUO CHA MAENDELEO YA UTALII ZANZIBAR

Mhe. Spika, jukumu la msingi la Chuo cha Maendeleo ya Utalii Zanzibar ni kutoa taaluma itakayowezesha kujenga rasilimali watu wenye ujuzi, utaalamu na stadi zinazohitajika na kukubalika katika viwango vya kimataifa ili kuimarisha sekta ya Utalii Zanzibar. Katika mwaka wa fedha 2010/2011 Chuo cha Maendeleo ya Utalii Zanzibar kilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuimarisha miundo mbinu ya chuo ili kuweka mazingira mazuri ya kujifunzia na ufundishaji.

ii. Kuimarisha hali ya taaluma ili iweze kuendana na mahitaji halisi kwa mujibu wa viwango vinavyokubalika kitaifa na kimataifa.

iii. Kufikisha huduma za kitalii kwa jamii ili kuijengea jamii uelewa mzuri wa shughuli za kitalii hapa Zanzibar, na waweze kuzitumia katika kuimarisha hali zao za maisha na kiuchumi.

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, Chuo cha Maendeleo ya Utalii kimefanikiwa kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Chuo kimekamilisha ukarabati wa jiko na mkahawa na kwa sasa anasubiriwa mtaalamu kuja kupanga "*setting"* ya vifaa vya jikoni.

ii. Mchakato wa ujenzi wa jengo jipya la mradi wa chuo umeshaanza baada ya kukamilika kwa mchoro na shughuli inayoendelea sasa ni kutafuta mjenzi kwa njia ya zabuni. Hii ni

hatua ya kuimarisha miundo mbinu ya chuo yenye lengo la kuongeza idadi ya madarasa, ofisi za wafanyakazi na maktaba.

iii. Kufuatia mazungumzo na Benki ya Maendeleo ya Afrika (*ADB*) tunatarajia ifikapo Julai, 2012 kuidhinishiwa jumla ya Dola za Kimarekani Milioni nane (8) kwa ajili ya kujenga jengo la ghorofa tatu na kununua samani, vifaa vya kutolea huduma na kukuza kiwango cha utaalamu kwa walimu na maafisa wa vitengo waliopo katika chuo hiki. Pia jengo hilo litakuwa na kituo cha kulelea wajasiriamali (*bussness incubator*).

iv. Chuo kimeweza kuajiri walimu wapya sita (6) ngazi ya digirii ya kwanza katika fani za Utalii, Uongozi, Sheria, Vyakula na Vinywaji; pamoja na teknolojia ya Habari na Mawasiliano.

v. Mapitio ya awali kwa mitaala ya Chuo yamefanyika. Chuo kimechukua baadhi ya
mawazo kutoka katika vyuo vinavyotumia mitaala ya kitaifa chini ya NACTE. Aidha, kimeingiza baadhi ya kozi kutoka mitaala ya Shirikisho la taasisi za taaluma ya utalii la Uingereza (*Confederation of Tourism and Hospitality - CTH* kwa daraja la diploma ya juu). Chuo cha Maendeleo ya Utalii cha Zanzibar kimejiunga na shirikisho hilo.

Mhe. Spika, mwishoni mwa mwezi wa June, 2011, Chuo kimepata usajili rasmi wa muda wa miaka 2 wa *NACTE* ambapo baada ya kukamilika masharti yaliyobaki usajili wa kudumu utapatikana.

MALENGO KWA MWAKA 2011/2012

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Chuo cha Maendeleo ya Utalii kimepanga kutekeleza malengo makuu yafuatayo:-

i Kuwa na mtaala bora wa chuo ili kuimarisha ubora wa kiwango cha elimu ya utalii utakaoendana na soko la utalii.

ii Chuo kuwa na vifaa vya kisasa vya kufundishia na walimu wenye sifa.

iii Kufanya ukarabati wa miundombinu ya Chuo cha Maendeleo ya Utalii.

Mhe. Spika, ili chuo kiweze kutekeleza malengo yake, naliomba Baraza lako tukufu matumizi ya shilingi 400,000,000 kwa kazi za kawaida na shilingi 400,000,000 kwa kazi za maendeleo kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

SHIRIKA LA UTALII

Mhe. Spika, majukumu ya msingi ya shirika ni kutoa huduma za usafirishaji na utembezaji wa watalii katika vivutio vya kitalii vilioko Zanzibar, na kuhudumia meli za kitalii zinazoleta watalii nchini. Katika mwaka wa fedha 201O/2011, Shirika la Utalii lilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i Kuendeleza juhudi za kutafuta ufadhili wa kulifanyia ukarabati Jengo la Livingstone ili liweze kutumika kibiashara kwa lengo la kuliongezea shirika mapato.

ii. Kuingia katika ushindani wa kibiashara ya utalii inayokua kwa kasi nchini.

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Spika, Katika mwaka wa fedha wa 2010/201, Shirika la Utalii limefanikiwa kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Hatua za kuwasiliana na vyombo vya ndani na nje zimefanyika ikiwa ni pamoja na kampuni ya *"Royal Institution of Charter Surveyor"* ya Uingereza katika juhudi za kutaka kulifanyia matengenezo jengo la Livingstone.

ii. Kufanyika kwa mazungumzo na uongozi wa Meli ya *"PC Oceani Mist"* ya nchini Kenya kwa ajili ya kuleta wageni kwa njia ya pwani kuja kutembea Zanzibar. Meli hiyo *PC Oceani Mist* imefika Unguja Disemba, 2010 kwa majaribio na itaendelea kuleta wageni mwaka huu wa fedha utakapoanza msimu wa wageni.

iii. Kufanya utafiti wa kuangalia uwezo wa shirika kujiendesha kibiashara, timu ya wataalamu wanne (4) walipewa jukumu hilo. Ripoti ya utafiti huo imeshawasilishwa Wizarani kwa mazingatio.

MALENGO KWA MWAKA 2011/2012

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Shirika la Utalii imepanga kutekeleza malengo makuu yafuatayo:-

i. Kuimarisha hudhuma za biashara kwa watalii wanokuja kwa njia ya bahari (*cruise tourism).*

ii. Kuongoza utoaji wa huduma bora kwa watalii watakaoshughulikiwa na Shirika (*package tourism*).

iii. Kuanzisha vyanzo vipya vya mapato kwa kuchochea kuibuliwa kwa utalii wa ndani kwa kuzitumia nyumba za shirika zilizopo Makunduchi na Jambiani. Aidha, kutafuta wawekezaji watakaoingia ubia na Shirika katika kuyatumia maeneo yalioko Kuji na Vitongoji Pemba.

Mhe. Spika, ili shirika liweze kutekeleza malengo yake, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe matumizi ya shilingi 245,440,000/= kwa kazi za kawaida kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

HOTELI YA BWAWANI

Mhe. Spika, jukumu la hoteli ni kutoa huduma za malazi na chakula kwa wageni na wenyeji wanaotembelea Hoteli. Aidha, hutoa huduma za kumbi kwa ajili ya sherehe mbali mbali za kitaifa na kijamii. Katika mwaka wa fedha 2010/2011, Hoteli ya Bwawani ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuinua kiwango cha utendaji wa kazi huku mkazo zaidi ikiwa ni kuwajengea uwezo wafanyakazi wake kwa kuwapatia mafunzo.

ii. Kuendelea na mipango yake ya matengenezo ya vyumba vya kulala wageni, kumbi tatu za mikutano na miundo mbinu mengine.

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, Hoteli ya Bwawani imefanikiwa kutekeleza malengo yafuatayo:

i. Imeweza kuwapatia mafunzo wafanyakazi wake watano katika fani mbali mbali, Mafunzo ya Hoteli na Utalii wafanyakazi

wawili (2), Utawala mfanyakazi mmoja (1), Afisa Manunuzi mfanyakazi mmoja (1) na *Computer* mfanyakazi mmoja (1).

ii. Hoteli imeweza kuvifanyia matengenezo vyumba 6 na paa la Ukumbi wa Salama. Pia imeweza kununua samani mpya na kuwekwa katika kumbi zake mbili za Pemba Bar juu na ukumbi wa Salama.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2011/2012

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Hoteli ya Bwawani imepanga kutekeleza malengo makuu yafuatayo:

i. Kuwa na miundombinu bora na ya kisasa kwa huduma bora za hoteli kwa kuendelea kufanya matengenezo ya vyumba, kumbi za mikutano na miundombinu mengine.

ii. Kuwa na wafanyakazi wenye ufanisi mkubwa wa kazi kwa kuwajengea uwezo na kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi.

iii. Kutatua tatizo la mmong'onyoko wa ardhi kwenye kingo za hoteli zinazosababishwa na mawimbi makali ya bahari kwa kushirikiana na mamlaka husika.

Mhe. Spika, ili hoteli iweze kutekeleza malengo yake naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha matumizi ya shilingi 800,000,000 kwa kazi za kawaida kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

KAMISHENI YA UTAMADUNI NA MICHEZO

Mhe. Spika, Kamisheni ya Utamaduni na Michezo imeundwa na Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale, Baraza la Kiswahili, Baraza la Sanaa, Bodi ya Sensa ya Filamu na Sanaa za maonesho, kituo cha *EACROTANAL* na Baraza la Taifa la Michezo. Taasisi hizi zimepewa jukumu la kusimamia, kuratibu, kufufua, kuendeleza na kudumisha shughuli zote za Utamaduni na Michezo Zanzibar.

MALENGO YA KAMISHENI YA UTAMADUNI NA MICHEZO KWA MWAKA 2010/2011

Mhe. Spika, Kamisheni ya Utamaduni na Michezo iliundwa baada ya Serikali kuamua kuziweka pamoja shughuli za Michezo na Utamaduni. Majukumu ya msingi ya Kamisheni hii ni kuratibu na kusimamia maendeleo ya utamaduni na michezo hapa Zanzibar kwa kushirikiana na Idara na Mabaraza yaliyo chini yake. Katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, Kamisheni iliyoundwa kutekeleza shughuli zilizokuwa zikisimamiwa na Idara ya Utamaduni na Idara ya Michezo ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kufanya utafiti wa urithi wa utamaduni wa majina ya miji na mitaa ya Zanzibar kwa kutumia taarifa za mchoro wa ramani ya urithi wa utamaduni zilizokusanywa katika Wilaya za Zanzibar.

ii. Kuendelea kutekeleza Sera ya Utamaduni Zanzibar kwa kuelimisha jamii kuhusu utamaduni wetu kupitia matamasha ya utamaduni, vipindi vya redio, televisheni na vipeperushi na kusimamia utekelezaji wake.

iii. Kuandaa na kushiriki michezo ya kimataifa kwa lengo la kuwapa nafasi wachezaji chipukizi kushiriki vizuri kwenye mashindano ya kitaifa na kimataifa.

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2010/201, Kamisheni ya Utamaduni na Michezo imetekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kamisheni ya Utamaduni imefanya marekebisho ya baadhi ya takwimu zilizokuwemo katika mchoro wa ramani ya urithi wa utamaduni Pemba. Aidha, Kamisheni imefanya semina kwa maafisa wa Utamaduni wa Wilaya na Mikoa kwa Unguja lengo ni kuwaelewesha juu ya dhana nzima ya utafiti.

ii. Imefanikisha kufanyika kwa Tamasha la Utamaduni wa Mzanzibari kwa Unguja na Pemba.

iii. Timu ya *Zanzibar Heroes* ya mpira wa miguu ilishiriki katika mashindano ya *"Tusker Tanzania Senior Challenge Cup"* yaliyofanyika Dar es Salaam na Zanzibar ilifanikiwa kufikia robo fainali.

iv. Aidha, timu za vijana chini ya umri wa miaka 12 - 13 na chini ya umri wa miaka 14 - 15 ya mpira wa miguu imeshiriki katika mashindano ya vituo ya Akademia ya Michezo (*Olympafrica Centres*) vya Afrika Mashariki na Kati nchini Burundi na timu ya chini umri wa miaka 14-15 kufanikiwa kuwa bingwa kwa kushika nafasi ya kwanza na kutunukiwa kombe lijulikanalo kwa jina la *"Daimler Cup 2010/2011"*.

v. Mashindano ya kuinua vipaji vya wanamichezo yamefanyika na msisitizo umetolewa wa kuanzishwa timu za watoto na vijana.

vi. Imeweza kuzisaidia timu ya mpira wa miguu kushiriki katika mashindano ya klabu bingwa na kombe la washindi Barani Afrika.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2011/2012

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Kamisheni ya Utamaduni na Michezo imepanga kutekeleza malengo makuu yafuatayo:-

i. Kujenga studio ya kisasa ya kurikodia michezo ya kuigiza na muziki.

ii. Kushajiisha na kuendeleza maendeleo ya vikundi vya Utamaduni kwa vijana katika wilaya, mikoa na Taifa.

iii. Kulinda na kuendeleza urithi wa utamaduni kama jukumu la mwananchi.

iv. Kuziwezesha timu kushiriki michezo ya kimataifa kwa lengo la kuwapa nafasi wachezaji chipukizi kushiriki vizuri kwenye mashindano ya kitaifa na kimataifa.

v. Kusimamia na kushajiisha kufanyika mashindano ya mawizara na Mashirika ya Serikali kwa michezo mbali mbali.

vi. Kusimamia uanzishaji wa viwanja vya michezo vya wilaya kwa kushirikiana na ofisi za wilaya zinazohusika.

Mhe. Spika, ili Kamisheni ya Utamaduni na Michezo iweze kutekeleza malengo yake, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe Shilingi 564,600,000/= kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na Shilingi

120,000,000 kwa ajili ya kazi za maendeleo kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012 na makusanyo ya Shilingi 17,000,000 kwa ajili ya kuchangia katika Mfuko wa Serikali.

IDARA YA MAKUMBUSHO NA MAMBO YA KALE

Mhe. Spika, majukumu ya msingi ya Idara hii ni kuenzi, kuhifadhi na kuendeleza historia ya Zanzibar kwa kutumia makumbusho, magofu na mambo ya kale. Aidha, kuelimisha jamii juu ya umuhimu na faida za matumizi ya makumbusho na mambo ya kale. Katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, idara ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kufanya utafiti wa Kiakiolojia katika maeneo ya kihistoria.

ii Kuimarisha majengo yenye kuonesha historia ya Zanzibar.

iii. Kufanya utanuzi wa maonesho (*exhibitions*) katika makumbusho.

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale imetekeleza malengo yafuatayo:-

i. Utafiti wa uchimbaji wa Ngome ya Mazrui Chwaka, Tumbe ulifanyika kwa ufadhili wa *MACEMP*/*DAMA* pamoja na utafiti wa Kiakiolojia katika eneo la Ngome Kongwe, Forodhani na Unguja Ukuu, chini ya udhamini wa *'African Archaeology Network'* na *DAMA*. Katika uchimbaji huo kuligunduliwa vigae vya vyungu, '*Kwale pottery*' vya karne ya kwanza. Aidha, tafiti hizo zilihusisha visiwa vidogo vidogo kama Pungume, Chumbe, Fundo na Funzi na utafiti katika Kisiwa cha Kwale.

ii. Kufanikiwa kufanya ukarabati wa mahandaki yaliotumiwa na Askari wa Kiingereza katika vita ya pili ya Dunia na Ujenzi wa ngazi ya 'Mnara wa Kumbukumbu ya vita vya pili vya Dunia huko Mangapwani. Aidha, Ukarabati wa Makaburi na Misikiti ya kale ya Mazrui, Chwaka, Tumbe, Mkia wa Ng'ombe na Msuka Mjini chini ya ufadhili wa *"Millenium Challenge Project"*.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2011/2012

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale imepanga kutekeleza malengo makuu yafuatayo:-

i. Kuyaimarisha makumbusho na mambo ya kale na kushajiisha jamii kuwa na muamko wa kuyatembelea kwa ajili ya kufahamu umuhimu na matumizi yake.

ii. Kuanzisha makumbusho ya mkoa katika maeneo muhimu ya kihistoria na kuhimiza jamii kuanzisha makumbusho ya kijamii katika maeneo yao.

Mhe. Spika, ili Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale iweze kutekeleza malengo yake ipasavyo, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe shilingi 300,760,000/= kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012 na makusanyo ya Shilingi 170,000,000/= kwa ajili ya kuchangia katika Mfuko wa Serikali.

BARAZA LA KISWAHILI:

Mhe. Spika, majukumu ya msingi ya Baraza la Kiswahili la Zanzibar ni kukuza, kushajiisha na kufuatilia matumizi na maendeleo ya Kiswahili ndani na nje ya Zanzibar. Katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, Baraza hili lilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kukiendeleza Kiswahili kwa kuwashajiisha wasanii wa sanaa za uandishi, kushiriki mashindano ya uandishi wa mashairi, tenzi, hadithi na insha.

ii. Kushajiisha na kukuza matumizi ya lugha ya Kiswahili fasaha kitaifa na kimataifa kupitia vyombo vya habari.

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, Baraza la Kiswahili limetekeleza malengo yafuatayo:-

i. Mashindano ya tenzi yamefanyika kwa kuwashirikisha waandishi na wasanii wakiwemo mahiri na chipukizi. Jumla ya tenzi zilizokusanywa ni 32, na zawadi kwa washindi zimetolewa katika maadhimisho ya siku ya Kiswahili Zanzibar yaliyofanyika 13/03/2011.

ii. Baraza la Kiswahili limeendelea kuelimisha jamii juu ya matumizi sahihi, fasaha na sanifu ya lugha ya Kiswahili kupitia vipindi vya redio na televisheni pamoja na makala katika magazeti. Jumla ya vipindi 42 vya redio na 42 vya televisheni vimerushwa. Aidha, Baraza limerikodi vipindi vinne (4) vyenye mada za Kiswahili zikiwemo umuhimu wa visawe (maneno yanayokaribiana kimaana) na semi katika kukuza Kiswahili na kufanya mahojiano yanayohusu umuhimu wa Kamusi la Kiswahili Fasaha kupitia Shirika la Utangazaji la Uingereza (*BBC*).

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2011/2012

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Baraza la Kiswahili limepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kushajiisha kuendeleza matumizi ya Kiswahili mkoa, kitaifa na kimataifa.

ii. Kuchapisha makamusi ya lahaja ya Kitumbatu, Kipemba na Kimakunduchi.

iii. Kuandika Kamusi la lugha mbili, Kiingereza - Kiswahili.

Mhe. Spika, ili Baraza la Kiswahili Zanzibar liweze kutekeleza malengo yake ipasavyo, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe Shilingi 90,000,000/= kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012.

BODI YA SENSA YA FILAMU NA SANAA ZA MAONESHO.

Mhe. Spika, jukumu la msingi la Bodi ya Sensa ya Filamu na Sanaa za Maonesho ni kukagua na kuzihakiki filamu na sanaa za maonesho ili kuhakikisha kuwa haziharibu maadili ya jamii zinapooneshwa hadharani na kusikika kwenye vyombo vya habari na rekodi *CD*,*DVD*,na kadhalika. Katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, Bodi hii ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuendelea kutoa elimu na miongozo kwa jamii juu ya uandaaji wa sanaa za maonesho na filamu kwa kutumia semina na vyombo vya habari kuhusu umuhimu wa kutunza na kulinda maadili ya jamii.

ii. Kuendelea kukagua na kuhakiki kanda za sanaa zinazooneshwa hadharani na kwenye matamasha mbali mbali.

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, Bodi ya Sensa na Filamu za Maonesho imetekeleza malengo yafuatayo:-

i. Semina 2 na vikao 3 juu ya elimu na miongozo imetolewa kwa jamii, wasanii, vyombo vya ulinzi, pamoja na kufanya mkutano na Masheha. Aidha, jumla ya vipindi vitano (5) vya Redio vilirushwa kupitia Redio; Zenj FM vipindi vitatu (3), Hits FM kipindi kimoja (1) na Televisheni Zanzibar kipindi kimoja (1).

ii. Bodi imeweza kuzikagua jumla ya Sanaa 6,132 na kuweza kuchukua hatua kulingana na matokeo ya ukaguzi huo. Sanaa zilizokaguliwa (angalia kiambatanisho namba 8).

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Bodi ya Sensa na Filamu za Maonesho imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuhakikisha maadili ya utamaduni wa Zanzibar kwa kuongoza, kusimamia na kukagua kazi za wasanii kwa maendeleo ya utamaduni wa Zanzibar.

ii. Kufanya utafiti juu ya maadili ya kizanzibari na kutumia matokeo ya utafiti huo kwa kuendeleza sanaa yenye maslahi kwa faida ya Wanzanzibari.

Mhe. Spika, ili Bodi iweze kukamilisha shughuli zake, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe shilingi 37,000,000/= kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012.

BARAZA LA SANAA ZANZIBAR

Mhe. Spika, majukumu ya msingi ya Baraza la Sanaa Zanzibar ni kusimamia na kuratibu maendeleo ya shughuli za sanaa Zanzibar. Katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, Baraza la Sanaa lilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kushajiisha wasanii na vikundi vya wasanii katika kuendeleza mila, silka na desturi.

ii. Kuifanyia marekebisho Sheria namba. 6 ya mwaka 1983 ya Baraza la Sanaa Zanzibar na kuandaa kanuni zake.

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, Baraza la Sanaa limetekeleza malengo yafuatayo:-

i. Limeweza kukutana na vikundi vya ngoma na maigizo mara 40 na vikundi vya taarab asilia na kisasa mara 16.

ii. Imeifanyia marekebisho sheria Nam. 6 ya mwaka 1983 ya Baraza la Sanaa Zanzibar na kufikia katika hatua ya Kamati Tendaji.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2011/2012

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Baraza la Sanaa limepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kushajiisha maendeleo ya kazi za sanaa kwa wasanii na vikundi vya sanaa.

ii. Kuendelea kushirikiana na nchi mbali mbali na kubadilishana utaalamu katika fani za sanaa.

Mhe. Spika, ili Baraza liweze kutekeleza malengo yake ipasavyo, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 40,000,000/= kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012.

KITUO CHA AFRIKA MASHARIKI NA KATI CHA UTAFITI WA SIMULIZI ASILI NA LUGHA ZA AFRIKA (*EACROTANAL*)

Mhe. Spika, jukumu la msingi la *EACROTANAL* ni kuwa chombo kikuu cha kupashana habari, kuhifadhi kumbukumbu na kuwa chanzo cha utafiti katika ngazi ya kitaifa na kimataifa kuhusu lugha za Kiafrika na simulizi asili za nchi wanachama ambazo ni Burundi, Comoro, Ethiopia, Madagascar, Mauritius, Msumbiji, Somalia, Sudan na wenyeji Tanzania.

Mhe. Spika, naomba kuliarifu Baraza lako Tukufu kuwa, Kikao cha Wakuu wa *ACALAN* yaani *African Academy of Language* kilifanyika *EACROTANAL* tarehe 15-16/12/2010 kwa kuzishirikisha nchi za Mali, Gabon, Ethiopia, Afrika

ya Kusini, Niger, Cameroon na Tanzania. Maamuzi ya kikao hicho ilikuwa ni kila mjumbe apeleke taarifa katika nchi zao, kuhusu ufufuaji wa kituo hicho.
Mhe. Spika, katika mwaka 2011/2012, Kituo kimepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kwa kushirikiana na wizara inayoshughulikia masuala ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kufuatilia uanzishaji wa Makao Makuu ya Kamisheni ya Kiswahili ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, kazi hii bado inaendelea kufanywa.

Mhe. Spika, ili Kituo kiweze kutekeleza malengo yake, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe shilingi 20,000,000/= kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012.

BARAZA LA TAIFA LA MICHEZO

Mhe. Spika, majukumu ya msingi ya Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar ni kusimamia maendeleo ya michezo yote iliyosajiliwa. Katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, Baraza hili limepanga kutekeleza malengo yafuatayo:

i. Kuwapatia wanamichezo mafunzo ya ndani na nje ya nchi yanayohusu utawala, ualimu na uamuzi wa michezo na kutilia mkazo mialiko ya mechi za kujipima nguvu na mechi za kirafiki.

ii. Kusimamia marekebisho ya Katiba na kanuni za vyama vya michezo pamoja na kukamilisha uchaguzi wa viongozi kwa vyama ambavyo muda wao wa kuongoza umemalizika.

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, Baraza la Taifa la Michezo limefanikiwa kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Zanzibar imeweza kushiriki katika mashindano mbali mbali ya Kitaifa na Kimataifa. (angalia kiambatanisho namba 9).

ii. Baraza kwa kushirikiana na wataalamu wa ndani na nje ya nchi limemudu kuwapatia wanamichezo mafunzo kama ifuatavyo:

- Mafunzo ya Tiba ya Michezo ya kitaalamu kwa madaktari wa michezo, makocha na waamuzi wa michezo.

- Wachezaji wanne (4) wa mchezo wa Judo wamepelekwa kwenye mafunzo ya mchezo huo nchini Japan kwa muda wa miezi mitatu (3).

- Wakufunzi na wanamichezo wa mchezo wa Karati (*Shotokan*) wamepatiwa semina ya siku mbili (2) ya mchezo huo na Mkufunzi kutoka Afrka ya Kusini.

- Baraza kwa kushirikiana na Ubalozi wa Japan nchini Tanzania umewawezesha wachezaji wa mchezo wa Judo kuhudhuria katika mafunzo maalumu ya vitendo yaliyoendeshwa na wakufunzi wanne (4) kutoka Japan yaliyofanyika Dar es Salaam katika Ukumbi wa Don Bosco.

- Baraza kwa kushirikiana na *TOC* iliandaa Mafunzo ya Utawala na Uongozi kwa viongozi wa vyama vitano vya Taifa vya Michezo.

- Baraza limewasaidia walimu wa chama cha kuogelea kushiriki katika mafunzo ya kuogelea yaliyofanyika Dar - es - Salaam na kuendeshwa na mkufunzi kutoka Ujerumani Mr.Gerd Nottelmann. Aidha mkufunzi huyo aliahidi kutafuta kocha atakayekuja kuifundisha timu ya kuogelea ya Zanzibar.

iii. Baraza la Taifa la Michezo limemudu kusimamia marekebisho ya Katiba za vyama vifuatavyo:-

- Chama cha Baskeli (*CHABAZA*), Chama cha Netiboli (*CHANEZA*), Chama cha Riadha (*ZAAA*), Chama cha Mpira wa Wavu (*ZAVA*), Chama cha Mpira wa Magongo (*HOCKEY*), Chama cha Mpira wa Vikapu (*BAZA*), Chama cha Mchezo wa Mapikipiki (*ZAMOCA*) Chama cha mazoezi ya viungo (*ZABESA*) na Chama cha soka (*ZFA*).

- Aidha, limemudu kukamilisha uchaguzi wa Chama cha Baskeli (*CHABAZA*), Mpira wa Magongo (*HOCKEY*),

Mpira wa Wavu (ZAVA) na Chama cha Mpira wa Miguu (*ZFA*). Kwa upande wa Chama cha Mchezo wa Netiboli (*CHANEZA*), Chama cha Riadha (*ZAAA*) na Chama cha Mpira wa Kikapu (*BAZA*) wametakiwa kukamilisha marekebisho ya katiba zao kabla ya kufanya uchaguzi.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2011/2012

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Baraza hili limepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kutilia mkazo ushiriki wa jamii katika michezo kwa kuandaa mabonanza na mashindano ya ndani katika ngazi za shehia, wilaya, mkoa hadi taifa.

ii. Kuimarisha vyama vya michezo katika ngazi zote kwa kuvipatia vifaa vya michezo.

iii. Kuwapatia mafunzo wakufunzi wa michezo mbali mbali kwa kushirikiana na taasisi za michezo za kimataifa.

Mhe. Spika, ili Baraza la Michezo liweze kutekeleza malengo yake, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe shilingi 140,000,000/= kwa matumizi ya kazi za kawaida kwa mwaka 2011/2012.

SHUKRANI

Mhe. Spika, kabla ya kumaliza Hotuba yangu naomba kuwashukuru wote waliochangia katika kuitayarisha hotuba hii. Shukrani za pekee na za utiifu mkubwa zimwendee Rais wetu Mhe. Dk. Ali Mohamed Shein kwa muongozo anaotupa ambao Wizara imeuchukua na kuufanya kuwa ndiyo dira ya utekelezaji wa shughuli zake katika kipindi cha kwanza cha Serikali ya Awamu ya Saba.

Mhe. Spika, shukurani maalumu zimwendee Mhe.Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu,Wakurugenzi wa Wizara yangu na wasaidizi wao wote kwa kufanya kazi kwa juhudi, maarifa na uadilifu mkubwa. Kwa kweli wamekuwa wakinisaidia sana kutekeleza majukumu yetu. Pia nawashukuru Wenyeviti wa Mabaraza na Bodi mbali mbali kwa kusimamia vyema taasisi zetu na kunishauri kwa busara.

Mhe. Spika, naomba kuishukuru Kamati yako ya Mifugo, Uwezeshaji, Habari na Utalii kwa mchango wao mkubwa ulioipatia Wizara baada ya kupitia baadhi ya taasisi zetu na kuona utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Hii imetusaidia sana katika kuiweka vizuri bajeti ya wizara yetu.

Mhe. Spika, naomba kuwashukuru wafanyakazi, wanamichezo, wasanii, wadau wa utalii na wananchi wote wa Unguja na Pemba kwa mchango wao katika kufanikisha shughuli za Wizara. Pia navishukuru kwa dhati vyombo vyote vya habari vya umma na vya binafsi kwa mchango wao mkubwa walioutoa katika kuwahamasisha wananchi kushiriki katika Kura ya Maoni iliyowezesha kutandika mfumo mpya wa uongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye muundo wa umoja wa kitaifa, na baadaye kushiriki kwenye Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, 2010.

Mhe. Spika, nitakuwa mwizi wa fadhila kama sikuishukuru Wizara ya Nchi Afisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa ushirikiano mkubwa iliyotupa kila tulipoikabili kwa mahitaji ya fedha, hasa katika hali ya dharura.

Mhe. Spika, naomba nichukue nafasi hii pia kuzishukuru Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo na Wizara ya Maliasili na Utalii za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa namna tunavyoshirikiana na kufanya kazi kwa pamoja na kwa karibu katika sekta zetu hizi za Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo.

Mhe. Spika, naomba vile vile nitumie fursa hii kuishukuru kwa namna maalumu Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China kwa misaada yao katika sekta ya Habari, Michezo na Utalii. Aidha, nazishukuru Serikali za Misri, India, Korea, Dubai, Iran, Ujerumani, Japani, Uingereza na Marekani kwa mashirikiano na misaada yao ya kitaaluma katika fani ya Habari, Utalii na Michezo. Vile vile napenda kuyashukuru mashirika ya kimataifa ya *UNESCO*, *UNICEF*, *ADB*, *WB*, *UNDP* na *JICA*. Pia, naomba kuzishukuru kampuni za *Zantel*, *Vodacom*, *Tigo* na Shirika la Mfuko wa Taifa wa Hifadhi wa Jamii Tanzania (*NSSF*) kwa kutuunga mkono katika kufanikisha mashindano yetu mbali mbali katika sekta ya michezo na utamaduni.

Mhe. Spika, shukurani za pekee ziende kwa timu yangu ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa kunyakuwa kombe la *NSSF* kwa upande wa Mpira wa Netiboli wanawake, jambo lililoleta faraja kwa Wizara ya Habari na Zanzibar kwa jumla. Aidha, nimpongeze Naibu Waziri wangu kwa kuwa bega kwa bega na wachezaji hao hadi kufikia kupatikana kwa ushindi huo mnono na wa kipekee kwa wizara yangu mwaka huu.

Mhe. Spika, shukurani nyengine za pekee ziende kwa timu ya netiboli Polisi wanawake ya Zanzibar kwa kupata ushindi wa pili katika mashindano ya Klabu Bingwa ya Afrika Mashariki, jambo lililoleta faraja kwa Wizara pamoja na fahari kwa Taifa.

Mhe. Spika, mwisho naomba kukushukuru wewe binafsi, pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kunisikiliza kwa utulivu na uvumilivu. Aidha, natanguliza shukurani zangu kwao kwa michango yao watakayoitoa katika kujadili Hotuba hii. Naamini kabisa michango hiyo itaisaidia sana Wizara yangu katika kutekeleza malengo yake ya mwaka wa fedha wa 2011/2012.

Mhe. Spika, sasa naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya matumizi ya shilingi 6,257,000,000/= kwa kazi za kawaida na shilingi 2,960,000,000/= kwa kazi za maendeleo na makusanyo ya Shilingi 1,212,800,000/= kwa ajili ya kuchangia katika Mfuko wa Serikali kwa Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa mwaka 2011/2012.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

(Saa 1:45 Baraza liliahirishwa hadi tarehe 20/07/2011
saa 3:00 asubuhi)